**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Hamsini na Tatu – Tarehe 29 Juni, 2016**

(*Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi*)

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Maswali!

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana sasa aulize swali lake.

Na. 452

**Nyumba za Kambi ya Polisi Mabatini**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kumaliza ujenzi wa nyumba za kambi ya Polisi Mabatini zilizoanza kujengwa tangu mwaka 2012 na sasa zinazidi kuwa magofu ili zisaidie hizo familia chache zipatazo 13?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nyumba za kambi ya Polisi Mabatini zilianza kujengwa mwaka 2012. Kutokana na ufinyu wa bajeti nyumba hizo hazikuweza kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetenga fedha katika mwaka wa Fedha 2016/2017 ili kukamilisha ujenzi wa nyumba hizo.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza; namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri yaliyonyooka, ningependa sana kujua swali langu la kwanza kwamba, pamoja na fedha zilizotengwa, ni kiasi gani cha fedha hasa kilichotengwa kwa sababu hiyo ingetusaidia kuwa uhakika na hii bajeti kwamba fedha hizi zilizotengwa zitakwenda kukamilisha majengo haya, ili kuwafanya Askari hawa waliosubiri takribani miaka minne sasa walau hizi familia ishirini zipate makazi bora na salama ya kukaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa sababu tunafahamu Nyamagana ndiyo kitovu cha Mkoa wa Mwanza, nyumba hizi zinazotarajiwa kukamilika zinaweza kukidhi mahitaji ya familia zisizozidi ishirini na tano. Ukweli ni kwamba Askari ni wengi na umuhimu wa kambi hii ni mkubwa sana kwenye Mkoa wa Mwanza. Sasa ningependa tu kujua mpango wa Serikali, kuongeza nyumba zingine kwa muda na wakati ili Askari hawa wanaoishi kwenye kambi hiyo ya Mabatini na familia zao ambao sasa ina mwingiliano mkubwa na wananchi wa kawaida waweze kupata makazi mengine bora zaidi ili waweze kuwa kwenye mazingira salama nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mabula kwa jitihada zake za kushughulikia changamoto za Jimbo lake. Tulikuwa pamoja kwenye ziara wakati nilipokwenda kutembelea Nyamagana na alitupa ushirikiano mkubwa sana. Kuhusiana na kiwango ambacho kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizo ni takribani shilingi milioni 565 kwa kuwa nyumba zenyewe zimefika katika hatua ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili alitaka kujua kwamba kwa kuwa hizo ni familia chache ambazo zitakidhi kukaa katika nyumba hizo, kuna mpango gani mwingine nilitaka nimjulishe tu kwamba, tuna mpango wa kujenga nyumba takribani 300 kupitia ile programu ambayo iko katika hatua nzuri za utekelezaji wa ujenzi wa nyumba 4,136 nchi nzima. *(Makofi)*

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa, Jimbo la Mwibara ambalo kwa muda mrefu kulingana na jiografia yake matukio kwenye visiwa ya ujambazi tulishaomba kuwa na Wilaya ya kipolisi. Je, Serikali mpaka sasa ina mpango gani wa kujenga kituo cha Polisi na kutupa hadhi ya Wilaya ya kipolisi. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, upo mpango wa kujenga vituo vya Polisi nchi nzima, ambapo kimsingi tuna upungufu mkubwa wa vituo vya Polisi vinavyokadiriwa kuwa zaidi ya 4,500 nchi nzima ikiwemo eneo ambalo Mbunge amelizungumza. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatambua changamoto ya upungufu wa vituo vya Polisi ikiwemo katika Jimbo lake na tupo katika harakati za kuhakikisha kwamba tunapunguza tatizo hilo katika Jimbo hilo na maeneo mengine ya nchi nzima.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, humu ndani maswali yote huwa yanaelekeza nyumba za Polisi. Je, Waziri anasema nini kuhusu nyumba za Askari Magereza hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli pia tuna tatizo la upungufu wa nyumba katika Jeshi la Magereza. Kama ambavyo ipo katika Jeshi la Polisi, pia iko programu ya ujenzi wa nyumba ambazo zinakwenda sambamba na hizi za Polisi, kwenye Polisi tuna nyumba 4,136 na Magereza tuna nyumba takribani 9,500 kama nitakuwa sijakosewa sawasawa takwimu zake. Kwa hiyo, tunatambua hiyo changamoto na zipo katika hatua nzuri tu za utekelezaji naamini kabisa katika kipindi cha miaka mitano hii, tutaanza kuona miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba hizi pindi mipango ya upatikanaji wa fedha na taratibu za kifedha kupitia Hazina itakapokamilika basi nyumba za Polisi na Magereza kwa pamoja zitakwenda sambamba.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii.

Kwa kuwa, tatizo la Nyamagana la nyumba za makazi ya Polisi linafanana sana na tatizo la makazi kwa Polisi wa Kisiwa cha Mafia. Je, Mheshimiwa Naibu waziri anaweza kulitolea maelezo gani tatizo la makazi kwa Polisi wa Kisiwa cha Mafia? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli lipo tatizo la makazi ya Polisi pia katika Jimbo la Mafia. Nataka tu nimpe taarifa Mheshimiwa Dau kwamba katika ujenzi wa hizi nyumba ambazo

tunataka kujenga, kwa upande wa Pwani tunatarajia kujenga nyumba 150. Mpaka sasa hivi, bado mchanganuo wa ujenzi kwa kila Wilaya ama kila Jimbo haujakamilika. Kwa kuwa, Mheshimiwa Mbunge amelizungumza hilo tatizo la Mafia basi tutalichukua tuone katika ujenzi wa hizo nyumba 150 kwa upande wa Pwani tuone uwezekano wa kuweza kuhakikisha kwamba naamini kabisa Mafia itakuwa imo katika mpango huu, lakini siwezi kuzungumza ni nyumba ngapi kwa upande wa Mafia, hilo tunaweza tukafanya kazi kwa kushirikiana mimi na yeye baadaye.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Mashimba Ndaki kwa niaba yake.

Na. 453

**Hitaji la Chuo cha Ufundi *(VETA*-SIMIYU)**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI (K. n. y. MHE. LEAH J. KOMANYA)** aliuliza:-

Mkoa wa Simiyu hauna Chuo cha Ufundi *(VETA)* na kuwa vijana wengi waliohitimu elimu ya msingi na sekondari:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga chuo cha ufundi ili vijana hao waweze kupata elimu ya ufundi na kuweza kujiajiri?

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mkoa wa Simiyu tayari imeshatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Simiyu, katika bajeti ambayo Waheshimiwa Wabunge waliipitisha ya Wizara yangu, kiasi cha fedha cha shilingi 4,045,000,000 kimetengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya ujenzi huo. Maandalizi ya awali ikiwemo kumpata mshauri elekezi, uandaaji wa michoro pamoja na makadirio ya ujenzi yaani *Bills of Quantities (BOQ)* na kumpata Mkandarasi yanatarajiwa kukamilika ifikapo Novemba, 2016 na ujenzi unatarajiwa kuanza rasmi mwezi Januari, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Simiyu ni kutoa mafunzo ya ufundi stadi na huduma kwa vijana wanaohitimu

elimu ya msingi na sekondari katika Wilaya zote za Mkoa wa Simiyu ili waweze kupata elimu ya ufundi na hivyo kuwawezesha kujiajiri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mashauri, Mashimba Ndaki swali la Nyongeza!

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naitwa Mashimba Mashauri Ndaki hivyo ukisema Mashauri Ndaki bado ni sawa. Niulize swali moja la nyongeza, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa, tuna chuo kizuri cha *VETA* pale Maswa Mjini na kwa kuwa pia, tuna Chuo cha Maendeleo ya Jamii Malampaka, wakati huu ambapo matayarisho ya kujenga Chuo cha *VETA* cha Mkoa yanaendelea, Je, Serikali ina mpango gani wa kuviboresha vyuo hivi viwili ili viweze kuanza kuchukua vijana wakati tunaendelea na mpango wa kujenga Chuo cha *VETA* mkoani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwamba Serikali ina mpango gani wa kuviboresha vyuo vya ufundi vya Malampaka na Chuo cha Ufundi cha *VETA* niseme tu kwamba, Serikali itafanya mapitio ya uendeshaji wa mafunzo ya ufundi stadi nchini. Nimekuwa nikisikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge na maswali ambayo wamekuwa wakiuliza kuhusiana na suala la mafunzo ya ufundi stadi *VETA* ni kwamba, Wizara ya Elimu inaona kuna umuhimu wa kufanya tathmini ya mafunzo ya ufundi stadi yanatolewa katika vyuo vyote nchini kwa lengo la kuangalia upya aina ya mafunzo yanayotolewa, kuangalia teknolojia inayotumika, na niseme tu kwamba hili ni zoezi ambalo baada tu ya kufunga Bunge lako hiyo ndiyo kazi agenda namba moja ambayo tutafanya tathmini kwa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikiwasikiliza sana Waheshimiwa Wabunge michango yao mizuri na maswali yao kuhusiana na *VETA* wamekuwa pia wanahoji kuhusiana na teknolojia, kwa mfano baadhi ya vyuo vya ufundi vinaendelea kutumia labda cherehani za miguu, wakati zimepitwa na wakati kwa hiyo hiyo ni tathmini ya ujumla ambayo itahusisha nchi nzima ikiwa nii pamoja na maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyauliza. Baada ya hapo hatua mahsusi zitachukuliwa katika kuhakikisha kwamba *VETA* zinatoa mafunzo ya kisasa, mafunzo ambayo yanaendana na mahitaji ya sasa hivi ya viwanda tunavyotarajia kuvianzisha. *(Makofi)*

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Sera ya Serikali ni kuwa na chuo cha ufundi *VETA* kila Wilaya lakini hadi sasa ipo baadhi ya Mikoa haina hata chuo kimoja cha ufundi *VETA* kwa mfano Mkoa wa Rukwa.

Je, Serikali ina mpango gani, wa kiuwiano wa kuhakikisha Mikoa yote ambayo haina vyuo vya ufundi *VETA* inapewa kipaumbele kwanza? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba kila Wilaya inakuwa na *VETA* na kila Mkoa inakuwa na *VETA* bado uko palepale. Niseme tu kwamba kwa mfano Mkoa wa Rukwa aliyosema changamoto iko ndani ya Mkoa katika kutoa kiwanja, kwa hiyo tungeomba kwamba zile changamoto ambazo zinajitokeza za upatikanaji wa eneo Mkoa wakamilishe ili ahadi ya Serikali iendelee kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kwa sababu Mheshimiwa Rais ameipatia Wizara yangu, vyuo vya *Folk Development College's* Wizara kama nilivyosema kwenye majibu ya awali itafanya tathmini ya *VETA,* itafanya tathmini ya hizo *Folk Development College's* ambazo ni 53 tumekabidhiwa kwa lengo la kuhakikisha kwamba tutatoa kipaumbele kwenye yale maeneo ambayo yalikuwa hayana vyuo vya ufundi ili kuhakikisha kwamba hii ahadi ya Serikali inatekelezwa kwa vitendo.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa, katika Wilaya ya Mkalama wako wafadhili wa Marekani wanaitwa *Family Community Connection* wana pesa takribani zinazozidi shilingi bilioni moja, wamejitokeza kujenga kituo cha *VETA* Nkungi kwa masharti kwamba Halmashauri ipeleke maji na umeme, na Halmashauri haina pesa. Je, Wizara inasema nini, katika mazingira kama hayo na pesa ziko mkononi?

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningemwomba kama fedha ziko mkononi anikabidhi basi niwe nazo mfukoni, zisiishie kuwa mkononi ziingie mfukoni kwangu. Lakini ningependa tu kusema kwamba kama suala ni upatikanaji wa maji na miundombinu, nadhani hayo ni mambo ambayo yanazungumzika na Wizara yangu haikuwa na taarifa na hili jambo basi atuletee tu rasmi tutalifanyia kazi, lakini naomba hiyo hela ije iingine mfukoni kwa Waziri wa Elimu ili tuweze kufanyia kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, amepotea! Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Karagwe tuna kituo cha ufundi stadi cha *KVTC* Kayanga. Serikali iliandaa mchoro wa kupanua hiki chuo kwa muda mrefu sasa miaka mingi. Ningependa kumuuliza Mheshimiwa

Waziri ni lini Serikali itatenga bajeti kwa ajili ya kupanua hiki chuo cha *KVTC* Kayanga.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba bajeti ya mwaka 2016/2017 Serikali imetenga fedha za kufanya ukarabati wa vyuo viwili. Chuo cha Ufundi Stadi cha Korogwe pamoja na Karagwe kwa hiyo fedha zimetengwa katika bajeti ya mwaka huu. *(Makofi)*

Na. 454

**Kuongeza Thamani kwenye Mazao ya Kilimo na Mifugo**

**MHE. JOHN P. KADUTU (K. n. y. MHE. MAGDALENA H. SAKAYA)** aliuliza:-

Njia pekee ya kuinua uchumi wa Taifa linalotegemea kilimo kwa sehemu kubwa ni pamoja na kuongeza thamani kwenye mazao ya kilimo na mifugo;

(a) Serikali ina Mkakati gani wa kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na mifugo kwenye Mikoa yote ya kilimo na yenye mifugo mingi nchini;

(b) Wafanyabiashara wa mazao ya kilimo na mifugo wanafanya udanganyifu mkubwa wa kujaza magunia lumbesa, kutanua madebe, pia kupima mifugo kwa macho na kwa kupapasa hali inayowaumiza na kuwapa hasara kubwa wakulima. Je, kwa nini Serikali inashindwa kuweka matumizi ya mizani rasmi kwa mazao hapa nchini?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya Mbunge wa Kaliua lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, na Serikali ya India kupitia Mradi wa *Supporting* India *Trade and Investment for Africa (SITA)* imefanya juhudi kubwa kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya nguo na mavazi, ngozi, mafuta ya alizeti na mazao jamii ya kunde. Tayari mikakati ya jinsi ya kuendeleza sekta hizo yenye mipango kamili ya utekelezaji imekwisha andaliwa na utekelezaji wake utaanza mwaka 2016/2017. Aidha, Wizara inapanga kuanzisha makongano ya viwanda katika mikoa ili kuwezesha uzalishaji wa bidhaa. Wizara inahimiza kila Wilaya kuanzisha mitaa ya viwanda vitakavyotumia malighafi zinazopatikana katika maeneo hayo ili kuhamashisha uongezaji thamani katika mazao hivyo kuinua kipato cha wananchi na kukuza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha mapitio ya Sheria ya Vipimo, Sura ya 340 ili iendeane na mazingira ya sasa. Lengo la Serikali ni kumlinda muuzaji kwa kuwadhibiti wanunuzi wanaotumia njia za udanganyifu. Wizara yangu itawasilisha mabadiliko hayo Bungeni mara taratibu zitakapokamilika. Pamoja na marekebisho ya sheria ya vipimo niliyoitaja hapa juu, wakala wa Vipimo imewasilisha mapendekezo Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ya kutungwa kwa sheria ndogo (*By- Laws)* katika Mamlaka za Serikali za Mitaaa zitakazowaongoza wakulima na wafanyabiashara kufungasha mazao yao kwa mujibu wa sheria ya vipimo na kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kurahisisha usimamizi wa matumizi ya vipimo rasmi katika ununuzi wa mazao, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaainisha vituo maalum (*Buying centers)* katika vitongoji nchi nzima na kwa mazao yote na hivyo hakuna mfanyabiashara atakayeruhusiwa kusafirisha mazao ambayo yamefungashwa kinyume na sheria ya vipimo. Aidha, Wakala wa Vipimo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa itaanzisha vituo maalum vya ukaguzi bila kusababisha usumbufu kwa wafanyabiashara. Maafisa Ugani walioko vijijini watumike kusimamia matumizi ya vipimo rasmi katika vituo hivyo na kutoa taarifa zote muhimu kwa wakala wa vipimo.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri wa Wiwanda, ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka ya karibuni viwanda vingi vilibinafsishwa na kuuzwa, vikiwemo viwanda vya mazao ya kilimo na mifugo na kubadilishwa matumizi yake.

Je, Serikali iko tayari kuhakikisha madhumuni ya awali yanatekelezwa kama ilivyoainishwa uko mwanzo?

Swali la pili, kwa vile suala la vipimo vya kienyeji, kama rumbesa na ndoo, maarufu kama Msumbiji limekuwa likilalamikiwa kwa muda mrefu; Je, Serikali haioni kuna haja ya kutoa tamko ni lini hasa wakala wa vipimo na mamlaka za Serikali za Mitaa zitaanzisha hivyo vituo? Ahsante.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya kujenga uchumi wa viwanda, inaendana na utaratibu wa kuhakikisha viwanda vyote vile vilivyobinaifishwa vinarudi kufanya kazi. Wale ambao walipewa viwanda hawakuuziwa walipewa, kwa sababu walilipa kishika uchumba tu, hawakulipa fedha kamili ya kununua kiwanda, ni kwamba wanapaswa wavirudishe. Na napenda nitoe taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba wanaitikia vizuri na wote watakuja kuendesha viwanda kwa misingi

ambayo walikusudia. Atakayeshindwa atanyang'anywa na atapewa Mtanzania mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mkapa, alikuwa na dhamira safi ya kuwapa Watanzania ili kusudi watoke, wajijenge kiuchumi lakini dhamira yake watu wakaitumia vibaya ndiyo hayo wakaenda kutumia viwanda ambavyo havikukusudiwa.

Mhesheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, vipimo aina ya rumbesa, Msumbiji, na wengine wanaita badimanyaira. Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, wameshatoa maelekezo na mtakuta hata njiani, mimi napokea simu nyingi, watu wengi wanakamatwa. Uuzaji wa mazao unakuwa na vituo maalum na Maafisa Ugavi na Watendaji wa Kata, ni moja ya jukumu lao kufika maeneo yale na mnunuzi yeyote hakikisha unapima kilo zisizidi 100. Nitafanya jitihada zaidi kuhakikisha kwamba tunawapelekea mizani kadri tutakapopata uwezo wa kuweza kununua mizani hiyo ili kusudi wananchi pamoja na kupima usawa wa gunia lakini wawe na uhakika kwamba ni kilo 100 tu, wasiwanyonye wauzaji.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mkoa wa Dodoma una mifugo mingi na kunahitajika kiwanda cha kuchakata mazao ya mifugo; Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kiwanda hicho katika Mkoa wa Dodoma?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Toufiq. Mpango wa Serikali ni kujenga viwanda vya kuchakata nyama, huu ni mkakati pamoja na faida ya zao hili la nyama, tunalenga kutumia njia hii kuwashawishi wafugaji waweze kutoa mifugo yao kwenye sehemu za hifadhi. Kwa hiyo Sekta binafsi inahamasishwa na tuna machinjio hapa, tunategemea kutengeneza Kongwa, Ruvu, na tunaimani kwamba kwa kuwa na Kongwa na machinjio ya Dodoma kiwanda kitaweza kutangamka. Lakini nichukue fursa hii kukuomba Mheshimiwa Mbunge, ukimuona Mwekezaji yeyote mwambie aje awekeze Dodoma, mimi ninazo ekari 200, kama anataka kuwekeza aje tushirikiane nitampa eneo, ajenge sehemu ya kuchakatia, machinjio tunayo ni sehemu ya kuchakatika nyama tu.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii.

Kwa kuwa, ndizi ni kati ya zao ambalo linatumika sana nchini lakini kipimo chake kimekuwa na tatizo na wakulima wa ndizi wanapunjika sana zikiwemo

ndizi kama mishale, minyenyele, mlelembo, toke, kitarasa na mtwishe. Mheshimiwa Waziri anatueleza nini kuhusu soko la bidhaa kama hiyo?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ndizi zimenilea, lakini msema kweli ni mpenzi wa Mungu, sijui *international standard* za kupima ndizi, nitakwenda kuwa *task* watu wa *TBS* na watu wa vipimo kusudi tuweze ku-e*stablish* kipimo *standard* cha ndizi. Lakini kitakachoamua bei nzuri kwa mkulima ni soko la ndizi, watu wa (*TAHA*) *Tanzania Horticulture*, chini ya ndugu Jacquline wanatafuta soko la ndizi nje ya nchi, na tumeshapata soko ambalo tunahitaji kuuza nje ya nchi tani 50 kwa wiki. Kwa hiyo tunawasiliana na mama Raymond kusudi tuweze kumuunganisha na Jacquline tuone kama Kilimanjaro mnaweza kulima kusudi kupeleka nje ya nchi.

**MHE. MUSSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru pia kwa juhudi nzuri za Mheshimiwa Waziri anazozifanya katika kuhakikisha kwamba Mikoa ambayo inalima mazao mbalimbali, inakuwa na uwezekana wa kupata viwanda vya ku-*process* hayo mazao. Mkoa wetu wa Tabora una zao la tumbaku, na juhudi ambazo anazifanya Mheshimiwa Waziri tunaziona;

Je, Mheshimiwa Waziri anatuelezaje kuhusu uwezekano wa kupata mwekezaji wa kuja kuweka kiwanda katika cha kuchakata kuchakata zao la tumbaku katika Mkoa wetu wa Tabora?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ambayo ninayahangaikia sana ni kuweza kupata viwanda Tabora. Kwa sababu ameniuliza kuhusu tumbaku nitajibu tumbaku lakini siku nyingine nitakueleza na viwanda vingine ambayo viko kwenye *pipe line*. Tumehangaika, tumewapata Wachina tunawashawishi wakatengeneze kiwanda cha ku-*process* tumbaku pale, lakini panapo majaliwa ya Mwenyenzi Mungu, huenda mwisho wa mwezi huu au mwezi ujao nikaenda Vietnam, nakwenda mahsusi kutafuta kiwanda cha tumbaku na kukipeleka Tabora, kwa hiyo nahangaika jambo la muhimu watu wa Tabora muiombee Serikali hii ili kusudi tuchape kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Emannuel Adamson Mwakasaka Mbunge wa Tabora Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 455

**Kiwanda cha Nyuzi - Tabora**

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza.

Kiwanda cha Nyuzi Tabora hakiendelezwi kwa muda mrefu sasa:-

Je, Serikali itasaidia vipi kumwajibisha mwekezaji wa kiwanda hicho kwa kushindwa kukiendeleza?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Tabotex kilichopo Mkoani Tabora kilikuwa kikifanya shughuli ya usokotaji nyuzi tangu mwaka 1978 chini ya umiliki wa Serikali. Ilipofika mwezi Aprili, 2004. Serikali ilikibinafsisha kiwanda hicho kwa Kampuni za *Noble Azania Investments Ltd* na *Rajani Industries ltd.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa wamiliki, kiwanda hicho kimesimamisha uzalishaji mwaka 2015 kutokana na changamoto ya soko la uzi ndani na nje ya nchi. Aidha, kiwanda bado kina akiba *(stock)* kubwa ya uzi uliozalishwa mwaka 2013, ambao hadi sasa bado unaendelea kuuzwa. Kawaida wanunuzi wakubwa wa uzi ni viwanda vinavyofanya shughuli ya ufumaji vitambaa, lakini viwanda vyote inavyofanya kazi ya ufumaji vitambaa *(weaving)* nchini vikiwemo *21st Century, Sunflag* (*T) Ltd,* Urafiki, NIDA, na Musoma *Textile* vina mitambo yake ya usokotaji nyuzi, hivyo soko la ndani la Tabotex limekuwa likitegemea wafumaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hilo, kiwanda hicho hivi sasa kinatafuta mwekezaji ambaye atakuwa tayari kuingia nacho ubia kwa kupanua wigo wa uzalishaji na kufanya shughuli za ufumaji vitambaa *(weaving)* hadi ushonaji *(finishing)*. Wakati huo huo, kwa kuwa kiwanda hicho ni moja viwanda vilivyobinafsishwa, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea na tathmini ya kiwanda hicho na pindi tathmini hiyo itakapokamilika na tukajiridhisha kuwa mwekezaji huyo hajatimiza matakwa ya mkataba wa Serikali, Serikali itachukua hatua stahiki ambayo itakuwa na faidia kwa Serikali na wananchi kwa ujumla.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Pamoja na majibu mazuri ya Waziri, ninaomba kumuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa kwenye bajeti ya Serikali mwaka huu moja ya vitu vilivyoainishwa mle ni pamoja na kufanya *review* ya mikataba mingi kwa hawa waliobinafsishiwa viwanda. Sasa ni lini Serikali itafanya *review* ya kujua uwezo wa huyo mwekezaji kuhusu kuwekeza Tabora Mjini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kuna tuhuma zinazomuhusu mwekezaji huyo wa kiwanda cha Nyuzi kwamba kuna mashine mbalimbali ambazo aliziuza kama vyuma chakavu, ambazo zilikuwa mle

kwenye kiwanda na kwamba kuna mashine nyingine ambazo tayari zilishasafirishwa, hazipo kabisa pale;

Je, ni lini Serikali itafanya ukaguzi ili kujiridhisha kwamba mwekezaji yule kweli hajaziuza mashine hizo au kuzihamisha nje ya nchi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *review,* sina sababu ya kukuficha, *review* ilishaanza kuhusu Tabotex, nimeshakwenda kumuona hata aliyekuwa Meneja, ambaye sasa hivi ni Meneja Mwatex. Aliyekuwa Meneja wa kiwanda hiki sasa yuko Mwatex Mwanza, nimemfuata nikamuhoji. Ngoja nikueleze, kuna mambo mengine anapoteza muda, kuna majibu amenipa anapoteza muda na iko kwa Msajili wa Hazina na atamshughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu namba mbili, kwamba kuna mashine zimeuzwa, ile tathmini nzima ndiyo itakuja kuhitimisha kwamba alipotoa mashine hii na kuleta mashine nyingine aliitoa kwa misingi gani. Niwaeleze ukweli ambao nimeushuhudia, mitambo ya viwanda vyetu vya nguo, viwanda vingine vilikuwa na mitambo ya mwaka 1963, kwa hiyo mwekezaji makini anapoingia ile mitambo ya mwaka 1963 ataiondoa. Nimeona mashine moja imeagizwa kutoka Swiss, kwenye kiwanda kimojawapo, mashine moja ina uwezo wa kufanya kazi kuliko mitambo 10 ya zamani ukiunganisha. Kama amefanya kwa nia hiyo tutamhukumu kwa alivyotekeleza, lakini kama nilivyosema maslahi yetu ni kwamba kiwanda kifanye kazi, kitoe ajira, kizalishe bidha na hatimaye alipe kodi, akitimiza hayo sina tatizo naye.*(Makofi)*

**MHE.DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona.

Kwa kuwa, tatizo la Tabora linafanana sana na tatizo la Mbeya, mojawapo ya Sera ya Awamu ya Tano ni kufufua na kuimarisha viwanda vya ndani katika kukuza uchumi wa ndani, lakini vilevile kuongeza soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbeya tuna kiwanda cha Mbeya *Textile* ambacho kimetelekezwa kwa muda mrefu sana, ninaomba Mheshimiwa Waziri atuambie nini mkakati wa kiwanda kile cha Mbeyatex ambacho kimetelekezwa kwa miaka mingi sana? Ahsante sana.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kufufua viwanda hasa viwanda vya nguo, siwezi kutoa jibu moja likawaridhisha Watanzania au Waheshimiwa Wabunge, ni mapana ambayo siwezi kuyakumbatia, kufufua viwanda hivi lazima vifufuke. Ukisoma mkakati wa *(C to C) Cotton to Clothing*, unaelezea tutakavyofanya, inaanzia kwa wananchi kulima na Serikali kuwawezesha wananchi kulima. Lakini unakwenda

zaidi mpaka kwa kudhibiti wananchi wanaoagiza nguo kutoka nje ya nchi ambazo ni dhaifu lakini wengine hawalipi ushuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nimeletewa ripoti, *TRA* kuanzia mwezi Januari mpaka mwezi wa Mei, walikuwa wameshindwa kuwakamata watu waliopitisha nguo ambazo hazikulipa bilioni 133. Natoka hapa nakwenda kuripoti kwa Waziri wa Fedha, bilioni 133, nguo zilikuwa *under-valued*, nguo moja nimeoneshwa na wataalam, kilo moja ya nguo ilikuwa imeingizwa nchini kwa kadirio la bei ambayo ni ndogo kuliko pamba, *finishing cloth*, nguo iliyokwisha tengenezwa kilo moja yake ilikuwa imeingizwa nchini kwa thamani ambayo ni ndogo kuliko bei ya pamba ya Mwanza. Sasa mazingira yote kwa ujumla ndiyo yanafanya ufufuaji wa viwanda hivi iwe vigumu, lakini yote hayo tunayamudu, tutayafanyia kazi, Mbeyatex na yenyewe itafanya kazi. *(Makofi)*

**DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa, Mkoa wa Tabora ni kati ya Mikoa ambayo tunalima pamba sana hususan Wilaya ya Igunga, na kwa kuwa miaka ya nyuma tulikuwa na kiwanda hicho cha nyuzi lakini pia tulikuwa na kiwanda cha kuchambua pamba kule Manonga *ginnery* katika Jimbo la Manonga.

Je, Serikali ina mpango gani wa  kufufua hicho kiwanda ili kiweze kulisha kiwanda cha nyuzi cha Tabora?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mwizikulu, Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Uwekezaji na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwa Mheshimiwa Mchungaji Manjelwa, ili Manoga *ginnery* ifanye kazi na Viwanda vya Tabora ni lazima ule mkakati mzima wa kuanzia pamba mpaka nguo upitiwe wote. Kama nilivyoeleza ni pamoja na kuzuia nguo zinazokuja katika ushindani usio sawa. Tukiweza kutekeleza hayo wakulima wakaridhika, hivi viwanda vitafufuka vyenyewe, lakini wale waliokuwa wamepewa na Mheshimiwa Mkapa na awamu zilizopita, wakashindwa kutumia fursa hiyo tutawanyang’anya viwanda hivyo, tutawapa Watanzania wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii ninyi ndiyo wawakilishi wangu, nendeni mkawaambie wananchi anayeona upenyo wowote kwamba mtu anazembea aniletee kielelezo na mimi nitatumia mamlaka niliyonayo kwa kufuata Sheria, tumpe yeye na yeye ajasilie.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri kwamba, nakumbuka ulifanya ziara mkoani Mwanza na ulizungumza na wadau wa pamba. Msimu wa pamba

umeanza Jumatatu, bei elekezi tunaambiwa ni shilingi 1,000, lakini wapo wanunuzi wengine wanasema hawawezi kununua pamba kwa bei ya shilingi 1,000.

Je, nini msimamo wa Serikali kuhusu bei ya pamba, kwa sababu viwanda vyote hivyo Manonga, *MWATEX*, vinahitaji pamba ya kutosha; na ili wakulima wa zao la pamba waweze kulima zaidi lazima bei iwe nzuri, nini msimamo wa Serikali kuhusu bei ya pamba?*(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UFUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya zao la pamba inataka bei elekezi itajwe na Bodi ya Pamba kwa kushauriana na wakulima, wanunuzi na wadau wengine wa zao lenyewe. Hiyo *processes* ilifanyika na hatimaye Bodi ya Pamba ikatangaza bei elekezi ya shilingi 1,000 kwa kilo moja pamba mbegu. Sasa wanunuzi wanayo hiari ya kupima wenyewe, kama hiyo bei wakinunua kwa bei hiyo elekezi au zaidi ya pale, watakuwa na faida katika biashara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuarifu Mheshimiwa Mbunge, kwamba hadi hapa ninapozungumza makampuni nane, yamekwisha pewa *license* ya kununua pamba, na ununuzi wa pamba umeanza. Utaratibu wa msimu wa pamba ni mrefu kidogo, kwa hivyo kwa miaka ya nyuma msimu unapoanza kampuni hizi huwa zinaendelea kupata leseni na kuongezeka kadri msimu unavyokwenda mbele. Kwa hivyo, bei ya pamba ya sasa ni nzuri kwa wakulima, pia baada ya bodi kupitia vizuri ile mjengeko wenyewe wa bei, wana hakika pia itakuwa na manufaa hata kwa wanunuzi wa pamba.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, sasa aulize swali lake.

Na. 456

**Tatizo la Maji - Mji wa Mpwapwa**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Mji wa Mpwapwa wenye wakazi zaidi ya 41,000 unakabiliwa na tatizo kubwa sana la maji, ambapo wananchi wanapata shida kubwa sana kutembea mwendo mrefu zaidi ya kilometa tano kufuata huduma ya maji; na kuna baadhi ya mitambo imeharibika na Mamlaka ya Maji Safi na Salama hawana fedha za kukarabati mitambo hiyo. Je, Serikali haioni kwamba ipo haja kubwa ya kusaidia ukarabati wa mitambo hiyo ili wananchi wa Mji wa Mpwapwa na vitongoji vyake waweze kupata huduma ya maji karibu na makazi yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya ukarabati wa mitambo ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mpwapwa, kwa gharama ya kiasi cha shilingi milioni 24.5. Kazi zilizotekelezwa ni ununuzi na ufungaji wa mota mbili, pamoja na *control panel* ambazo zimebadili kutoka mfumo wa *star delta starter,* kwenda *soft starter,* kwa ajili ya kuendesha mota hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa kazi hiyo mwezi Aprili mwaka 2016, kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka asilimia 59 hadi kufika asilimia 71, kupunguza gharama za uendeshaji pamoja na kuondoa tatizo la kuungua mara kwa mara kwa mota za mitambo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kufanya matengenezo ya mara kwa mara, ili kuhakikisha huduma ya maji katika Mji wa Mpwapwa inakuwa endelevu.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Mtuka samahani mwenye swali alikuwa hajauliza bado maswali ya nyongeza. Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza;

Kwanza ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ni kweli mitambo imekarabatiwa, lakini bado huduma ya maji haiwafikii wananchi wa vijiji vya Ving'awe namba 30, Mbuyuni, Ving'awe Juu, Ilolo, Kwa Mshangu, Mahang'u na Ising'u; kwa hiyo nilikuwa nakupa taarifa tu kwamba maji hayafiki kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni kwamba kuna vijiji ambavyo hakuna uwezekano mwingine wa kupata chanzo cha maji ni kuchimba visima. Sasa naiomba Serikali, kwa vijiji nitakavyovitaja iwachimbie visima ili waweze kupata huduma ya maji. Kwanza Ngalamilo, Mgoma, Mzogole, Kisisi, Godegode, Mkanana, Chamanda, Lupeta, Makutupa, Nana, Simai, Isalaza, Nzonvu pamoja na Iwondo. Naomba sana wananchi hawa wana shida kubwa sana ya maji Serikali iwasaidie. Je, Waziri unasemaje kuhusu hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, la kwanza nadhani lilikuwa ni taarifa, kwa hiyo swali liko moja tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lubeleje babu yangu gereda la zamani huyu, lakini makali ni yale yale, anafanya kazi nzuri sana kwa wananchi wa Jimbo la Mpwapwa.

Mheshimiwa Naibu Spika nikupe taarifa tu kwamba, wiki mbili zilizopita Mheshimiwa Lubeleje, aliondoka na Waziri wangu kwenda Mpwapwa kwenda kuangalia ukarabati wa hizo *starter* na sasa hivi kwa kweli Mpwapwa maji yanapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijiji bado havifikiwi na hayo maji, katika jibu langu la msingi nimesema kwamba Serikali itaendelea kufanya matengenezo na nimuahidi kwenye awamu ya pili ya *program* ya maendeleo ya maji, tutahakikisha kwamba Mpwapwa tunahakikisha vijiji vyote vinafikiwa na maji. Swali hapa muhimu ilikuwa ni kuna vijiji kwa sababu Mpwapwa ni kubwa, kuna vijiji ambavyo bado havijapata huduma ya maji yenye mfumo na ameomba kwamba tuchimbe visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu na Babu yangu Mheshimiwa Lubeleje katika Bajeti ya mwaka huu, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 1.58 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kipaumbele. Kwa hiyo, nikuombe ushirikiane na Halmashauri yako kuhakikisha hivi vijiji, basi mnafanya *study* na mnachimba visima ili mwaka wa fedha utakaofuata, tuendelee kutoa hela kuhakikisha kwamba vijiji vyote vinapata huduma ya maji, kwa maana ya kuchimba visima; lakini ikiwa ni pamoja na kujenga mabwawa ili tuwe na uhakika wa maji katika maeneo ya Mpwapwa.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona, naomba na mimi niulize swali dogo la nyongeza;

Kwa kuwa, Mji wa Manyoni ni mkongwe ni sawa na ule wa Mpwapwa na matatizo ni makubwa, mitambo ya maji iliyopo sasa hivi imezeeka sana. Sasa hivi inakisiwa kwamba asilimia 35 tu ya wananchi wa Manyoni ndiyo wanapata maji na asilimia 65 hawapati maji;

Je, Serikali inatoa kauli gani ya matumaini kwa wananchi wa ule Mji wa Manyoni Mjini, kwa sababu shida ya maji ni kubwa. Maeneo ya Sayuni, Mwanzi, Kipondoda, Mgulang'ombe, Mwembeni, Manyoni Mjini, Majengo hali ni mbaya

akina mama wanapata shida sana, Serikali ina kauli gani kuhusu shida hii ya maji katika Mji wa Manyoni. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji akija kujibu niwashauri tu maswali yale ni vizuri ukaenda moja kwa moja. Ukiliuliza swali hilo hilo mara mbili unamchanganya Waziri anashindwa kujibu umeuliza lipi, la kwanza au la pili kwa hiyo ni vizuri ukaweka swali lako vizuri ili mwishoni ndiyo uliweke swali ili ajue unachouliza ni nini, ukiuliza mawili na ni swali la nyongeza unamchanganya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji jibu swali moja kati ya hayo mawili yaliyoulizwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIJAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumeishaelekeza kwamba sasa hivi katika awamu ya pili ya *program* ya maendeleo ya maji, tutahakikisha kwamba miundombinu ya zamani inafanyiwa utafiti, tunatoa fedha na tunakarabati ili mfumo wa maji ule uweze kuendelea. Pamoja na kukarabati tutapanua kwa sababu katika hayo maeneo kwa mfano, kama mtambo ulijengwa muda mrefu miaka ya 1960 au 1970 wakati ule wananchi walikuwa ni wachache, sasa hivi wananchi wameongezeka, huduma za binadamu vilevile zimeongezeka kwa hiyo mahitaji ya maji yameongezeka. Hivyo, pamoja na kukarabati hiyo mifumo tutahakikisha tunaipanua ili kuhakikisha kwamba huduma ya maji inakuwa ya kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane pamoja na Halmashauri yako, ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa kuchimba mabwawa. Kama vile Itigi Serikali imekamilisha bwawa na ninayo taarifa bwawa hilo linavuja na nimeishaelekeza kwamba wataalam waende kuhakikisha wanaziba ili tuwe na maji ya kutosha.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Kwa kuwa, matatizo yaliyoko Mpwapwa yanafanana sana na matatizo yaliyopo katika Jimbo langu la Itigi. Watu wanaenda kilometa nyingi sana kufuata maji hasa katika vijiji vya Rungwa, Kintanula, Kalangali, Mitundu, Chabutwa na Mabondeni;

Je, Serikali itasaidiaje kutatua tatizo hili katika Jimbo la Manyoni Magharibi;

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha *program* ya utekelezaji wa maendeleo ya maji, iliyodumu kuanzia mwaka 2006/2007 mpaka 2015. Sasa hivi tumeingia katika *program* ya

pili. Huu ni mwendelezo wa kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanapata huduma ya maji iliyo safi na bora, na kusogeza huduma ya maji iwe karibu ili akina mama wasitumie muda mrefu kupata maji.

Mheshimiwa Yahaya Masare nikuhakikishie kwamba tunaendelea na kama ambavyo umeona katika Bajeti ya mwaka huu tumehakikisha kwamba kila Halmashauri imetengewa fedha, tutaendelea kupeleka wataalam na tutasimamia tuhakikishe kwamba fedha hii inatumika. Sheria ndogo ndogo imepitishwa tumeweka *value for money,* tuhakikishe kwamba hela iliyopelekwa inafanya kazi nzuri na kuhakikisha wananchi wanapata maji.

Hivyo, nikuhakikishie kwamba tutatenga fedha kila mwaka, kuhakikisha kwamba wananchi wako wa maeneo hayo mpaka ya Rungwa wanapata maji. *(Makofi)*

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii.

Matatizo ya Mamlaka ya Maji ya Mji wa Mpwapwa yanafanana na matatizo ya Mamlaka ya maji ya Mji wa Mwanuhuzi. Mradi wa Mamlaka ya Maji ya Mji wa Mwanuhuzi ulikamilishwa mwaka 2009 na ukakabidhiwa katika Mamlaka ya Maji Mwanuhuzi. Mradi huu ulilenga kusambaza maji katika vijiji Nane lakini ni vijiji Vitatu tu vilisambaziwa maji; na kusababisha *qubic* mita za ujazo wa maji, ambayo yanatumika ni moja ya tatu tu, na hivyo gharama ya uendeshaji katika Mamlaka ya maji kuwa juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishiriki katika Bajeti ya mwaka huu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, naomba uulize swali tafadhali.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri haikuwa na fedha kwa ajili ya upanuzi wa mradi huu, kwa sababu fedha iliyokuwepo ilikuwa ni kwa ajili ya Mkandarasi mshauri wa vijiji 10;

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kusambaza maji katika vijiji vilivyobaki vya Bulyanaga, Mwambegwa, Mwagwila, na Mwambiti ili wananchi waweze kunufaika na mradi huu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze yeye ni Mama anajua matatizo ya maji, kwa hiyo ufuatiliaji wake ni kwamba unamgusa moja kwa moja. Ametoa taarifa kwamba kuna mradi ulikamilika lakini umehudumia vijiji vichache. Mheshimiwa Leah Komanya, naomba sana ushirikiane na Halmashauri; kwa sababu mwaka huu tumetenga fedha kwa kila Halmashauri, kuhakikisha kwamba hayo maeneo ya vijiji

yaliyokuwa yamekosa kupata maji basi muhakikishe kwamba nayo yanapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama kuna tatizo la utaalam, Mheshimiwa Komanya, naomba utakapokuwa umefika kule na mmepata shida ya wataalam basi tuwasiliane ili tuweze kushirikiana kuleta wataalam atuweze kufikisha huduma hiyo hapo. Suala la nyongeza ni kwamba hii Mwanuhuzi iko Mkowa wa Simiyu, na Mkoa wa Simiyu tuna mradi mkubwa ambao utachukua maji kutoka ziwa Victoria, usanifu sasa umekamilika; na wakati wowote tutakamilisha taratibu ili kuhakikisha kwamba Mkoa wote wa Simiyu sasa tatizo la maji tunaliondoa.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa sababu tatizo la Mpwapwa linalingana kabisa na tatizo kubwa la Makambako. Mji wa Makambako una wakazi wengi zaidi ya laki moja, na tatizo la maji ni kubwa sana. Wananchi wa Mji wa Makambako alipopita Mheshimiwa Dkt. Magufuli kipenzi chao na kipenzi cha watanzania, walimueleza tatizo la maji katika Mji wa Makambako, kuna mradi ambao ulishasanifiwa wenye gharama ya zaidi ya bilioni 57, na Waziri wa Maji ambaye yupo sasa alikuwepo siku hiyo wakati anaahidi.

Je, sasa tatizo hili la mradi mkubwa wa bilioni 57 litatatuliwa lini ili wananchi wa Makambako waendelee kupata maji. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Sanga kwa ufuatiliaji wake. Maana yake pamoja na kufuatilia miradi midogo midogo ya Halmashauri ya Makambako, lakini bado kumbe amesoma na nyaraka za mradi mkubwa unaolenga kutoa maji Mto Tagamenda, kuhakikisha kwamba maji yanapatikana katika Mji wa Makambako. Lakini nikufanyie marekebisho kidogo kwamba, mradi huo unatarajia kugharimu dola milioni 32.9 na Serikali yako Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo mwenyewe uliwashawishi wananchi wako wameichagua, ilipeleka andiko Serikali ya India, na nisema tu kwamba Mheshimiwa Sanga unawaisha shughuli, tunatarajia ifikapo tarehe 15 mwezi Julai, mwezi tunaouanza kesho kutwa mambo yanaweza yakaiva kutoka Serikali ya India na tayari tukaanza na taratibu ya kutekeleza huo mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, nikuhakikishie pamoja wananchi wa Mji wa Makambako, na hasa kwa kuzingatia kwamba ndugu yangu Sanga wewe ni shemeji yangu, kwa hiyo maji utapata.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, sasa aulize swali lake.

Na. 457

**Serikali Kuwapa Maeneo Wachimbaji Wadogo**

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawapa maeneo ya uchimbaji wachimbaji wadogo wa Kata za Nyarugusu, Nyaruyeye na Kaseme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2001 Wizara ilitenga eneo lenye ukubwa wa hekta 533.55 kwa ajili ya wachimbaji wadogo katika eneo la Nyarugusu. Pamoja na hatua hiyo, wachimbaji wadogo wameendelea kuomba kumilikishwa maeneo hasa ya Buziba yanayomilikishwa na Kampuni ya *Buckreef Gold Ltd*, kupitia leseni namba *PL* 6545/2010. Leseni hii itaisha muda wake tarehe 11 Julai, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Nyaruyeye na Kaseme pia yana leseni hai ya utafutaji wa madini yenye leseni RL 0007/2012 ya Kampuni ya *ARL* ambayo pia itaisha muda wake tarehe 20 Septemba, 2017. Kwa sasa Serikali inafanya mazungumzo na kampuni hizo ili kuona uwezekano wa kuachia maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea na utaratibu wa kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za wachimbaji wadogo hapa nchini. Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)* wanaendelea kutathmini maeneo mbalimbali ili kuona kama maeneo hayo yana mashapo ya kutosha kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Aidha, Serikali itaendelea kujadiliana na kampuni zinazomiliki leseni za madini kwa wachimbaji hapa nchini kwa ajili ya kuwagawia wachimbaji wa maeneo ya Nyarugusu, Nyaruyeye pamoja na Kaseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, katika kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo, vigezo vinavyozingatiwa ni pamoja na uwepo wa eneo lililo wazi kwa ajili ya kuwagawia wachimbaji kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, swali la nyongeza!

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Ni kweli kwamba Serikali imeweza kujibu kwamba itawapa maeneo wachimbaji wadogo katika maeneo hayo, lakini imekuwa ni ahadi ya muda mrefu sana hasa katika eneo la Nyarugusu maeneo ya *STAMICO*, kila wakati Serikali imekuwa ikiahidi kwamba itawapatia maeneo na wananchi wanahitaji kujua kwamba ni lini sasa Serikali itawapatia maeneo haya ya wachimbaji wadogo hasa maeneo ya Nyarugusu? *(Makofi)*

Swali la pili, mwaka 2015 Serikali ilizindua mradi mkubwa sana wa wachimbaji wadogo pale Rwamgasa na tuliuzindua mradi huu kwa vigelele na shangwe, lakini sasa hakuna kinachoendelea mpaka sasa. Ni mradi wa *World Bank*! Napenda kujua, ni lini sasa mradi huu utaanza rasmi ili wachimbaji wadogo waweze kunufaika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Serikali imekuwa ikikusudia kuwatengea maeneo wananchi, hasa wa eneo la Mheshimiwa Bukwimba. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Bukwimba, amekuwa akifuatilia sana maeneo ya wachimbaji wadogo katika eneo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimkumbushe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, mwaka 2015 kwa juhudi zake ambazo aliomba wananchi wachimbiwe maeneo, walitengewa maeneo 95, eneo la Rwanyamgaza. Kadhalika, maeneo ya Kaseme, walitengewa maeneo 43.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba tu Mheshimiwa Bukwimba awahamasishe wananchi, kwa sababu kati ya maeneo 95 aliyotengewa, ni maeneo 25 tu kule Rwanyamgaza yanafanya kazi; na kati ya maeneo 43 kule Kaseme ni maeneo 17. Hata hivyo Mheshimiwa Bukwimba kwa juhudi zako bado tunakutengea maeneo mengine ambayo yanaachiwa wazi na wananchi hasa eneo la Buziba. Buckreef itaachia hekta 200, lakini bado Kampuni ya *ARL* itaachia hekta 100; bado Kampuni ya Bismak itaachia hekta 120, lakini na Ernest Masawe ataachia hekta 90, hiyo ni kwa ajili ya wananchi wako Mheshimiwa Bukwimba. Kwa hiyo, bado tunakutengea maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini sasa? Mwezi wa Kumi tunaanza kutenga maeneo rasmi. Hii ni kwa nchi nzima ikiwemo eneo la Igunga kule Iborogero, maeneo ya Kibao kwa Mfipa, maeneo ya kule Mkuranga kwa ajili ya Waziwazi

lakini na maeneo mengine ya Busiri, pamoja na Londani Sambalu kule Singida kwa Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, bado tunaendelea kutenga maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala lake la pili ni kwamba Kituo cha Kuchenjua Madini kwa ajili ya wachimbaji wadogo, kimechukua muda mrefu. Mheshimiwa Bukwimba nakupongeza sana, tuna kituo kimoja tu cha mfano cha kuchenjua madini hapa nchini na ndiyo kituo cha Rwamgasa ambao Mheshimiwa Bukwimba, mwaka 2015 na mwaka 2014 ulihangaika sana. Mheshimiwa Bukwimba nakupongeza sana, utakuwa ni Mbunge wa mfano kwa sababu ndiyo eneo tunalofungua Kituo cha Kuchenjua cha Mfano hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini kinakamilika sasa? Leo tumefungua tenda kwa ajili ya kumpata mjenzi na kazi ya kujenga itaanza mwezi Septemba mwaka huu na mradi ule utakamilika mwezi Mei mwakani. Gharama yake ni hela nyingi kidogo, ni Dola 800,000, tutazitenga ili kituo hiki kianze kufanya kazi. Pia nawapongeze mgodi wa GGM nao wanachangia Dola 200,000. Kwa hiyo, kituo hiki kitaanza kufanya kazi lakini mantiki ya kituo hiki kitasaidia sana wachimbaji wadogo kujua thamani sasa ya dhahabu wanayochimba hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawahamasisha wananchi wote ambako madini yanachimbwa sasa wote tupeleke kwenye eneo hili la Rwamgasa ambacho Mheshimiwa Bukwimba amekifungua ili wananchi wetu sasa wanufaike na rasilimali yetu ya dhahabu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa Moses, swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri utakapokuja kujibu, sina hakika kama una sifa za kila Mheshimiwa Mbunge atakayekuuliza swali. Mheshimiwa Ikupa Moses. *(Kicheko)*

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Naitwa Ikupa Alex, samahani. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, wachimbaji hawa wadogo nchini ni muda mrefu sasa wamekuwa wakikumbwa na migogoro ya mara kwa mara na wachimbaji wakubwa hasa kule Mererani. Je, Serikali ina mpango ama mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inatatua migogoro hii na kuhakikisha kwamba haijirudii tena? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa wachimbaji wadogo wadogo na siyo Mererani peke yake ni kote nchini, wamekuwa wakikumbwa na migogoro hasa kati yao na wawekezaji wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mererani, kwanza kabisa kuna migogoro ya aina mbili; iko migogoro ya wao kutoboza chini kwa chini kuingia kwenye mgodi wa *Tanzanite One* ambao ni mgodi mkubwa kwa ajili ya kuchukua kidogo *Tanzanite*. Huo mgogoro tunashughulika nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wachimbaji wa Mererani wana maeneo madogo, lakini hatua tuliyofikia sasa ni kuwatafutia maeneo wananchi wa Mererani ili wachimbe karibu na eneo la mgodi ule kwa sababu na kwenye kuna *Tanzanite* ya kutosha. Hiyo ni hatua ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya tatu, mgogoro ambao sana sana ni wa kiufanyakazi, ni mgogoro kati yao na waajiri wao. Mgogoro huu tunawasiliana kwa ukaribu sana na Wizara ya Kazi. Mwezi uliopita tulikaa kama Kamati na kusuluhisha mgogoro huo. Kwa sasa tunaamini kwamba wananchi wa Mererani kwa sababu watapata maeneo yao na taratibu za ajira zitazingatiwa. Kwa hiyo, matatizo sasa ya mgogoro kati yao na wachimbaji wakubwa zinakoma mara moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTATINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Wakati wa kampeni tulihamasisha sana vijana kujiunga kwenye *SACCOS* ili baadaye waweze kupatiwa maeneo ya uchimbaji wa madini. Nataka kufahamu Mheshimiwa Naibu Waziri anawaahidi nini vijana waliolundikana kwenye maeneo ya Samina, Mgusu, Nyakabale kwamba watapata lini maeneo hayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa wananchi wa Kasema, Wanela pamoja na eneo la Geita Mjini, lakini siyo Geita Mjini tu, Nyakabale na maeneo mengine wanahitaji maeneo. Namhakikishie Mheshimwia Constantine kwamba mwaka huu tumetenga hekta 12,000 na kati ya hizo, hekta 2,000 ni maeneo ya Geita kwa hiyo wananchi wa Nyakabale, wananchi wengine wa Mtakuja na wengine ambao walikosa mgao wa Geita watapata maeneo ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, kwa Mkoa wa Geita, mwaka 2015 na mwaka 2014, kuna *SACCOS* sita zilizoundwa. *SACCOS* mojawapo ambayo haijapata eneo la uchimbaji, ni pamoja na wakeretwa wa *SACCOS* ambayo ilipata lesseni tano; lakini Tupendane *SACCOS* walipata ekari sita pamoja na Tunakuja *SACCOS* walipata ekari nane; Ujamaa *SACCOS* kwa sababu zote zinatoka Geita walipata ekari tisa, pamoja na Mapinduzi *SACCOS*.

Kwa hiyo, wananchi wote wa Geita tunaomba wajiunge na *SACCOS* ili kusudi tuendelee kuwagawia maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Constantine sana kwamba, ningependa sana waanze kuziunda *SACCOS* sasa hivi, kwa sababu utaratibu sasa wa kuwatengea maeneo unaanza mwezi wa Kumi mwaka huu. Kwa hiyo, tunaomba sana *SACCOS* zote na siyo kwa Geita tu, ziwe tayari ili kuanzia mwezi wa Kumi waanze kugawiwa pesa. Hata hivyo, tumewatengea ruzuku sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge walipitisha shilingi bilioni 6.68 kwa ajili ya ruzuku ya wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, pamoja na kuundwa *SACCOS,* lakini pia tutawagawia ruzuku kwa ajili ya kuendeleza uchimbaji wao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza!

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Rais alipokuja mwaka 2015 kwenye mikutano yake ya kampeni katika Jimbo la Nyang'hwale, aliweza kuwaahidi wachimbaji wadogo wa Jimbo hilo kwamba eneo la Kasubuya litapimwa na kugawiwa wachimbaji wadogo wadogo. Je, Serikali inasemaje kwa hili kwa wachimbaji wadogo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kati ya maeneo 12 tuliyotenga kwenye Mkoa wa Geita pamoja na maeneo mengine ya Kahama ni pamoja na eneo la Kasubuya. Eneo la Kasubuya tumetenga hekta 4,098.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Hussein, wananchi wa Nyang'hwale tayari wana eneo. Isipokuwa nawaomba sana, hata wakishindwa kupata maeneo pale Kasubuya, tunatenga maeneo mengine. Kule Chato kuna hekta 1,282. Kwa hiyo, wananchi wako bado wanaweza kwenda kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maeneo yale, maeneo ya kwa Mheshimiwa wa Mbunge wa Bukombe tuna hekta 682, wanaweza wakaenda kuchimba Bukombe. Kwa hiyo, tunaendelea kutenga maeneo ili wananchi wa Kasubuya na maeneo mengine wapate maeneo ya kutosha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Gibson Ole-Meiseyeki, Mbunge wa

Arumeru Magharibi. Swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu.

Na. 458

**Barabara ya Lami Kuunganisha Arusha – Simanjiro – Kongwa**

**MHE. ZAYNAB M. VULU – (K.n.y. MHE. GIBSON B. MEISEYEKI)** aliuliza:-

Mkoa wa Arusha na Wilaya ya Simanjiro ni maeneo yanayotegemeana sana kiuchumi lakini hayana barabara ya kuwaunganisha kiuchumi:-

Je, ni lini Serikali itayaunganisha maeneo haya ya Arusha, Simanjiro, Naberera, Kibaya – Kongwa kwa barabara ili kuimarisha maendeleo ya kiuchumi katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gibson Ole Meiseyeki, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa barabara ya Arusha – Simanjiro – Kibaya hadi Kongwa yenye urefu wa Kilomita 434 ni muhimu kwa shughuli za kiuchumi, kwani inapita katika maeneo muhimu ya uzalishaji wa kilimo, madini, ufugaji na utalii na pia inaunganisha mikoa mitatu ya Arusha, Manyara na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hiyo, Serikali imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Arusha – Simajiro – Kibaya hadi Kongwa yenye urefu wa Kilomita 434 ili hatimaye iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Aidha, shilingi milioni 521.3 tayari zimetengwa na kiasi cha shilingi milioni 350 zimeombwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya kuanza taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata mhandisi mshauri wa kufanya kazi hiyo ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Mara baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, Serikali itatenga fedha za kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mipango hiyo na kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Serikali imekuwa ikitenga fedha za matengenezo kila mwaka ili kuhakikisha inapitika majira yote ya mwaka. Kuanzia mwaka wa

fedha 2013/2014 hadi 2015/2016, jumla ya shilingi 4,383,895,000/= zilitengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hii ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nami naomba niulize maswali mawili ambayo yanafanana na barabara ya Arusha - Simanjiro. Kwa kuwa barabara ya kutoka Mkuranga hadi Kisiju ilikuwa ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne na Awamu ya Tano, kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami na kwa kuwa hadi leo hii wananchi wa Wilaya ya Mkuranga na Wilaya ya Mafia wanaitegemea sana barabara hiyo: Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Swali la pili; kwa kuwa katika Kisiwa cha Mafia wananchi wake wanapata shida sana ya usafiri wa kutoka Mafia hadi kwenda nchi kavu ambayo ama ni Bandari ya Kisiju ama Bandari ya Nyamisati, lakini pia bado wana matatizo ya barabara za lami katika kisiwa hicho. Je, Serikali haioni sasa ni vyena ikatimiza ahadi yake ambayo ilitolewa na Rais ya kujenga barabara kuanzia Kilindoni hadi Rasinkumbi?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara ya Mkuranga hadi Kisiju ilitolewa ahadi na Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa kuanzia Rais wa Awamu ya Nne na sasa Rais wa Awamu ya Tano. Naomba nichukue fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Vulu, kama ambavyo tumekuwa tukiongelea hili suala mbele ya Waziri wangu, nami nampongeza sana kwa juhudi hizo za kufuatilia hizi barabara pamoja na mwenzake kwamba barabara hii kama ambavyo tumemwahidi tutaijenga kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidiwa na Viongozi wetu Wakuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la lini tutaanza, naomba Mheshimiwa Zaynab Vulu utupe muda, maana yake tuna miaka mitano, ndiyo tumeanza tu, nikuhakikishie katika kipindi hicho ambacho kazi yetu kubwa itakuwa ni kuwajengea miundombinu Watanzania, tutahakikisha tunakupa jibu kamili la lini tutaanza kwa vitendo kwa maana ya kupitia bajeti zinazokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la pili la kuhusiana na barabara inayoanzia Kilindoni ambayo ni sehemu muhimu sana ya kuunganisha mawasiliano kati ya wenzetu wa Mafia pamoja na Kisiju, naomba nayo nikuhakikishie kwamba tutaijenga kwa kiwango cha lami kama ambavyo imeahidiwa na unafahamu kwamba barabara hii kwa pale Mafia tumeashaanza sehemu kuijenga, tutahakikisha tunaikamilisha kujenga na hatimaye wananchi waweze kunufaika na matunda mazuri ya Serikali ya

Awamu ya Tano aliyoiweka madarakani ikiongozwa na Jemedari, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwenye nia ya dhati ya kuwasaidia watu wenye kipato cha chini ili waweze kuinuka na kupata maisha mazuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Umbulla, swali la nyongeza!

**TAARIFA**

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa. Naomba nitoe taarifa, Mheshimiwa Naibu Waziri afanye masahihisho kwa ajili ya *Hansard*. Hakuna barabara inayotoka Kilindoni hadi Kisiju. Kutoka Kilindoni hadi Kisiju ni bahari, kwa hiyo, ni kutoka Kilindoni hadi Rasinkumbi. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Nadhani Mheshimiwa Zaynab Vulu, kwa sababu ulikuwa unamkumbusha Waziri barabara inapita wapi, nadhani ameshaipata hiyo taarifa. Mheshimiwa Martha Umbulla, swali la nyongeza!

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa maeneo yaliyotajwa kwenye swali la msingi, Naberera iko Simanjiro na Kibaya iko Wilaya ya Kiteto na ni maeneo yanayozalisha sana mahindi hapa nchini, kwa hiyo, ni maeneo muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu, lakini hakuna barabara hata moja inayounganisha hata na Makao Makuu ya Mkoa ambayo ni Babati na barabara zake ni za vumbi na hivyo zinaharibika sana kwa ajili ya kubeba mahindi nyakati za mvua.

Je, Serikali ina mikakati gani sasa kwa umuhimu nilioutaja kuhakikisha kwamba angalau kuna barabara hata moja inayounganisha maeneo hayo muhimu kwa uchumi na Makao Makuu ya Mkoa wa Babati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda unipe fursa, katika swali lililopita nilisema barabara inayoanzia Kilindoni na wakati huo tunaongelea mawasiliano kati ya Mafia na Kisiju. Sikuongelea barabara kutoka Kilindoni kwenda Kisiju. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye kumbukumbu, *Hansard* nadhani zitakuwa zimesema sahihi. Nilikuwa naunganisha usafiri kati ya Mafia na Bara, Kisiju wakati huo tunaongelea barabara ya Kilindoni inayoanzia Kilindoni, ambayo sasa amesema inaishia Rasinkumbi na hiyo barabara tumeanza kuijenga. Nilitaka tu niliweke sawa ili liweze kueleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje kwenye barabara ya kutoka Naberela hadi Kiteto. Naomba kuchukuwa fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikai hii ya Awamu ya Tano tuna dhamira ya dhati ya kuhakikisha Mkoa wa Manyara nao unaingia katika ramani ya barabara za lami ukiacha ile Barabara Kuu ambayo inatoka Arusha kupitia Babati na kuja Singida. Nako huko tunaingiza katika ramani ya barabara za lami. Nimhakikishie kwamba hii barabara ambayo nilijibu katika swali langu la msingi kwamba, tunaanza kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, hii inayopita Kiteto kwenda Arusha na inayounganisha Mkoa wa Dodoma, hiyo nao ni sehemu ya kuhakikisha Mkoa wa Manyara tunaufungua katika kuuwekea barabara ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika miaka hii mitano tutafanya kazi ya uhakika kuhakikisha eneo hili tunaliweka sawa na tunajenga baadhi ya barabara ambazo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi tulishaainisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Alex Gashaza, kule nyuma!

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, barabara ya Mrugarama – Rulenge kwenda mpaka Mzani iko kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kujengwa kwa kiwango cha lami, lakini kwa mwaka wa fedha 2016/2017 haiko kwenye bajeti, badala yake ni Kilometa tatu na nusu tu ambazo zimewekwa kwenye bajeti kwa ajili ya kiwango cha changarawe chini ya *TANROAD;* na barabara hii imekuwa mbaya sana kwa kipindi kilichopita cha mvua na mwaka mzima maana yake hakuna bajeti nyingine itakayotengeneza barabara hii:-

Je, Waziri haoni umuhimu wa kuongeza fungu ili kwa kipindi cha mwaka wa 2016/2017, barabara hii iweze kupitika kwa wepesi japo itakuwa imetengenezwa kwa kiwango cha changarawe? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gashaza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wa kuongeza bajeti sina kwa sababu nina uhakika huu mwaka ndiyo tumemaliza, mmetupa kazi, mmepitisha bajeti yatu na tunawahakikishia sisi tutaisimamia kwa nguvu zetu zote. Kitu ambacho ninamhakikishia, tutahakikisha hii barabara aliyoiongelea, inapitika mwaka mzima. Kama itatokea mahitaji makubwa ya fedha kutokana labda na kuharibika kwa kiwango ambacho hakitegemewi, namhakikishia kwamba tutatafuta fungu la dharura ili kuweza kurudisha mawasilino kama yatakatika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mawasiliano yatakuwepo katika kipindi chote cha mwaka wakati tukijiandaa na bajeti ya miaka inayokuja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stephen Ngonyani, swali la nyongeza!

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Tanzania nzima ili iwe barabara ni lazima kuwepo na madaraja. Katika Wilaya yangu ya Korogwe Vijijini wakati wa mvua barabara za Mkoa zote zimevunjika madaraja na hakuna magari yanayoweza kupita katika barabara ya Mkoa kutoka Korogwe kwenda Mnyuzi kwa kupitia Muheza; na barabara ya kutoka Korogwe kwenda Magoma kwa kupitia Maramba hadi Daruni.

Je, Serikali hamna mpango wa dharura kutusaidia madaraja haya ambayo wananchi wamepata taabu kwa muda mrefu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilishasema huko nyuma kwamba baada ya mvua kwisha kipaumbele cha kwanza ni kufungua mawasiliano katika yale maeneo ambayo yalikuwa yamekatika na tulishawaelekeza viongozi wa *TANROAD* Mikoani kwamba wahakikishe tunafungua mawasiliano pale ambapo yalikatika. Naomba Mheshimiwa Stephen Nganyani tuwasiliane pamoja na *TANROAD* Mkoa ili tuone kitu gani kinaweza kufanyika kutekeleza kile ambacho nilikisema humu Bungeni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 459

**Bandari ya Karema**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa Bandari ya Karema na ina mikakati gani na Bandari hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa awali wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* ulikuwa wa kujenga gati dogo kwa ajili ya kuhudumia abiria wanaozunguka eneo la Karema. Hata hivyo, kutokana na mpango wa Serikali wa kuboresha Reli ya Kati ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Reli ya Kaliua – Mpanda – Karema yenye urefu wa kilometa 360 ambayo kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea, *TPA* imelazimika kuboresha mpango wake kwa kujenga bandari badala ya gati ili kukidhi matarajio ya shehena ya kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo itakayopitia Bandari hiyo ya Karema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ipo katika hatua za mwisho za kumpata Mshauri Mwelekezi atakayefanya upembuzi yakinifu wa mradi huu ambaye anatarajiwa kuanza kazi ifikapo Juni, 2016 na kukamilika mwezi Desemba, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongezee kusema kwamba, hiyo kazi imeshaanza. Aidha, baada ya kupokea taarifa ya upembuzi yakinifu, *TPA* itatangaza zabuni kwa ajili ya kuwapata wajenzi ambapo kazi ya ujenzi wa Bandari ya Karema unatarajiwa kuanza katika mwaka fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Karema wavute subira, kwani Serikali yao imedhamiria kujenga bandari hiyo ambayo itakuwa ni kichocheo muhimu cha ukuaji wa uchumi wa wananchi wa Karema na Taifa kwa ujumla.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anna Lupembe, swali la nyongeza.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ilitumia pesa nyingi sana kwa ajili ya gati na kwa kuwa Serikali ilijenga majengo, mpaka sasa hivi yale majengo yamekuwa magofu na Wananchi wa Karema wamepoteza imani kabisa na Serikali kwa kwasababu walilia sana gati hili na wakalikosa mpaka sasa hivi:-

Je, ni lini sasa Serikali itaweka imani kwa wananchi wa Karema?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa, tulikuwa tuna mpango wa gati na tumetumia pesa nyingi, majengo yale yapo hayana kitu chochote, popo tu wanaingia na sasa tuna mpango wa bandari:-

Je, Serikali inaweka mikakati gani, kwa kuwa inatumia pesa nyingi na kupoteza kujenga bandari hii na wananchi wa Karema wawe na matumaini?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ambayo ilishaanza kufanyika wakati tulikuwa tunategemea kujenga gati, siyo kwamba imepotea, hapana. Tunapojenga bandari haina maana ile kazi yote iliyofanyika wakati tunajiandaa kukamilisha ujenzi wa gati inapotea. Hayo majengo bado yatatumika na kwa hiyo, fedha hazijapotea, ila tutakapoikamilisha hii kazi, majengo hayo na mengine ambayo yataongezeka, badala ya kuwa na gati peke yake tutakuwa sasa na bandari. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba hizo fedha hazijapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kama ambavyo ilielezwa katika bajeti yetu, kama utakumbuka katika kitabu chetu cha bajeti katika ukurasa wa 199 utaona kwamba Serikali imetenga shilingi bilioni 24.05 kupitia *TPA* kwa ajili ya ujenzi wa gati, bandari katika Maziwa Makuu.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika fedha hivi ambazo tayari zimetengwa, tutaangalia ni kiasi gani tukipeleke pale ambapo kilishapangwa toka mwanzo ili kuweka mazingira ya haraka ili wale wananchi waanze kupatumia pale mahali wakati wakisubiri ujenzi wa bandari ambayo ndiyo mambo makubwa na mazuri zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 mpaka 2020/2021 na katika mpango huo upo pia mpango wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo; na kwa kuwa katika ujenzi huo uliwekwa jiwe la msingi na kwa kuwa katika Mji wa Bagamoyo limetengwa eneo la viwanda ambapo kunahitaji uwepo wa bandari:-

Je, mpaka sasa Serikali imefikia hatua gani ya kuanza ujenzi huo ukuzingatia unategemea utaratibu wa *Public Private Partnership?* Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tulieleza kwa kirefu dhamira na mpango ambao tayari Serikali imeshauweka wa kujenga Bandari ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie kwamba mpango huo tunautekeleza kwa kupitia *PPP.* Kama ambavyo tulieleza katika bajeti, ni nchi tatu zinashirikiana katika hili kwa mpango wa *PPP.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyosema, kikao cha karibuni kitakachofuata cha kufanya maamuzi ya kuingia katika hatua ya pili, kwa sababu kwa sasa kuna *Joint Technical Committee* imeundwa na inafanya kazi kila wakati kujaribu kupangilia, hatimaye utaratibu wa ujenzi wa hiyo bandari utakuwaje na hizo kazi zinapelekwa kwa hizi nchi tatu ambazo wanashiriki katika *PPP* hiyo; namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa itakapofika mwezi wa Kumi tutakuwa na jibu la uhakika la nini kitaanza na kitaanzia wapi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Moshi Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Serikali ilitumia fedha nyingi sana kujenga gati la Karema, fedha hizo ambazo zilipotea na kilichojengwa pale ni nyumba moja ambayo haijakamilika na kuna choo ndicho ambacho kilikamilka; lakini fedha zilizotolewa na Serikali ni nyingi sana:-

Je, wale walioisababishia Serikali hasara kubwa sana ya fedha nyingi, mmewachukulia hatua gani ambazo ni za kisheria? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Mheshimiwa Moshi Kakoso, naomba tuijadili kwa undani kama ambavyo tulianza na tuwashirikishe watu wengi zaidi ili hatimaye kama kweli kuna tatizo hili linaloongelewa tuanze kuwashughulikia wahusika kwa kutimia vyombo vyetu vya dola kuanza kufanya uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa ninachomwomba Mheshimiwa Mbunge, tupate taarifa kamili. Tunavyofahamu, bajeti ilitumika kama ilivyopangwa na kazi ilifanyika kama ilivyopangwa. Sasa kwa taarifa ya Mheshimiwa Moshi Kakoso, naye akiwa ni mmoja kati ya watu ambao tumedhamiria kwa pamoja kuwajengea miundombinu Watanzania, nina uhakika ana taarifa za ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuzipate hizo taarifa za ziada ili hatimaye tuzipeleke kwenye vyombo vya dola wazifanyie kazi na baadaye tuchukuwe maamuzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza naishukuru Serikali kwamba tukiwauliza maswali hapa kuwaomba waende kwenye maeneo, maeneo mengine wameshafika. Namshukuru sana Mheshimiwa Jafo kwani ametembelea barabara nilizokuwa nimeziomba za kule Msingi na Kinyangiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ikungi ni moja kati ya Wilaya kubwa sana ambayo haina mtandao wa barabara na wananchi wamekuwa wakipata shida sana kufika kwenye Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hususan Jimbo la Ikungi Magharibi ambao wamemwamini sana Mheshimiwa Magufuli na kumpa kura nyingi sana; ni lini sasa Serikali itaenda kule ikaangalie mzunguko wa barabara zile Puma, Ihanja, Iseke pamoja na Mwintiri hadi Igilasoni? Ahsante sana.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Martha Mlata kwamba, changamoto tunazozipata katika Wilaya ya Ikungi, nina uhakika baada ya wewe sasa kuwa Mwenyekiti wa Mkoa wa CCM utatusaidia ili tuweze kuzitatua moja kwa moja ili wale wananchi wanapoambiwa nia ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kufanya maendeleo wasirudishwe nyuma kwa kukataa kushiriki katika masuala ya maendeleo kutokana na changamoto ambazo tunazo katika hiyo Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi watu wa miundombinu tutashirikiana naye kuhakikisha kwamba eneo hilo, changamoto zote za miundombinu tunazitatua ili Wilaya ya Ikungi iwe na hadhi kama Wilaya nyingine za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo sasa aulize swali lake.

Na. 460

## Ujenzi kwa Kiwango cha Lami wa Barabara Kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Kalambo Yaliyopo Matai Kwenda Kasesya

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Kalambo yaliyopo Matai kwenda Kasesya ni ahadi ya muda mrefu ya Serikali na Ilani ya CCM tangu mwaka 2010:-

(a) Je, Serikali itaanza lini kukamilisha ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami?

(b) Je, ni lini ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Sumbawanga hadi Kasanga *Port* utakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshmiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Matai hadi Kasesya yenye urefu wa Kilometa 50 ni sehemu ya Barabara Kuu inayounganisha nchi za Tanzania na Zambia katika mpaka wa Kasesya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Serikali ya Tanzania imekwishaanza kutekeleza mpango wa kuijenga kwa lami. Kazi ya usanifu wa kina na maandalizi ya zabuni ilianza mwezi Julai, 2014 na kukamilika Januari, 2015. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga shilingi bilioni 11.614 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Sumbawanga – Matai hadi Kasanga *Port* yenye urefu wa Kilometa 112 imekamilika kwa takriban asilimia 53 ambapo kilometa 56 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga shilingi bilioni 32.01 ili kukamilisha ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai hadi Kasanga *Port* ambapo ujenzi unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2017.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza naomba

nishukuru majibu ambayo yametolewa na Naibu Waziri na naipongeza Serikali kwa utendaji mahiri wa kazi ambazo zinakuwa zinaletwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba, kwa kuwa, umuhimu wa barabara kwa suala zima la kiuchumi halina mbadala; na kwa kuwa, Mkoa wa Rukwa ni miongoni mwa mikoa ambayo ilikuwa imeachwa nyuma kwa maana ya ukosefu wa barabara kwa kiwango cha lami, na kwa kuwa, umuhimu wa barabara kwa *junction* ya kuanzia Kangesa, kwenda Liapona, Kazila, unapita Mwaze pale anapotoka Muadhama Polycarp Pengo, hadi kwenda kufika Kijiji cha Mozi ambapo ndiyo *customs,* ni ya muhimu sana na iko chini ya *TANROADS.* Je, Serikali iko tayari kuiingiza katika mpango wa kuanza kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa katika bajeti ya 2016/2017 barabara hii haijaingizwa kwa ujenzi wa kiwango cha lami: Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari nimkabidhi barua ya maombi maalum ili iingizwe katika mpango wa kuanza usanifu kwa 2017/2018? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kandege Serikali yake ya Awamu ya Tano ina Ilani ya uchaguzi na ahadi ambazo zimetolewa na viongozi wa Kitaifa. Naomba atupe fursa kwanza tuanze kukamilisha zile barabara ambazo tumeanza kuzifanyia kazi ikiwa ni pamoja na hii barabara ambayo niliielezea kwa kirefu ambayo ipo katika Jimbo lake. Naomba sana hii sasa tuangalie huko mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la pili, niko tayari, naomba niletewe hiyo barua maalum ili tukaijadili Wizarani na baadaye tuangalie kama tunaweza tukaiingiza katika miaka inayokaribia karibu tunaingia kipindi kingine, kama tunaweza kuikamilisha kufanya *feasibility study* na *detailed design* ili kuiandaa sasa ije ijengwe kwa kiwango cha lami katika kipindi hiki cha miaka 10 ya Mheshimiwa Dkt John Pombe Joseph Magufuli.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza!

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami kuweza kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la barabara katika Wilaya ya Kalambo linafanana na tatizo lililopo katika Wilaya ya Wanging'ombe; naomba kujua ni lini Serikali itatengeneza barabara ya kutoka Njombe – Iyai inayopita Makao Makuu ya Igwachanya kutokea Mkoa wa Mbeya kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina uhakika Mheshimiwa Mgaya anakumbuka, wakati mnaipitisha bajeti yetu; na kwa kweli tunashukuru sana mlipoipitisha; katika maeneo ambayo tumeyatengea fedha na tutahakikisha tunayasimamia katika mwaka huu wa fedha, ni pamoja na barabara hii ya Njombe – Iyai na kuendelea. Kuna kiwango cha fedha kimetengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mgaya, nafahamu kwamba unanikumbusha, pamoja na kwamba tuliahidi wakati wa bajeti lakini unaendelea tena kutukumbusha kila wakati ili kwa kutumia njia hiyo ya kurudia kutukumbusha kwamba tutatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mgaya kwamba, sisi tuliopo Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasilaino tukiongozwa na Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, tukiahidi mara moja tunafuatilia utekelezaji. Nami namhakikishia kwamba ataona mwenyewe mwaka huu wa fedha utakapokwisha, ahadi hiyo ambayo ilishatolewa wakati wa kipindi cha bajeti itakuwa imetekelezwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Fred Atupele Mwakibete, swali la nyongeza!

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja. Kwa kuwa tatizo la Barabara ya Kalambo linakwenda sambamba na tatizo la barabara iliyopo Jimbo la Busokelo Wilayani Rungwe inayotoka pale Tukuyu Mjini kuanzia Katumba – Suma – Mpombo – Isange – Ruangwa – Mbwambo hadi Tukuyu Mjini; na barabara hii imekuwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi zaidi ya miaka 10: Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Kilometa 73 zilizobaki?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka tulikaa pamoja kati yako wewe, Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waziri wangu kuhusu barabara hii. Nilikiri wakati ule na ninarudia kukiri hapa kwamba hatujaitendea haki, kwamba ni ahadi ya muda mrefu sana, lakini tumepanga kujenga Kilometa moja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuahidi na Mheshimiwa Mwakibete nilimwahidi kwamba mwaka ujao wa fedha mazingira hayo hayatajirudia. Naomba nirudie ahadi hii sasa hapa, maana yake pale hatukuwa hadharani, leo tuko hadharani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nami naweka kwenye *diary,* hilo swali halitaulizwa tena likisubiri ahadi yako ya mwakani. Mheshimiwa Hussein Bashe, swali la nyongeza! *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza naishukuru Serikali kwa niaba ya wananchi wa Nzega, Mheshimiwa Profesa Muhongo na Mheshimiwa Kalemani wametekeleza ahadi ya kuturudishia machimbo ya Na. 7 na wiki hii wachimbaji wadogo watakabidhiwa maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza swali moja tu. Mwaka 2005 Rais wa Awamu ya Nne aliwaahidi wananchi wa Wilaya ya Nzega, hasa wa Jimbo la Bukene ujenzi wa kilometa 146 wa Barabara ya kutoka Tabora, kupita Mambali, kuja Bukene, kwenda Itobo, kwenda Kahama na Kilometa 11 kutoka Nzega Mjini kuunganisha mpaka Itobo kuweza kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti ya mwaka 2014/2015 Serikali ilitenga fedha za upembuzi yakinifu na tenda ikatangazwa, Wakandarasi wote walioomba wakawa wame-*bid* zaidi. Je, Serikali iko tayari sasa kuongeza fedha ili barabara ile upembuzi yakinifu ukamilike na ujenzi uweze kuanza? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Bashe kwa kunipa elimu ya kina utofauti kati ya hii barabara anayoongelea ya kutoka Tabora kupitia Mambali – Bukene hadi Kahama na ile ya kutoka Tabora kupitia Nzega Mjini hadi Kahama; ni barabara mbili tofauti na zote zina umuhimu mkubwa kiuchumi katika maendeleo ya eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi za viongozi wa Kitaifa tumekabidhiwa tuliopo Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhakikisha kwamba tunazitekeleza. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano, barabara hii kama ilivyoahidiwa, pamoja na hii nyingine ya kutoka Nzega hadi Itobo tunazishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kwa suala lile la kukamilisha *feasibility study* na *detailed design* nimhakikishie Mheshimiwa Bashe kwamba tutawataka *TANROADS* waliangalie upya ili fedha ziongezwe na kazi ile ifanyike, kwa sababu lengo ni kukamilisha kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadri tunavyoendelea kuahirisha upatikanaji wa Mkandarasi kwa sababu ya bajeti kuwekwa kiwango cha chini, tutakuwa hatuwatendei haki wananchi wale wanaohitaji huduma ya ile barabara. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Tutaendelea na ratiba iliyopo mbele. Kwanza tunaanza na matangazo ya wageni.

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ambao ni Viongozi wa Ushirika *TANECU Limited* kutoka Newala, Mkoa wa Mtwara, wakiongozwa na Ndugu Hassan Nakuya ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa *TANECU.* Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ambao ni wanafunzi wa mwaka wa tatu wa Shahada ya Sheria na Rasilimali Watu kutoka Chuo cha Mipango kilichopo Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Ester Michael Mmasi ambaye ni Ndugu Lusekelo Asheli kutoka Mbeya Mjini ambaye ni Mwenyekiti wa Asasi ya Kiraia ya Vijana *(Tanzania Ambassadors of Youth Voices)*. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni tisa wa Mheshimiwa Rita Kabati ambao ni wananchi wake kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya kujifunza nao ni wanafunzi nane kutoka Chuo cha Bandari kilichopo Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo mengine; kuna tangazo la kikao kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Hawa wanatakiwa kukutana leo saa 7.00 mchana mara baada ya kuahirisha Bunge, Ukumbi wa Msekwa 'D.' Mwenyekiti wenu ameleta hili tangazo anaomba wote mfike bila kukosa.

Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC),* Mheshimiwa Khalfan Hilali Aeshi, ameleta tangazo hapa kwamba anataka kuonana na Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati hii, leo saa 7.00 mchana mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge katika Ukumbi Na. 229, Jengo la Utawala. Anaomba mfike bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Joseph Selasini ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moore hapa Bungeni. Anasema leo siku ya Jumatano, tarehe 29 Juni, kutakuwa na Ibada ya Misa kwa Wakristo wa Madhehebu ya Kikatoliki mara baada ya kuahirishwa Bunge saa 7.00 mchana.

Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao siyo Wakatoliki wanaopenda kushiriki ibada hiyo, pia wanakaribishwa.

Waheshmiwa Wabunge, tangazo la mwisho. Tangazo hili limeletwa na Naibu Katibu wa Bunge (Shughuli za Bunge), Ndugu John Joel, na anawatangazia Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Shirika la Reli Tanzania *(TRL)* limetoa usafiri wa treni ya *Deluxe* kutoka Dodoma kuelekea Dar es Salaam, siku ya Ijumaa tarehe 01, Julai 2016, saa za asubuhi.

Lengo ni kuwawezesha Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kuweza kuona eneo korofi la Gulwe na Kilosa ambapo reli huchukuliwa na maji mara kwa mara.

Hii itawawezesha Waheshimiwa Wabunge kuweza kusihauri Serikali ipasavyo. Tafadhali orodhesha jina lako kwa Makatibu wa Kamati ya Miundombinu, yaani Ndugu Hosiana John na Ndugu Richard Masuke ambao watakuwa eneo la mapokezi Ukumbi wa Msekwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, katika moja ya majukumu yetu ya kuishauri Serikali, tunaombwa na *TRL* kwamba tutumie reli yao siku ya Ijumaa na tafadhali mkajiorodheshe Ukumbi wa Msekwa tukishaahirisha shughuli za Bunge ili waweze kujua ni Wabunge wangapi watasafiri nao waweze kutayarisha mabehewa mahususi kwa ajili ya kazi hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninao mwongozo mmoja hapa ambao nataka kuuleta kwenu kabla hatujaendelea. Mwongozo huu uliombwa na Mheshimiwa Oscar Mukasa kuhusu kutojibiwa kwa ufasaha swali la nyongeza aliloliuliza kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Waheshimiwa Wabunge, katika kikao cha Hamsini na Moja cha Mkutano wa Tatu wa Bunge kilichofanyika tarehe 27, Juni 2016, Mheshimiwa Oscar Mukasa aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kutokana na majibu ya swali la msingi namba 437 lililoulizwa na Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma.

Mheshimiwa Mukasa aliuliza kuwa ipo ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati akiomba kura kwa wananchi wa Biharamulo ya kujenga barabara kilometa nne mpaka tano kwa kiwango cha lami kwenye Mji wa Biharamulo, hivyo anaomba kufahamu kutoka Serikalini kwamba utekelezaji wa ahadi hiyo umefikia wapi?

Swali hilo lilijibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kama ifuatavyo, nanukuu:-

"Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi anayoongelea ni kweli ilitolewa na Mheshimiwa Rais na kwa kweli ahadi hiyo ilianza kutoka Serikali ya Awamu ya Nne na ni kwa ajili ya eneo hilo, lakini vilevile eneo jirani ambalo Mheshimiwa Dkt. Kalemani anatoka. Hayo yote, ahadi hizo zote tutazitekeleza. Lini? Itategemea na upatikanaji wa fedha kwa sababu utekelezaji wa ahadi hizo unahitaji rasilimali fedha.

Kwa hiyo, mimi naomba nikuahidi ahadi hizo tutazitekeleza na nikuahidi miaka mitano hii ambayo ndiyo tumepewa hii dhamana ya kuwajengea Watanzania miundombinu na kutekeleza ahadi zote ambazo viongozi wetu walizitoa, nikuhakikishie tutazitekeleza."

Mheshimiwa Oscar Mukasa hakuridhika na majibu hayo na ndiyo sababu ya kuomba Mwongozo wa Spika. Mheshimiwa Oscar Mukasa aliomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7), sambamba na Kanuni ya 46 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika mwongozo wake alisema, nanukuu:-

"Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la nyongeza kufuatia swali la msingi namba 437 lilikuwa linauliza juu ya ahadi ya Mheshimiwa Rais kuhusu Kilometa nne mpaka tano za lami Biharamulo Mjini, lakini kwenye majibu yake amezungumzia ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne ambayo imeshakamilika, imetimizwa na akazungumzia habari ya Chato kwa Mheshimiwa Kalemani ambavyo vyote viwili sikuona mahusiano na ahadi ya Rais wa sasa wa Awamu ya Tano ya ujenzi wa barabara nne mpaka tano kwa kiwango cha lami Biharamulo. Naomba mwongozo wako kwa sababu sijaridhika Mheshimiwa Naibu Spika."

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuomba muongozo huo nilijibu kuwa nitafuatilia kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge ili niweze kuona swali liliulizwaje na namna gani majibu yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri ili niweze kutoa Muongozo.

Baada ya kuzipitia Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge nimeridhika kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano alijibu swali hilo kwa ufasaha. Katika majibu ya swali hilo la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kuwa utekelezaji wa ahadi hizo itategemea upatikanaji wa

rasilimali fedha. Alieleza zaidi kuwa ahadi hizo Serikali itazitekeleza ndani ya miaka mitano ambayo amepewa dhamana ya kuwajengea Watanzania miundombinu na hivyo atatekeleza ahadi zote ambazo viongozi walizitoa. *(Makofi)*

Hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 45(3) na Kanuni ya 46(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge nimeridhika kuwa swali hilo la nyongeza la Mheshimiwa Oscar Mukasa lilijibiwa kikamilifu na huo ndio Muongozo wa Spika.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo tunaendelea na ratiba.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mwongozo wa Spika.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Amina Mollel.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa Mwongozo wangu na kwanza kabisa nasimama kwa kanuni ya 68(7) lakini pia kwa sababu jambo hili halijatokea hapa Bungeni na kwa kuwa linatugusa Waheshimiwa Wabunge pamoja na jamii yote kwa ujumla naomba kusimama kwa Kanuni ya 47(2) lakini 48(2)(a) pamoja na ya (3).

Mheshimiwa Naibu Spika, jana katika kituo cha *Clouds TV* kilikiuka maadili na taaluma hii ya habari kwa kurusha kipindi ambacho maudhui yake yalikuwa yaki-*promote* ushoga. Kwanza naomba ni-*declare interest* kwamba mimi mwenyewe ni mwanahabari na maadili ya taaluma hii nayafahamu na ndiyo maana nikaona ni vyema nisimame ili kuweza angalau kupata mwongozo wako lakini pia kwa kanuni niliyoitaja ya 47 na 48.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taaluma ya habari ni vyema kama mwanahabari anataka kuelimisha jamii na hasa katika mambo ambayo kwanza kabisa katika nchi hii sheria za nchi haziruhusu ushoga. Kwa maana hiyo kama alikuwa anataka kuzungumzia ushoga basi ni afadhali angezungumzia kwa watu ambao wamekwishafanya matukio hayo lakini nafsi yao wana-*regret* kwa kile walichofanya ili kutoa taarifa kwa wengine kwamba tukio hilo siyo zuri kwa jamii. Lakini kwa jinsi ambavyo lilivyotumika kwa kituo hiki yule alikuwa aki-

*promote* lile tukio na alionyesha kwamba ni mtu anayefurahia kitendo kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha asubuhi hii muendeshaji wa kipindi kile alialikwa katika kipindi cha asubuhi lakini badala ya kuonyesha ni kwamba ni kwa jinsi gani kwa namna moja au nyingine kwa kuomba radhi kwa kuwakwaza watazamaji, lakini yeye alijitetea. Kwa mwongozo wako na kwa kanuni hizo nilizo tumia naomba mwongozo wako na kwa kuwa Serikali ipo hapa je, tuna-*promote* ushoga hapa nchini au ni hatua gani ambazo vituo vingine visije vikafanya ambazo kituo hiki kinapaswa kuchukuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE.KANGI A. LUGOLA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

**MHE.KANGI A. LUGOLA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE.KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, nimesimama hapa na mimi chini ya Kanuni ya 68(7) niombe Mwongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na muendelezo humu Bungeni wa baadhi ya Naibu Mawaziri kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge mara nyingi kwa kubahatisha au kukubaisha au kulipua na hivyo kutufanya Waheshimiwa Wabunge kuona kutokuwepo umuhimu wa sisi kuuliza maswali hasa ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi anajibu swali langu la nyongeza nililoliuliza kwenye swali la msingi namba 452, Mheshimiwa Naibu Waziri nilimuuliza juu ya changamoto za usalama ambazo ziko kwenye Jimbo langu la Mwibara na hasa kijiografia ambapo kuna visiwa vingi na mara nyingi kunatokea uhalifu. Ni lini Serikali itaweza kuipa hadhi jimbo la Mwibara kuwa Wilaya ya Kipolisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yeye alijibu kwamba Serikali ina mpango wa kujenga vituo vya polisi hapa nchini.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu swali langu kwa kulipua kwa sababu mimi sikuuliza Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo vya polisi ila niliuliza ni lini jimbo la Mwibara litapewa hadhi ya Wilaya ya Kipolisi. Kwa hiyo ninaomba

mwongozo wako kama ni sahihi Mheshimiwa Naibu Waziri kunipa majibu ya swali ambalo mimi sikumuuliza, ahsante sana.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

**MBUNGE FULANI:** Muongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, Mwongozo.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara alipokuwa akijibu swali namba 454 la Mheshimiwa Magdalena Sakaya na swali la nyongeza likawa limeulizwa na Mheshimiwa Kadutu kuhusu suala la lumbesa. Mheshimiwa Waziri ameelekeza kwamba lumbesa ni kilo 100 kwa gunia lakini Halmashauri yangu ya Nyang'hwale Wakala wa Vipimo wanawalazimisha wasafirishaji wa mpunga na mahindi kwamba gunia liwe na kilo 75 tu.

Kwa hiyo, panakuwa na usumbufu kwa wafanya biashara wetu wa Nyang'hwale, ninaomba muongozo wako Serikali na Halmashauri tuchukue kauli ipi kilo 75 za Halmashauri ama kilo 100 ambazo amezitamka Mheshimiwa Waziri wa Viwanda?

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mwongozo wa Spika Mheshimiwa, Mchengerwa hapa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa …

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Agness.

**NAIBU SPIKA:** Leo miongozo ni mingi sana yaani kipindi chote cha maswali na majibu kimeenda kinyume na Kanuni, Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupitia Kanuni hiyo ya 68(7) ambayo binafsi ninaona ina mapungufu makubwa kwa kuwa Kanuni hii haitoi mamlaka kwa hoja ambazo zimeibuka nje ya Bunge kuweza kujadiliwa ndani ya Bunge hili. Lakini pia kwa ridhaa yako Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri yetu ya Muungano ambayo inatoa mamlaka ya kusimamamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa kutumia Kanuni ya 50 ya Kanuni zetu za Bunge kama zilivyorekebishwa mwezi Januari 2016, Kanuni ya 28 ambayo pia ina mapungufu kwa muda wa masaa ambayo yametolewa kwa

Mbunge kuweza kuwasilisha Mwongozo. Lakini Kanuni ya 48(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambayo inazungumzia jambo la muhimu lililotokea lenye maslahi kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba *discretion* yako kwa mujibu wa kanuni ya 5 ya kanuni zakudumu za Bunge ili uruhusu sasa niweze kuomba muongozo huu na hii inatokana na tukio lililotokea jana katika Jimbo la Rufiji ambapo watu wenye silaha waliwashambulia wananchi wangu wa Jimbo la Rufiji, ambapo wananchi kadhaa walipigwa mapanga na kuuwawa na pia ilipelekea mwananchi mmoja kupigwa risasi, na risasi kazaa zilipigwa na wananchi wengine walijeruhiwa maeneo mbalimbali ya mwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio haya ya uhalifu yametokea jana katika Jimbo langu la Rufiji katika Tarafa ya Muholo, katika Kata ya Mbwara na katika kijiji cha Nyamwage. Matukio haya ya uhalifu yameendelea kutokea pia katika nchi yetu hii ya Tanzania na matukio haya yameripotiwa maeneo ya Mwanza, Tanga na maeneo mengine ya nchi. Lakini matukio haya yanasababishwa na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa, Kanuni unayoitumia ukishasema maneno machache kuhusu hoja unayotaka kutoa unatakiwa unipe mimi nafasi ya kujibu kama uendelee au hapana.

Kwa hiyo, nadhani kimsingi maneno yako machache unayotaka kuyatolea hoja umeshayasema kwa hiyo nimeyaelewa. Nilisikia mtu mwingine ametoa mwongozo.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Agness, Mwongozo wa Spika

**NAIBU SPIKA:** Yuko wapi Mheshimiwa nayeomba muongozo simuoni

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Sehemu gani?

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Agness.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agness Marwa.

**MHE. AGNESS M. MARWA:**Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana mimi pia nilikuwa nataka kuiongelea suala la huyo kijana shoga na nimeliongelea kwa sababu ametokea mkoani kwangu Mara tena ni jirani yangu Musoma Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kushangaza huyo kijana alituma *message* kabla akiwa anasema anataka kwenda kuelimisha jamii na yeye amechoka na shughuli hizo na ushahidi upo kuna ndugu yake ambaye yuko nyumbani kwangu hadi sasa hivi alikuwa ametuma *message* kwamba anataka kwenda kuelimisha jamii.

Mheshimiwa naibu Spika, yeye baada ya kufika pale kaenda kuongea mambo mengine ametuaibisha sana Musoma, lakini pia ni kijana ambaye amefanya tabia mbaya sana kiasi kwamba watafikiria kwamba labda mwenye redio ndiyo kamtuma, yawezekana ni tabia zake. Kwa kweli Serikali imchukulie hatua huyo kijana kwa sababu anawafundisha ndugu zetu tabia mbaya, lakini pia anataka kuwachonganisha Serikali na baadhi ya vyombo vya habari ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Waheshimiwa Wabunge watano hivi.

Nianze na mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Amina Mollel ambaye alianzakwa kutaja kanuni ya 68(7) akataja kanuni ya 47(2) pia akataja kanuni ya 48(2)(a).

Waheshimiwa Wabunge, kwanza nianze kwa kukumbusha tena kuhusu mwongozo unaombwa katika mazingira gani? Mazingira aliyoeleza Mheshimiwa Mollel nadhani wote tulikuwepo hapa ndani ameeleza kuhusu kipindi cha kituo kimoja cha *television* ambacho kilionyesha mambo ambayo kwa mujibu wa Mheshimiwa Amina Mollel yalikuwa yanaenda kinyume na maadili ya wananchi lakini pia maadili ya utangazaji.

Waheshimiwa Wabunge, nitaeleza kwa msingi kwamba jambo hilo halikupaswa kuombewa mwongozo, lakini kwa sababu ni jambo ambalo limeelezwa kwa namna ambayo Mheshimiwa Mollel ametaja na Kanuni zingine ambazo zinaweza zikatumika katika mazingira aliyoyaeleza yeye na jambo hili kutokea. Waheshimiwa Wabunge Kanuni ya 47 Mbunge anaweza kusimama kwa kutumia Kanuni hiyo bila kuomba mwongozo wa Spika.

Kanuni ya 47 inamtaka Mbunge atoe hoja kwamba shughuli za Bunge zisitishwe ili jambo hilo analolitoa yeye ambalo anaona ni la dharura liweze kujadiliwa.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge unapotaka kusimama kuhusu jambo la dharura ili shuguli za Bunge zisimame unatoa hoja yako kwa mujibu wa Kanuni ya 47 na hauombi Mwongozo. Lakini hata hivyo kwa sababu kwa namna hoja ya Mheshimiwa Amina Mollel ilivyotolewa inavyoonekana hili jambo ni zito. Mimi binafsi Waheshimiwa Wabunge sikuliona lakini hiyo haimaanishi kwamba

haliwezi kutolewa maelezo kwa mujibu aliotoa Mheshimiwa Amina Mollel. *(Makofi)*

Lakini Waheshimiwa Wabunge Kanuni hiyo hiyo ya 47 ukiisoma na Kanuni ya 48 hili ni jambo ambalo linapaswa kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria tulizonazo. Kwa hiyo, ni jambo ambalo linawezekana kabisa kushughulikiwa kwa utaratibu ambao upo na kwa sababu Mheshimiwa Amina Mollel ametusaidia kwamba katika taaluma ama tasnia ya uandishi wa habari chombo hicho kwa yeye alivyoona kimekiuka maadili ya utangazaji. Mimi naamini hata hapa tunapoongea vyombo vilivyo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano vimeshaanza kufanyia kazi suala hilo, kwa hiyo hatuna haja ya kulijadili kama jambo la dharura kwa sababu linayo namna kisheria ya kushughulikiwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hiyo hatutalijadili jambo hilo kwa mujibu wamasharti ya Kanuni ya 47 na 48 sasa pamoja na kwamba niliombwa muongozo lakini maelezo ni hayo Waheshimiwa Wabunge. Wakati mwingine Mbunge akiwa na jambo analotaka lijadiliwe atoe hoja kwa mujibu wa Kanuni hiyo niliyoitaja.

Nimeombwa pia muongozo na Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola kuhusu swali lake la nyongeza alilouliza kwamba ni lini Jimbo la Mwibara litabadilishwa hadhi kwa maana ya kipolisi na kuwa Wilaya ya Kipolisi. Kwa maelezo ya Mheshimiwa Kangi Lugola wakati akitoa hoja yake anasema, majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi yanasema kwamba Serikali ina mpango wa kujenga vituo vya polisi maeneo mbalimbali nchi nzima na kwamba Jimbo la Mwibara ni eneo mojawapo. Kwa mujibu wa Mheshimiwa Kangi Lugola hilo halikuwa jibu la swali aliloliuliza.

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wa Mheshimiwa Kangi Lugola utanitaka nikaapitie Kumbukumbu Rasmi za Bunge ili niwe na uhakika na kile alichokuwa ameuliza Mheshimiwa Kangi Lugola na kile ambacho amejibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi halafu nitatoa Mwongozo hapo baadaye kama Kanuni ya 68(7) inavyosema.

Lakini pia nimeombwa muongozo na Mheshimiwa Hussein Amar kuhusu majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji juu ya swali alilouliza Mheshimiwa John Kadutu la lumbesa na kwamba majibu yalitoka kwamba ni kilo 100.

Lakini Mheshimiwa Hussein Amar anasema katika Jimbo lake la Nyang'hwale Wakala wa Vipimo anaonyesha kwamba kipimo hicho hicho alichokisemea Mheshimiwa Waziri kwamba ni kilo 100 huko Nyang'hwale wanasema kilo 75. Sasa pamoja na kwamba nimeisikia hoja ya Mheshimiwa

Hussein Amar kuhusu Waziri kusema kilo 100 na yeye katika Jimbo lake kuambiwa kilo 75 nitahitaji muda ili nifuatilie jambo hili halafu niweze kulitolea mwongozo. Lakini pia nitamtaka Waziri aniletee hizo taarifa ili muongozo wangu niutoe vizuri, kwa hiyo ili wananchi wote nchi hii wajue hiyo lumbesa ni kilo 100 ama 75.

Mwongozo mwingine uliombwa na Mheshimiwa Mchengerwa lakini wacha niufanye mwongozo wa Mheshimiwa Mchengerwa wa mwisho, nimeombwa pia mwongozo na Mheshimiwa Agness Marwa ambae jambo lake lilikuwa linashahabiana na jambo alilokuwa ameliombea Mheshimiwa Amina Mollel nakutaka kwamba hoja hiyo ijadiliwe.

Mheshimiwa Agness Marwa, kimsingi hakuwa ameomba mwongozo yeye alikuwa anatoa ushauri wa mambo ambayo huyo anayehusika na kituo kinachohusika cha *television* wanaweza kufanyiwa.

Lakini Waheshimiwa Wabunge kwa sababu mambo haya yako kisheria na sheria zimeweka wazi nini cha kufanya katika mazingira hayo, mimi naamini kwamba vyombo vinavyohusika vitachukua hatua hizo kwa mujibu wa sheria kwa hiyo haitajalisha sisi tutalijadili kwa kiasi gani, lakini lazima sheria tulizotunga wenyewe ziweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mchengerwa ametoa maelezo kwa mujibu, na yeye ameanza kwa kuomba Mwongozo wa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7); Waheshimiwa Wabunge nisingependa kurudia maelezo niliyoyatoa na alianza pia kwa kueleza kwamba Kanuni hii haitoi fursa ya mjadala wa mambo yanayotokea nje ya Bunge kwa hivyo ni kama imepungua hivi.

Kimsingi kanuni hizi inawezekana yapo mambo ambayo yamepungua, lakini hili la Mheshimiwa Mchengerwakanuni ziko vizuri tu hautakiwi kupitia kanuni ya 68(7), kama jambo lako lina Kanuni nyingine ambayo inahusika. Unatumia Kanuni ya 68(7) pale tu unapotaka kuuliza jambo lililotokea wakati huo humu ndani. Kama unataka kuzungumza kuhusu jambo la dharura unaenda moja kwa moja kwenye Kanuni ya 47; huna haja ya kupitia Kanuni ya 68(7) inayohusu mwongozo.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 47(4) ina sema hivi; iwapo Spika ataridhika kwamba jambo hilo ni la dharura halisi na lina maslahi kwa umma basi ataruhusu hoja hiyo itolewe kwa muda usiozidi dakika tano. Kwa hiyo kimsingi Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ameshatoa hoja yake, kwa hiyo mimi natakiwa kuitolea maamuzi kama atoe sasa hoja hiyo au hapana.

Waheshimiwa Wabunge, suala la mauaji nilishawahi kusema hapo nyuma ni suala linalotisha sana lakini mtakumbuka nilitoa maelezo ama maelekezo kwa Serikali, kwamba ituletee taarifa itakapomaliza uchunguzi wake juu ya mambo hayo ili sisi tuweze kutoa taarifa kwa wananchi wetu kwa sababu sisi ni wawakilishi wao, lakini pia kama Bunge kwa sababu ndio tunaoletewa hayo matatizo tujiridhishe na sisi juu ya kile wananchofanya. Lakini nilitoa pia wakati huo kwamba hatuwezi kutoa muda kwamba lini wafanye hivyo kwa sababu hili ni jambo zito na linahitaji uchunguzi wa vyombo vingi. Kwa hiyo, na Serikali isingeweza kuleta taarifa kama halijakamilika.

Sasa jambo alilolielezea Mheshimiwa Mchengerwa wote Waheshimiwa Wabunge mmelisikia, amelieleza ni jambo la kutisha kwamba watu wengine wamepigwa mapanga na risasi zimesikika kwa hiyo watu wa Jimbo lake wametishwa. Nikubaliane naye kwamba hili jambo linatisha sana. Lakini kwa mujibu wayale tuliyonayo Waheshimiwa Wabunge ukiisoma hii Kanuni ya 48 inatutaka hata sisi hata ili tuweze kujadili ni lazima tuwe na hizo taarifa.

Jambo kama anavyosema limetokea jana usiku maana yake taarifa hizi pengine yeye anazo kwa sababu ni Mbunge wa huko, ningeweza kuiambia Serikali ieleze sasa hivi; lakini pengine haina hata hizo taarifa kwa muda huu. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mchengerwa kwamba mimi nitaitaka Serikali ifuatilie jambo hili leo, itueleze kesho kwamba ni nini kimetokea. Si kwa taarifa za kiuchunguzi lakini kutueleza Wabunge, kwa sababu tumeelezwa hapa na Mheshimiwa Mchengerwa kwamba ni nini kilichotokea huku Rufiji.

Mheshimiwa Mchengerwa alienda kwenye Kanuni nyingine kadhaa na baada ya mimi kutoa maelezo hayo si dhani kama kuna haja ya kwenda kwenye hizo Kanuni, isipokuwa nitoe tu maelezo kidogo Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya uelewa.

Kanuni ya 28 aliyoitaja Mheshimiwa Mchengerwa, ukisoma fasili ya (8) inataka Mbunge anayetaka kutoa Maelezo Binafsi awe ameleta taarifa kwa Spika angalau siku moja kabla, na hiyo taarifa atakayokuwa ameileta kwa Spika ndiyo atakayoisoma hapa ndani. Kwa sababu Kanuni hizi tumejiwekea wenyewe kwa hiyo niseme tu jambo la Mheshimiwa Mchengerwa limepokewa kwa uzito, kwa namna yeye alivyolipokea kutoka huko Jimboni. Lakini kwa kuwa wengi wetu hatuna taarifa ikiwa ni pamoja hata na mimi nimeisikia kutoka kwa Mheshimiwa Mchengerwa, Serikali siku ya kesho tutakapokutana ituletee hiyo taarifa juu ya hilo lililotokea huko Rufiji.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunaendelea.Katibu.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mwongozo Mheshimiwa Naibu Spika.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Miswada ya Sheria ya Serikali….

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa sasa tunatakiwa kuendelea. Labda kama una..maana umetaja mwongozo maana yake utaje sasa kuna jambo limekosewa humu ndani asubuhi. Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Kanuni ya 68(7) Mheshimiwa mwongozo wako, kwa kuwa nilitumia Kanuni kadhaa na Kanuni hizi, kama nilivyosema kwamba, Kanuni hizi zimekuwa zikikosewa na waandishi, na tunaomba sasa Kamati ya Kanuni ijipange katika kuangalia mambo ya msingi ambayo yanakuwa yanatokea nje ya bunge hili ili yaweze kujadiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitumia pia Ibara ya 63 na Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inaitaka Bunge hili kuisimamia Serikali na kwa kuwa hoja hii binafsi kama nilivyosema kutumia Kanuni ya 48(4) sikuwa na haja ya mjadala, isipokuwa tu ni kutoa taarifa pamoja na kuzungumzia yale yaliyotokea ili Serikali iweze kujipanga. Kwa hiyo nina mambo mawili tu, ukiniruhusu niweze kuyazungumza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimwa Mchengerwa sitaweza kukuruhusu kwa sababu naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mchengerwa kuisimamia Serikali ni lazima wewe mwenyewe kwanza uwe na hizo taarifa mahususi, hatutaweza kuisimamia hapa Serikali kama yenyewe haitaweza kujibu hizo hoja tunazotaka kuzileta mbele yake, na jambo hili Waheshimiwa Wabunge, ni jambo la mauaji kama anavyosema, ni jambo la watu kutumia silaha za moto, tutakapoanza kulijadili humu ndani, tunalijadili kwa kufanya nini? Ndio maana mimi nimesema hivyo ni jambo zito, lakini ukisema kwamba ni jambo la dharura ambalo ni lazima; yeye anasema ametumia Kanuni ya 48 ili aitolee maelezo. Kanuni ya 48 haihusu kutoa maelezo. Waheshimiwa Wabunge, tuelewe tu, inahusu masharti ya jambo la dharura, ambayo maana yake inasomeka pamoja na Kanuni ya 47; ukitaka kutoa maelezo binafsi, ni Kanuni ya 50 na kanuni ya 28(8).

Kwa hiyo, tuelewane tu hivyo Waheshimiwa Wabunge, na jambo hili Mheshimiwa Mchengerwa unasema unataka kulitolea taarifa, mimi kwa kutumia kanuni hizi hizi, sitairuhusu hiyo taarifa kwa sababu nimeshatoa maelezo kwamba Serikali ilete taarifa kesho kuhusu jambo lililotokea Rufiji. Tunaendelea Waheshimiwa. Katibu. *(Makofi)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**MUSWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa mwaka 2016**
***(The Public Procurement Amendment Bill 2016)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano. Wapo Wabunge wachache watakaopata fursa ya kuchangia asubuhi hii kabla sijamwita mwenye hoja kuhitimisha. Tutaanza na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Kasenyeda Sanga.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niwezeze kuchangia muswada ulioko mbele yetu wa kurekebisha Sheria ya Ununuzi wa Umma wa mwaka 2016.

Kwanza kabisa naomba nipongeze Serikali, nimpongeze Waziri na Naibu wake, kwa kutuletea sheria nzuri kabisa ambayo itaweza kutuokolea fedha nyingi. Kwenye bajeti ya mwaka huu tumepitisha asilimia 40 ya fedha zote kwenye shughuli za maendeleo; sasa kama tumepitisha asilimia 40 maana yake ni fedha nyingi. Fedha nyingi hizi, bila kuwa na sheria ya kuzilinda hazitafikia wananchi. Kwa hiyo naomba niipongeze Wizara kwa kweli, na Mheshimiwa Waziri Mpango, kwa kuleta mpango mzuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya muswada huu wa kupunguza gharama na kuleta ufanisi ni jambo jema ambalo wote Wabunge lazima tuliunge mkono ili sheria hii iweze kufanya kazi. Lakini nipongeze kipekee kwa sheria hii kuja kuangalia wazawa, kwamba wale wenye makampuni ya wazawa, *local* waweze kupewa kipaumbele, nalipongeza sana na naipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kujali makundi mbalimbali, kina mama, walemavu, wazee ni jambo jema na Serikali makini lazima iangalie watu wake na makundi yake waweze kushiriki kwenye uchumi huu, kwa hiyo nalo nisuala ambalo nimesimama kuipongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ku-*promote local production* ya bidhaa zetu ni jambo zuri ambalo kwa kweli nahamasisha kwamba Wabunge wengine tuweze kuiunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria imekwenda mbele zaidi kwa kurekebisha ushiriki wa Madiwani kwenye manunuzi. Mimi naishurukuru Serikali kwamba kazi ya Madiwani iwe ni kuisimamia Serikali kwa maamuzi iliyoyafanya, siyo na Madiwani kuwa wanashiriki kwenye *tender* ambacho kinakosesha ile roho yenyewe ya usimamizi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu uko kwenye bei ya soko. Hatuna tafsiri ya bei ya soko na sioni kama kuna mtu yeyote anajua bei ya soko. Bei ya soko inategemeana na bidhaa yenyewe, lakini kwa kuwa ni manunuzi ya Serikali, mimi nilikuwa napenda kwamba Serikali iwapongeze wazabuni na wakandarasi wote, kwa sababu wakandarasi hawa wanaikopesha Serikali, kabla hawajawalipa. Kwa hiyo wana umuhimu mkubwa sana katika Serikali hii, kwamba wanafanya vitu *in advance* kwa kutumia fedha zao, Serikali inakuja kuwalipa baadaye. Kwa hiyo hawa ni wabia muhimu sana; na hasa kwenye *PPP* tunayoisema kila siku, kwa hiyo mimi naona kwamba bei ya soko ili tuweze kuipata Waziri inabidi sasa ujipange, je, unazo fedha za kuwalipa wakandarasi kwa muda ili waweze kukupa bei ya soko?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama unawalipa baada ya mwaka, miezi sita hakuna mfanya biashara yeyote mwenye kampuni ambaye anaweza ku-*predict* bei ya vifaa baada ya mwaka mmoja, kwa hiyo lazima aweke bei ambayo itakuja ku-*compensate loss* yoyote ile atakayo ipata. Lakini ni vizuri ujipange sasa kwa fedha hizi uweze kuwalipa wazabuni, na wenyewe watakupa bei ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipo kipengele cha kujadiliana ni kipengele kizuri, lakini wasiwasi wangu itakuja kuleta migongano ya makampuni kulingana na ulivyofanya majadiliano, kama ulijadili na kampuni moja ambayo unaitaka ipate na ikashusha bei na ukaiacha nyingine, hapa ndio utakuwa ni kwenye mgogoro. Kwa hiyo hiki kipengele ni vizuri tukiangalie kwa makini, tuweze kujua namna ya kuja kutatua migogoro hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali kwenye ujenzi kwa nini isiboreshe vituo vyake vya ujenzi, kwa kununua mitambo, ma-*grader* ili gharama ya kutengeneza barabara iweze kupungua. Kama mnataka gharama zipungue basi ningeshauri kwamba mboreshe kila Wilaya ipelekewe mitambo ya ukandarasi, iwepo kitengo cha ujenzi, na iwe inatengeneza barabara wawe weka mafuta na madereva wanaajiriwa. Hiyo inawezekana, kama mmeamua kwamba tuweze kupunguza gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko *emergency procurement* ambayo kwa kweli naona kwenye muswada huu haijasema vizuri, labda kwenye kanuni za Waziri, Hospitali huwa zinaishiwa *gloves*, zinashindwa kununua kwa sababu mlolongo wa manunuzi umekuwa mrefu. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri ninakuomba

kwenye ununuzi wa ghafla hasa kwenye dawa hospitali, *MSD* ni vitu muhimu lazima uziweke kwenye kanuni, kama hujaweka kwenye kanuni mtu anaweza akafa nashindwa mtu kuchukua hela ofisini au ndani ya kituo kwa sababu milolongo ya manunuzi iko mbali; kwa hiyo kanuni tunaomba uweze kuiweka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sina mengi, ninashukuru na sheria ni nzuri tuipe nguvu tuipe *support*, nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali naye kwa kutuandalia sheria nzuri, na mara nyingi amekuwa akifanya hivyo, naye tunampongeza sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, wapo wachangiaji watatu, kama wataweza kutumia muda pungufu ya dakika kumi nitawashukuru. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba.

**MHE. DEO K. SANGA:**Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naipongeza sana Serikali kwa kuleta muswada huu ambao Wabunge wameelezea kwa muda mrefu sana ili kuleta tija na mabadiliko makubwa ambayo huko nyuma lilikuwa ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kupitia Waziri wa Fedha, Naibu na watendaji wote wa Wizara hii ya Fedha ikiongozwa na Mheshimiwa Mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli lilikuwa tatizo kubwa sana tulifika mahala unakuta bati moja lilikuwa linaweza kununuliwa kwa shilingi 35,000; simenti shilingi 22,000; mimi ninasema hivyo iko haja ya kipindi kilichopita mimi kama Mbunge, Mfuko wa Jimbo tulinunua simenti kwa shilingi 22,000 na bati la geji 28 kwa shilingi 35,000; ukiuliza wanasema Sheria ya Ununuzi. Jamani mbona huko madukani wanauza bei chini? Sheria ya Ununuzi. Kwa hiyo nadhani sasa imeletwa wakati muafaka kabisa kwamba sasa tutaangalia soko linasema nini. Kwa hiyo mimi nadhani tutawatendea haki watanzania walipakodi na kadhalika.

Lakini pamoja na marekebisho hayo, nivizuri marekebisho hayo bado Serikali iendelee kuangalia mapungufu madogo madogo ambayo yataendelea kujitokeza ili waendelee kukaa na kuona namna ambavyo waweze kurekebisha uendelee mpango mzuri zaidi kadri ambavyo itakavyokuwa inakwenda. *(Mkofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu Kamati ya Mipango na Fedha za Halmashauri, mimi nishauri na niombe sana, sijaona kama wameleta

*amendment* hapa; lakini ni vizuri Kamati hizi hasa Kamati ya Mipango na Fedha ya Halmashari iendelee kama ilivyokuwa ni lazima angalu ipitie kwa sababu Kamati hizi zinakaa kila mwezi mara moja ili kuona kwenye Halmashauri yao ni kitu gani ambacho kimejadiliwa kwenye Bodi ya Zabuni. Sasa tukiondoa kabisa Kamati hii ya Mipango na Fedha na wao ndio wenye fedha za Halmashauri na bajeti hii ambayo tumeendelea kuijadili na kuimalizia sasa Serikali imetenga fedha nyingi kwenda huko, haki ya Mungu zitakwenda kuliwa, tutakuwa tulichokifanya hakipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana kwamba waone uwezekano kabisa wa Kamati hii ya Mipango na Fedha kama alivyo Mpango mwenyewe Waziri wetu aone uwezekano wa kwamba Kamati hii ni vizuri ikapitia, itakuwa tumeitendea haki kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiuangalia muswada huu umelenga pia kuwa hudumia walemavu, jamii mbalimbali, akina mama, watoto na kadhalika, tumeutendea haki kabisa muswada huu nadhani umefika mahala pake ambapo sasa maelekeo ni mazuri.

Mimi niombe tu Waziri Mpango tunakuamini sana, Bunge hili linakuamini sana, wewe, Naibu wako pamoja na Wizara nzima, tuombe sana, Kamati ya Mipango na Fedha, niombe sana ishiriki kwenye mambo hayo ambayo wao watakuwa wamepitisha kule hawa wanapitia kuangalia kilichomo kwenye Halmashauri yao tutakuwa tumeitendea haki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo naunga mkono hoja, ahsante sana, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omary Tebwete Mgumba atamalizia Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika hoja iliyo mbele yetu.

La kwanza niipongeze Serikali kupitia Wizara ya Fedha kwa kuleta sheria hii katika Bunge lako, ili tuweze kuifanyia mabadiliko. Sheria hii ni muhimu sana tena imechelewa sana kuleta, kwa sababu ni sheria kandamizi ambayo ilikuwa inasababisha mzigo mkubwa kwa wananchi, Serikali kutumia fedha nyingi kuliko gharama halisi ya bidhaa ambazo zilikuwa zinatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Sheria hii ilikuwa inachelewesha maendeleo, hasa Serikali kuwahudumia wananchi wake kutokana na mchakato mrefu ambao ulikuwa unafanyika kupitia sheria hii; ambao zaidi siku 90 kwa maana ya zaidi ya miezi mitatu, kitu ambacho kilikuwa kina sababisha kuchelewa kupata huduma kwa wananchi wetu.

Baada ya utangulizi huo naomba kushauri vitu vichache kama ulivyosema nitumie muda vizuri kwa sababu muda siyo rafiki; nitaenda kwa haraka haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza kama sheria yenyewe inavyotaka lengo kubwa ni kwenda hasa kuzingatia *value of money*, ni kwa sababu ya kupata thamani halisi ya pesa ambazo zitatumika. Kwamba kama tukanunue bidhaa kutokana na bei ya soko ni kweli kabisa, lakini ni jambo zuri, ningeishauri Serikali sasa ijipange kuwa na fedha taslimu katika akaunti zake ili mtoa huduma huyu anapotoa huduma apate malipo yake kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hutoweza kupata bei ya soko kama mtu utamlipa ndani ya miezi mitatu, miezi sita au mwaka mmoja wakati mwingine mpaka miaka miwili inachukua mtu hajalipwa, halafu unategemea upate huduma ya soko, matokeo yake tutaweka sheria lakini sheria ambayo itakuwa haitekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ninao mfano hai kabisa ambao umetokea kwenye Mawakala wa Mbolea kwa mfano, Mawakala wa Mbolea wametoa huduma kwenye Serikali lakini leo wengine wana zaidi ya mwaka hawajalipwa na hivi vimesababisha matatizo makubwa sana kwa ucheleweshaji wa pembejeo kwa wakulima wetu. Kwa sababu hawa mawakala wamekosa sifa za kukopesheka katika mabenki, lakini pia wamekosa sifa za kukopesheka kwa wasambazaji wakubwa kupewa zile mbolea kuzipeleka kuzisambaza kwa wakulima wadogo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Serikali kwa jambo hili limekuja zuri na tumaimani kabisa litapunguza gharama za bidhaa na litaleta unafuu mkubwa kwa wananchi wetu, lakini sasa kwa imani tuliyokuwa nayo ya Serikali ya Awamu ya Tano ukusanyaji huu wa mapato nayo ijipange hivyo hivyo kurahisisha ulipaji wa fedha kwa watoa huduma ili waweze kutoa huduma kwa wakati na haya malalamiko kwa wananchi na sisi wenyewe yaweze kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili ambalo ushauri mwingine katika hili suala la mchakato wenyewe wazabuni ni hapa, kwa sababu ndio miongoni mwa matatizo makubwa kuna rushwa kubwa sana inafanyika katika mchakato huu wa manunuzi. Kwa sababu mchakato mrefu unahusisha watu wengi na lazima wale wanaosimama kwenye kutoa haki wanataka cha juu sasa watoa huduma wengi wanapigia hizo gharama zote kwenye bei ya bidhaa na bei hizi zote zinakuja kumlalia mlaji kule mwisho.

Kwa hiyo, ninaomba Serikali katika suala hili tuongeze uwazi ili bei ijulikane gharama halisi za bidhaa husika na ijulikane ni kipindi gani muhudumu akitoa huduma atalipwa na Serikali ili ikitokea serikali iki-*default* kumlipa yule basi kiwepo kipengele kabisa Serikali ibebe riba ya kulipa kwa kipindi chote ambacho itakaa na hizo hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia pamoja na kulipa hiyo riba ilipe fidia kwa mfanyabiashara yule ambaye katoa huduma na Serikali imechelewesha malipo, kwa sababu kwa kukaa na pesa ya mtoa huduma kwa kipindi kirefu unamsababishia yeye a-*block* yaani hafanyi biashara yoyote, hafanyi shughuli nyingine yoyote ya kiuchumi kwa ajili ya kujiongezea kipato, pesa zake unazo wewe kwa maana nyingine umesimamisha kila kitu yeye kwenda mbele kwaajili ya maendeleo. *(Makofi)*

Sasa sio kulipa riba tu lakini ni kumfidia ni faida gani angeipata kwa pesa ile kwa wewe kuwa nayo kwa kipindi kile lazima katika hili tuwe msumeno tusiwe visu tukate huku na huku. Kwa sababu mara nyingi watoa huduma waki-*default* kutoa huduma tuna-*cancel* mikataba yao na tunawafutia, lakini Serikali inapochelewesha kumlipa hata miaka mitatu anakuja kulipwa kiasi kile kile ambacho amechukua miaka mitatu iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunazungumza *value of money* tuzungumze *value of money* pande zote mbili hata kwa kuchelewesha pesa ile kwa muda mrefu Serikali inapaswa ibebe majukumu hayo ya kumlipa riba zake na pia faida aliyotaka kutarajia kuitengeneza ndani ya kipindi chote ambacho Serikali imeshikilia hela hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache nashukuru sana niwaachie wengine nao watoe mchango wao, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na mengi ya kuchangia siku ya leo na nilifanya tafiti za kutosha kuhusiana na marekebisho ya muswada huu hususani suala zima la tafsiri ambazo hazipatikani katika marekebisho ya sheria hii hata sheria mama hususani tafsiri kwa mfano *local firms* ambayo haipo katika sheria hii inayorekebishwa na hivyo wakati mwingine italeta tabu hapo baadae. Lakini pia nimeona Ibara ya 11 inayopendekeza marekebisho katika kifungu cha 31 ili kuondoa sharti la kubainisha katika kanuni la kusimamia ununuzi Halmashauri yaani Madiwani sasa kuondolewa katika usimamizi wa manunuzi yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kwamba siku ya leo nina majonzi na kwamba kwa kuwa wananchi wangu wamekatizwa haki ya kuishi

kwa mujibu wa Ibara ya 14 lakini pia kwa kuwa Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inatamka kwamba wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na Ibara ya 9 kwamba lengo kuu la Serikali itakuwa ni ustawi kwa wananchi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, majonzi haya yamenifanya nishindwe kuchangia siku ya leo na nitaomba nichangie kwa maandishi ili nishirikiane na ndugu zangu wa Rufiji ambao wameuwawa ikizingatiwa kwamba mmoja wa mtu aliyefariki ni ndugu bwana Ngayonga.

Kwa hiyo, naomba kwamba yale mapendekezo yaliyoletwa na Serikali mimi niaafikiana nayo na kwa siku ya leo kwa kuwa nina majonzi nitashindwa kuchangia, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa wachangiaji, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani za dhati kwako binafsi kwakuendesha vizuri majadiliano kuhusu muswada wa marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma *(The Public Procurement Amendment Act, 2016)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini kwa kuendesha vyema vikao vya Kamati ya Bajeti wakati ikijadili Muswada huu. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa maoni na ushauri mzuri ambao umesaidia sana kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kutambua michango iliyotolewa hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge, Serikali inakiri kwamba michango hiyo ilikuwa na afya. Aidha, hali hii ni kielelezo jinsi ambavyo Waheshimiwa Wabunge kama wawakilishi wa wananchi mmedhaminiwa kuhakikisha ununuzi wa umma ambao unatumia zaidi ya asilimia 70 ya bajeti ya Serikali unafanyika kwa ufanisi ili kupata ubora wa thamani iliyokusudiwa. Serikali imepokea ushauri huo na ninaahidi kwamba Serikali itafanyia kazi mawazo hayo mazuri yaliyotolewa. Ninawashukuru pia kwa pongezi za dhati zilizotolewa kwa Serikali kwa jitihada zilizofanyika kuandaa Muswada huu kwa kuzingatia maoni na ushauri wa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa nitoe ufafanuzi wa baadhi ya hoja za Kamati ya Bajeti pamoja na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Hoja ya kwanza ambayo imesikika sana na imeendelea kusikika hata leo asubuhi ni ile ya kuwaondoa Madiwani katika mchakato wa ununuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapema tulipowasilisha muswada huu kupitia kifungu cha 11 Serikali ilikusudia kufuta kifungu cha 31(4) cha sheria ili kuondoa jukumu la usimamizi yaani *oversight* la Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri katika masuala ya ununuzi wa Halmashauri. Hata hivyo baada ya kutafakari maoni ya kamati kupitia aya "D" ya jedwali la marekebisho Serikali imerejesha jukumu la Kamati kama ilivyokuwa awali. *(Makofi)*

Aidha, kupitia kifungu cha 20 cha Muswada Serikali imefuta kifungu cha 60(4) ili kuondoa sharti la Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri kutekeleza majukumu ya kiutendaji ya kufanya uchambuzi yaani *scrutiny* wa mikataba kabla ya tuzo kutolewa kwa mzabuni na Afisa Masuhuli. Hivyo basi, kifungu hiki kimefutwa ili Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri iendelee na jukumu lake la usimamizi yaani *oversight* na kuchukua hatua stahiki kwa watendaji pale ambapo watendaji wameshindwa kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ilikuwa ni kuweka tafsiri ya maneno *specialized goods and equipment* ili kuondoa utata katika utekelezaji wa sheria. Serikali inakubaliana na pendekezo la Kamati kwamba matumizi ya maneno *specialized goods and equipment* yanaweza kuleta utata katika utekelezaji wa sheria. Hata hivyo, badala ya kuweka tafsiri ya maneno *specialized goods and equipment* Serikali kupitia aya A ya jedwali la pili la marekebisho imeondoa neno *specialize* ili kuleta maana iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu, manunuzi ya Serikali yalingane na thamani ya fedha na kwamba gharama za ununuzi na matumizi ya magari zipunguzwe kupitia ununuzi wa jumla yaani *bulk procurement*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Ibara ya 3 ya muswada imeweka sharti kwa ununuzi wa bidhaa na huduma za Serikali kuzingatia thamani halisi ya fedha. Aidha, Serikali hivi sasa kupitia *GPSA* imekuwa ikifanya ununuzi wa jumla wa magari ambayo kwa kiasi kikubwa umeokoa fedha nyingi za Serikali ikilinganisha na utaratibu uliokuwa ukitumika awali kwa kuwa kwa kila Taasisi au Wizara kufanyaununuzi binafsi wa magari. Serikali itaendelea na utaratibu huu kupitia Ibara ya 23 ya Muswada ambayo inaweka utaratibu wa kuruhusu ununuzi wa bidhaa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile napenda kutoa taarifa kwamba Serikali imepokea na inafanyia kazi ushauri wa Kamati kuhusu umuhimu na uharaka wa kupunguza gharama za ununuzi na matumizi ya magari, ikiwa ni

pamoja na kutoa mikopo ya magari kwa watumishi wanaostahili badala ya kuwapa magari ya ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni uanzishwaji wa Mfuko wa Uwekezaji wa Wakandarasi ili kuweza kutoa dhamana wakati wa kuomba zabuni. Serikali imepokea ushauri wa kamati na itaufanyia kazi; hata hivyo ni vyema zaidi wakandarasi nao kupitia umoja wao watafakari namna ambavyo wanaweza kuweka nguvu pamoja kuanzisha mfuko unaopendekezwa. Serikali kwa upande wake itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Watanzania hususani katika sekta binafsi ikiwemo sekta ya ujenzi ili kuongeza ushiriki wa sekta hii katika uchumi kwa kuboresha huduma za upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kuimarisha soko la mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa kwamba Serikali itunge kanuni itakayobainisha vigezo vya uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Zabuni za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 31(3) cha sheria ya ununuzi wa Umma uundwaji wa bodi za zabuni katika Halmashauri hufanyika kwa mujibu wa kanuni zulizotayarishwa chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za mitaa sura ya 290. Kanuni ya 7 ya Kanuni za Uundwaji wa Bodi za Zabuni za Serikali zaMitaa imeweka bayana vigezo vinavyopaswa kuzingatiwa na Afisa Masuhuli wakati wa uteuzi wa wajumbe wa Bodi za Zabuni. Aidha, kanuni hizi imeweka sharti kwamba baada ya Afisa Masuhuli kuteuwa wajumbe wa bodi atapaswa kuwasilisha majina ya wajumbe pamoja na sifa zao kwenye Kamati ya Fedha na Mipango za Halmashauri kwa ajili ya kuidhinishwa na kuthibitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha Bodi za Zabuni za Halmashauri zinahusisha wajumbe wenye weledi wa kutosha ninatoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wajumbe katika Kamati za Fedha na Mipango za Halmashauri kutumia vizuri mamlaka yao ya kuidhinisha wajumbe wa Bodi za Zabuni za Halmashauri ili kupata watu wenye sifa stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba mapendekezo yaliyowasilishwa kupitia Muswada wa Sheria ya Ununuzi yataanza kutumika lini. Kwa mujibu wa kifungu cha 14 cha sheria ya tafsiri ya sheria mbalimbali Sura ya Kwanza, muswada huu utakapopitishwa na Bunge kuwa sheria utaanza kutumika tarehe ambayo utatangazwa na kuchapishwa katika gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ili kuwezesha utekelezaji wa mapendekezo ya muswada huu hivi sasa Wizara ya Fedha na Mipango ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha kanuni zitakazowezesha utekelezaji wake kuanza haraka iwezekanavyo. Kinachochelewesha kidogo ni kwamba ni

muhimu tuzingatie maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge katika ukamilishaji wa kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwepo hoja kwamba kanuni ziandaliwe ili kutoa fursa ya ushirikiano baina ya Halmashauri na wahisani katika utekelezaji wa miradi ya *PPP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kutoa ufafanuzi kwamba Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura ya 410 inasimamia masuala ya ununuzi yanayohusu fedha za Serikali pekee. Ununuzi katika miradi ya *PPP* baina ya Halmashauri na wahisani unapaswa kutumia taratibu za ununuzi ambazo zinasimamiwa chini ya kifungu cha 76 cha Sheria ya *Public Private Partnership* ambapo miradi ya *PPP* isiyozidi dola za kimarekani milioni 70 na umri wa miaka 15 inaidhinishwa na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kutokana na umuhimu wa miradi ya aina hii kwa wananchi Serikali tunapokea ushauri wa Kamati na tutaufanyia kazi kupitia kanuni hizo ambazo ziliandaliwa chini ya sheria ya *Public Private Partnership.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma zinatoa huduma kwa bei ya juu kuliko bei ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, yamekuwepo malalamiko mengi kuhusu Taasisi na Mashirika ya Umma yanayofanya biashara kutoa huduma kwa gharama za juu kuliko bei ya soko. Serikali katika kukabiliana na tatizo hili imechukua hatua, kwa mfano Ibara ya 24 imeweka utaratibu utakaoziwezesha Taasisi zinazojiendesha kibiashara kama *TEMESA*, *TBA* na *National Housing Corporation* kufanya manunuzi yake moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji ili kupata bidhaa kwa bei ya chini na hivyo kuziwezesha kuwa na unafuu wa bei pindi zitakapotoa huduma. Lakini vilevile Serikali kupitia Ibara ya 38 ya Muswada huu imeweka utaratibu utakaowezesha kuandaliwa kwa kanuni zitakazoweka utaratibu mahususi wa ununuzi utakaofuatwa na taasisi hizi na kuziwezesha kupata bidhaa na huduma kwa bei nafuu na hivyo kuwawezesha kuuza huduma au bidhaa wanazozalisha kwa bei ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize tu kwamba baada ya Serikali kuongeza nguvu katika ukusanyaji wa mapato na ninazidi kuwaomba Watanzania wote na Waheshimiwa Wabunge kulipa kodi ipasavyo ili kuipa uwezo Serikali kulipa watoa huduma kwa wakati. Kwa upande wetu Serikali itafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba watoa huduma wanalipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba majibu kuhusu hoja zilizowasilishwa na Kamati kupitia jedwali la marekebisho yaani *amendment schedule*. Pamoja na hayo maoni ya jumla ambayo nimekwisha kuyasemea Kamati ya Bajeti imetoa mapendekezo mengine katika hilo jedwali la marekebisho ambalo limewasilishwa hapa Bungeni. Ningependa kutoa majibu kama ifuatavyo:-

Moja ilikuwa ni kufuta Ibara ya 2(a) ya Muswada ili kuondoa tafsiri ya maneno *budget approving authority*. Serikali tayari imeridhia pendekezo hili lilipowasilishwa kwenye Kamati wakati wa mjadala wa muswada huu ambapo kupitia aya ya "A" ya jedwali la marekebisho la Serikali Ibara ya 2(a) imefutwa ili kuondoa tafsiri hiyo kama ilivyopendekezwa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inakubaliana na mapendekezo ya kiuandishi yaliyobainishwa katika aya ya "A", "B" ya jedwali la marekebisho la Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo lingine lilikuwa ni kuweka tafsiri ya maneneo *local firms* ili ihusishe kampuni zinazomilikiwa na watanzania kwa asilimia 100 pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakubaliana na pendekezo la tafsiri ya maneno haya kama yalivyobainishwa katika aya ya "A", "C" ya jedwali la marekebisho ya Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuweka tafsiri ya maneno *life saving commodities* na kurekebisha kifungu cha 67 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ili kuweka utaratibu wa ununuzi wa *lifesaving commodities*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yaliyobainishwa katika aya ya A, "D", "C", "B", "D" ya jedwali la marekebisho ya Kamati ya Bajeti yana malengo yafuatayo:-

Kwanza ni kuweka utaratibu wa ununuzi wa *life saving commodities* ndani ya sheria na pili ununuzi wa *life saving commodities* ufanyike kwa utaratibu wa dharura *emergence procurement*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ufafanuzi kwamba ununuzi wa dawa na vifaa tiba ikiwemo *life saving commodities* tayari umebainishwa chini ya kanuni ya 139 hadi 147 ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma. Aidha, kupitia Ibara ya 24 ya Muswada SerikaLI imeweka utaratibu utakaowezesha ununuzi wa bidhaa ikiwemo dawa na vifaa tiba kutoka kwa wazalishaji moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ununuzi *wa life saving commodities* kufanyika kwa utaratibu wa dharura, Ibara ya 65 ya Sheria ya Ununuzi wa Umma tayari imeweka utaratibu wa ununuzi wa dharura na mazingira yake. Chini ya utaratibu huu, ununuzi wa dharura unahusisha bidhaa au huduma ya aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati ina marekebisho katika Ibara ya 24 ya Muswada kwenye Ibara ya 65B(1). Serikali inakubaliana na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti ya aya ya C(a)(i),(ii) na (iii) yaliyobainishwa kwenye Jedwali la Marekebisho la Kamati ambayo yana lengo la kufanya marekebisho ya kiuandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo juu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge wengine. Hoja moja ilikuwa ni kuweka masharti kwa taasisi nunuzi kununua bidhaa zinazopatikana hapa nchini. Serikali imetekeleza ushauri huu ambapo kupitia Ibara ya 18 ya Muswada imebainisha utaratibu wa kutoa upendeleo maalum kwa kampuni zitazotumia bidhaa au malighafi zinazozalishwa Tanzania. Kampuni za aina hii zitapewa upendeleo maalum pindi zitakaposhiriki katika zabuni za Serikali tofauti na kampuni ambazo zitatumia bidhaa au malighafi zinazozalishwa nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni bei ya bidhaa na huduma zinazopangwa na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (*GPSA)* kwamba ni kubwa na haziendani na bei za soko. Serikali kupitia Ibara ya 17 ya Muswada imefanya marekebisho katika Ibara ya 50 ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ili kwanza kuondoa sharti la kuwepo kwa mikataba baina ya Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (*GPSA)* na wazabuni iliyofungamanishwa na bei ili kuondoa utaratibu wa kupanga bei elekezi na badala yake taasisi nunuzi zitafanya utaratibu wa ununuzi kwa kuzingatia bei ya soko kwa wakati husika. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama ya ununuzi kupitia taasisi hii ambayo imekuwa ikilalamikiwa kwa kipindi kirefu. Pili, ni kufafanua tafsiri ya *open framework agreement* ili kubainisha mikataba baina ya *GPSA* na wazabuni haitahusisha bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa kwamba *National Board of Materials Management* hawakushirikishwa kwenye mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma. Napenda kutoa taarifa kwamba iliyokuwa Bodi ya Wataalam ya Ununuzi na Ugavi (*NBMM)* ilifutwa na Serikali kupitia Sheria ya Bodi ya Wataalam na Ununuzi na Ugavi *(Procurement and Supplies Professionals and Technicians Board Act*) na kuundwa chombo kingine ambacho kinaitwa *Procurement and Supplies Professionals and Technicians Board (PSPTB)*. Bodi hii ndiyo yenye dhamana ya kusimamia wataalam wa masuala ya ugavi. Aidha, katika hatua zote za maandalizi ya Muswada huu *PSPTB* imehusishwa kwa kiasi kikubwa. Hata navyozungumza, wataalam wake ni

sehemu ya timu ya wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango iliyoshiriki katika majadiliano ya Muswada huu kwenye Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kwamba sifa za Mtendaji Mkuu wa *PPRA* ziwe zinatambulika na Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi. Kwa mujibu wa Ibara ya 23(3) ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Mtendaji Mkuu anaweza kuwa mtu mwenye sifa zozote za elimu kama ilivyobainishwa kwenye Muswada na ambaye ana ujuzi katika masuala ya ununuzi. Hivyo, kutokana na sharti hili mtu ambaye hana ujuzi katika masuala ya ununuzi hawezi kuteuliwa katika nafasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba Kanuni za Ununuzi za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu zifanane ili kupunguza uvunjifu wa taratibu za ununuzi wa umma. Serikali imepokea mapendekezo haya na tutayafanyia kazi pasipo kuathiri dhana ya ugatuaji madaraka *(D by D)*. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, palikuwa na hoja pia kwamba ununuzi wa dawa na vifaa tiba uwekewe utaratibu tofauti. Kama nilivyokwishaeleza wakati nikijibu hoja za Kamati ya Bajeti, tayari utaratibu maalum wa ununuzi wa madawa na vifaa tiba umebainishwa chini ya Kanuni ya 139 - 147 ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma zikisomwa pamoja na Ibara ya 24 ya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba, je, *GPSA* itaedelea kuchagua wazabuni na itaendelea kutoza asilimia mbili ya thamani ya zabuni? *GPSA* itaandaa orodha ya wazabuni kwa ajili ya kupunguza muda na gharama kwa niaba ya taasisi za Serikali. Hata hivyo, utaratibu huu hautahusisha kupanga bei ya bidhaa au huduma. Aidha, kupitia marekebisho yatakayofanywa kwenye Kanuni, Serikali itafanya mapitio ili kupunguza kiwango cha asilimia 2 kinachotozwa na *GPSA* kwenye kila thamani ya zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba sheria iweke wazi kiasi kitakachotengwa kwa ajili ya makundi maalum. Kwa mujibu wa Ibara ya 22 ya Muswada, kanuni zitakazoandaliwa baada ya kupitishwa kwa Muswada huu zitabainisha viwango mahsusi vya thamani za zabuni za taasisi nunuzi zitakazotengwa kwa ajili ya makundi ya vijana, walemavu na akina mama. Lengo la kubainisha viwango hivyo kupitia kanuni, ni kuweka urahisi wa kufanya mabadiliko wakati wowote endapo viwango husika vitaonekana ni vidogo pasipo kusubiri kuwasilisha tena hapa Bungeni. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba viongozi wa mikoa waache kuingilia Bodi za Zabuni za Halmashauri. Sheria ya Ununuzi wa Umma inasisitiza uhuru wa Bodi za Zabuni katika kutekeleza majukumu yake. Kuingilia shughuli za bodi ni uvunjaji wa sheria na kanuni zinazosimamia ununuzi katika halmashauri. Hivyo, napenda kutoa rai kwa viongozi wa mikoa kuzingatia

utaratibu uliowekwa kisheria. Kanuni ya 33 ya Kanuni za Kusimamia Ununuzi wa Umma inaelekeza ni wakati gani viongozi wa mikoa wanaweza na wafuate utaratibu gani kisheria pale ambapo inaonekana pana haja ya kuingilia michakato hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu pika, naomba nimalize kwa kusema yafuatayo:-

(i) Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2016 ni ahadi ya Serikali kupitia bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/2017 ambapo nilibainisha kwamba Serikali itawasilisha Muswada huu katika Mkutano huu wa Bunge unaoendelea.

(ii) Pamoja na mambo mengine, umuhimu wa Muswada huu kwanza ni kutekeleza azma ya Serikali katika bajeti ya kuwa na matumizi bora ya fedha za Serikali kwa kuwa na sheria madhubuti ya ununuzi wa umma na kuziba mianya ya upotevu wa fedha katika ununuzi wa umma na kuhakikisha ununuzi unawiana na thamani ya fedha itakayotumika.

(iii) Kutekeleza ahadi ya Serikali katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya kuwezesha kiuchumi makundi maalum na hususani vijana, wanawake na walemavu kwa kuweka upendeleo maalum kwa makundi haya ili kuyawezesha kushiriki katika zabuni za Serikali ili kuongeza ajira na kipato. *(Makofi)*

(iv) Kuiwezesha Serikali kusimamia utekelezaji wa kaulimbiu ya ujenzi wa viwanda, kuongeza uzalishaji viwandani na kupanua fursa za ajira kwa Watanzania kwa kuweka mazingira mazuri ya soko kwa bidhaa na malighafi zinazozalishwa hapa nchini kwa kuhimiza matumizi ya bidhaa na huduma hizo kama kigezo cha upendeleo katika kupata zabuni za Serikali.

(v) Kujenga uwezo wa wataalam wa Watanzania pamoja na kampuni zinazomilikiwa na Watanzania kwa kuwapa fursa zaidi kushiriki katika miradi ya Serikali kwa kupitia kampuni hizo moja kwa moja au kwa kushirikiana na kampuni za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge mridhie na kuupitisha Muswada huu ili kuiwezesha Serikali kutimiza azma yake ya kulinda matumizi ya fedha za Serikali, kukuza uchumi wa nchi na kuweka mazingira ya kuwawezesha kiuchumi wananchi wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono tutaendelea na taratibu zinazofuta, Katibu.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

Kamati ya Bunge Zima.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu.

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwenye ile *definition* ya *local firm* kwa sababu wamechukua ile *definition* ambayo Kamati ilipendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, napendekeza ku-*insert immediately* baada ya ile *definition* ya *local firm the following definition*. Kwanza, *life-saving commodities* ambayo tumetoa *definition* kwenye *schedule of amendment* kwa sababu hazipo kwenye Sheria ya Manunuzi. Kwa hiyo, naomba iongezwe *definition* hii inayosemeka:-

*"Life-saving commodities including medicine, medical devices and health supplies that effectively address leading avoidable causes of death during pregnancy, childbirth and childhood as the same may be modified from time to time by the order from time to time by the Minister responsible for health by order published in the Gazette".*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyofafanua Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anahitimisha hoja yake, suala hili limezungumzwa vizuri katika Sheria yenyewe hii ya Manunuzi ya Umma, Ibara ya 65 na kanuni zipo. Kimsingi yale yaliyopo kwenye sheria yenyewe ni mapana zaidi, yanajibu hoja ya Mheshimiwa Mbunge au Kamati, kama ni lazima hayo kuwepo, basi tutaingiza kwenye kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo kanuni hizi hapa, kama haya mambo hayapo *captured,* tutaingiza kwenye kanuni. Kwa mfano, Ibara ya 65 inasema hivi, *for the purpose of subsection (1), emergency procurement shall meet one of the following criteria:* Kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wanachopendekeza ni kuwezesha vitu hivi vya kuokoa maisha ya vinunuliwe kwa dharura. Sasa mfumo wa sheria tayari umewekwa na imeeleza hivi, (a) *compelling urgency that creates threats to life,* ndiyo kama haya anayozungumzia ya mama mjamzito, *health* (afya*), welfare or safety of public by reason of major natural disaster, epidemic, riot, war, fire or such other reasons of similar nature.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kifungu kidogo cha (4) kimetoa mamlaka kwa Waziri kutengeneza kanuni kwa ajili hiyo na kanuni zimetengenezwa vizuri. Ukisoma ile kanuni ya 64, 65, 66 kwenye zile Kanuni za Manunuzi ya Umma, *Government Notice* Na.446 ya Disemba, 2013 zinayagusa hayo. Kama kuna upungufu na maadam Mheshimiwa Waziri ameshapewa mamlaka haya, tunaipokea hoja ya Kamati halafu tutaiingiza humu ndani kama tukiona kuna unafuu lakini sheria jinsi ilivyo sasa hivi tunaona ni nzuri kwa sababu hii inakuwa *all inclusive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri hivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wanaona umuhimu wa hizi *life-saving commodities* kushughulikiwa ipasavyo, sioni kama kuna ugumu wowote kuingizwa kwenye Sheria ya Manunuzi badala ya kuweka kwenye kanuni ambapo inaleta utata. Tulipokaa na wadau hili ni eneo ambalo wamelilalamikia kwamba inategemea ni nani wakati huo anatafsiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani ili ikae vizuri nashauri ikae kwenye sheria, itafsiriwe vizuri na ikikaa kwenye kanuni huko hakuna tatizo lakini ianzie kwenye Sheria ya Manunuzi. Kwa sababu mtu kitu cha kwanza anachoangalia ni sheria, hizo kanuni zinatazamwa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba iingizwe kwenye sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla hujasimama, Mheshimiwa Adrew John Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kuimarisha hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili limesemwa sana na wadau na siyo mara ya kwanza kwenye mkutano huu lakini hata mkutano uliopita. Maadam sasa tumepata nafasi ya kuinyoosha sheria, ni vyema msingi wa haya yanayosemwa kwenye tafsiri ya *life-saving commodity* yakaanzia kwenye Sheria Mama. Huo ndiyo msingi wa utungaji wa sheria, kanuni zinaenda kufafanua yale yanayotokana na msingi wa Sheria Mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naungana na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti kwamba tuweke kwenye Ibara ya 3 ambapo ndiyo kwenye *definition*, *definition* inayopendekezwa na Kamati na baadaye tutakaa vizuri tu hata kwenda kunyoosha sasa kwenye kanuni ambayo ni mamlaka ya Mheshimiwa Waziri itakuwa rahisi sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla haujasimama ili Bunge litakapokuwa linatoa maamuzi tuwe na uhakika. Matumizi ya neno '*life-saving commodities*' kwenye Sheria Mama na kwenye mapendekezo mliyoleta ipo? Kwa sababu kuweka kwenye maana ya maneno ikiwa maneno hayo hayakutumika kwenye ile sheria itakuwa haitusaidii chochote. Lazima maneno '*life-saving commodities*' yawepo kwenye Sheria Mama, sasa utusaidie, wakati unajibu, ujibu yote hayo kwa pamoja. Kama neno '*life-saving commodities*' yapo humo na umuhimu wake wa kupewa maana, kama haya maneno hayajatumika humo utusaidie yatatumika kwenye eneo gani ili yote tuyafanye hapa wakati wa haya marekebisho. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru na ndiyo msingi wangu pia au wa Serikali wa kusema hayo tuliyosema, Ibara ya 65 jinsi ilivyo inajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ukija na hii *scheme* ya '*life-saving commodities*' ukai-*define* itakupelekea ufanye mabadiliko katika vifungu vingi kwa sababu sheria hii jinsi ilivyo haina neno hilo '*life-saving commodities*'. Kwa hiyo, uki-*introduce* tu hii hapa itabidi utengeneze vifungu vingine vya ku-*address* hiyo *issue*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema kwa sababu ni suala la manunuzi ya dharura kwa ajili ya kuokoa uhai, akina mama wajawazito na binadamu wote na *calamities* zote, sheria hii Ibara ya 65 imeweka mazingira ya kushughulikia masuala hayo tena imeondoa kabisa na urasimu. Ibara ya 65

inasema wata-*wave* zile *procedure* nyingine za kutangaza na kadhalika halafu watapata *retrospective* kibali. Kwa hiyo, ndiyo tunasema kama haya ambayo yanayozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ni muhimu na sisi tunakubali maadam Mheshimiwa Waziri amepewa mamlaka atayaingiza mule ndani kwenye kanuni kwa sababu atapata uhalali wake kwenye hii Ibara ya 65.

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nitoe hoja kwamba suala hili lijadiliwe, tunaiweka hii *definition* kwa sababu kuna kifungu ambacho tunataka kingie kiko kwenye Ibara ya *24*, baada ya Ibara ya *65*, kwenye *Principal Act* iingie Ibara ya *67*(3) ambapo tunataka isomeke:-

"*67(1) Life-saving health commodities, supplies and equipment will be treated as items of the national interest in their procurement. The procuring entity shall, in consideration of the importance and nature, upon satisfying the conditions stipulated in subsection (2), first-track their procurement process or use emergency procurement.*

*(2) Where a procuring entity seeks to procure life-saving health commodities, supplies and equipment pursuant to subsection (1), it shall seek approval of the Minister.*

(3) *Where the procurement referred to under subsection (1) is to be done under emergency procurement, the procedure stipulated under section 65 shall, within necessary modification, apply*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo anayosema kwamba tutabadilisha na maeneo mengine ni kweli tumeandaa ndiyo maana tunaanza na *definition* ili kule mbele kile kifungu kiweze kuingia. Kwa hiyo, naomba Wajumbe waniunge mkono kwa sababu wakati mwingine zile *family plan item* hawazioni kama ni *emergency procurement* lakini kwa mama ambaye anafuata uzazi wa mpango ukimcheleweshea zaidi ya miezi minne ukiona kwamba hizo *item* hazina umuhimu maana yake utamsababishia *unwanted pregnant*. Kwa hiyo, naomba hasa akina mama wenzangu wasimame na wachangie katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Samahani Waheshimiwa, mniwie radhi mkae kidogo. Nafikiri ili tuliendeshe jambo hili vizuri, tukianzia kupitisha kwenye *definition* halafu tukafika kwenye kifungu chenyewe tukakikataa tutakuwa hatujaenda vizuri.

Kwa sababu *definition* tutakuwa tumeshaihoji itabaki pale wakati vifungu vyake hatujaviangalia.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tukubaliane kwa sababu wakati wa kutoa hoja Mheshimiwa Hawa Ghasia ameenda kwenye kile kifungu ambacho ndiyo kitayaleta sasa hayo maneno anayopendekeza yaingie, pendekezo langu ni kwamba, tutaruka hivi vifungu vingine vyote tuende kwenye hayo mapendekezo yatakayotutaka tutafute maana ya hayo maneno. Tukikubali hii maana kabla hatujakikubali kile kifungu kwamba tunakubaliana na Kamati tutakuwa hatuendi sawasawa kwa sababu hayo maneno hata tukipata maana yake haitatusaidia kama kwenye vifungu hayajatumika.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tutaelekea kwenye Ibara ya 24 katika mapendekezo ya Kamati, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati nitamsimamisha baadaye kidogo lakini ameshatoa mwelekeo wa nini anachokipendekeza kwenye Ibara hiyo. Kwa sababu Ibara hii ndiyo itakayotutaka tuweke maana ya maneno, tutaanza nayo kwanza halafu tutarudi kwenye maana ya maneno.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati wakati akimalizia hoja yake aliomba Waheshimiwa Wabunge wamuunge mkono, naomba nimuombe tuahirishe mjadala wa maana ya maneno tuje kwenye Ibara mahsusi. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati utatoa maelezo kwa ajili ya Ibara mahsusi ya 24, Katibu.

Ibara ya 24

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutayaangalia marekebisho yote kwenye Ibara hii ili tuyamalize. Tutaanza na mapendekezo ya mabadiliko ya Kamati. Mheshimiwa Andrew Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ili twende vizuri na Wajumbe wa Kamati yako, napenda twende kwenye marekebisho ya Kamati ambayo ni kipengele C kwenye *schedule of amendment,* Ibara ya 24 lakini tushuke kwenye (b) ambayo inasema:-

*"Designating section 67 of the Principal Act as 67(3) and adding the following as subsections (1), (2) and (3) of section 67".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sheria ilivyo sasa hivi Ibara ya 67 haina mtoto, iko peke yake. Kwa hiyo, tunapendekeza kilichopo kwenye sheria ndiyo kiwe kifungu cha (4) maana tunaongeza kifungu cha (1), (2)na (3). Ibara ya 67 inayopendekezwa ambayo ipo kwenye *schedule of amendment* ya Kamati inasema:-

*"(1) Life-saving health commodities, supplies and equipment will be treated as items of the national interest in their procurement. The procuring entity shall, in consideration of the importance and nature, upon satisfying the conditions stipulated in subsection (2), first-track their procurement process or use emergency procurement.*

*(2) Where a procuring entity seeks to procure life-saving health commodities, supplies and equipment pursuant to subsection (1), it shall seek approval of the Minister.*

(3) *Where the procurement referred to under subsection (1) is to be done under emergency procurement, the procedure stipulated under section 65 shall, within necessary modification, apply".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo mapendekezo ya msingi kwa muktadha wa mapendekezo ya tafsiri ambayo ilikuwa inapendekezwa na Kamati kwenye Ibara ya 3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Ibara yenyewe ya *67 spirit* yake ni *competitive tendering*. Ukiingiza hii anayopendekeza Mheshimiwa Mtemi Chenge au Kamati lazima uta-*create* tatizo. Ndiyo maana manunuzi haya ya dharura yamewekewa utaratibu wake mahsusi chini ya Ibara ya 65. Hata vipengele anavyopendekeza viingizwe *does not serve any purpose* kwa sababu mambo yote ya *wave of procedures* yamewekwa pale. *Because you want to save life,* kwa nini iwe tu *life saving* hiyo? Haya yaliyopo hapa kwenye hii Ibara ya 65 yote ni *towards life saving.* Moja, *threat to life and then health, welfare or safety of the public by reason of major natural disaster,* siyo lazima yawe madawa tu, inaweza hata kuwa na vitu vingine. *Epidemic* ni magonjwa haya ya mlipuko, halafu *riot, war, fire or such other reasons of similar nature.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo tukasema haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wamependekeza kwenye Kamati ni mambo ya msingi sana lakini sheria jinsi ilivyo imeya-*capture* kwa upana wake. Tukiweka kwenye sheria humu kila siku itabidi mrudi hapa mrekebishe lakini sheria imempa madaraka Mheshimiwa Waziri wa masuala ya fedha ambaye ndiye mwenye dhamana ya sheria hii atengeneze kanuni. Kanuni ya 139 na kuendelea zimeweka utaratibu wa namna ya ku-*procure* madawa lakini kwenye *emergency* hii sheria inatusaidia ukisoma pamoja na Kanuni ya 63 - 66.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashauri hivi Waheshimiwa Wabunge, tukiweka kwa namna ambayo mnapendekeza tutakuwa tunatengeneza *loophole* nyingine ya watu kukwepa utaratibu wa kununua madawa kwa sababu hakuna mtu ambaye hajali uhai wa mtu. Leo tukiuliza swali hapa hivi ni kweli kwamba kuna watu wamekufa kwa sababu madawa yamechelewa kuwa *procured,* tutapata majibu hayo? Tusije tukatengeneza sheria Waheshimiwa Wabunge ambayo ina-*create* tatizo ambalo tunajitahidi kulikwepa. Sisi tunaona hoja yao lakini tunasema hoja hii tayari imeshakuwa *captured* kwenye ile sheria katika Ibara ya 65 inayotoa fursa ya manunuzi ya dharura ili kuokoa uhai iwe kwenye janga lolote lile, liwe la moto, liwe la uzazi ili mradi tu maisha ya binadamu yanatishiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona tukienda kwa pendekezo ambalo Waheshimiwa Wabunge wanalisema, hii sheria itabidi tuibadilishe sana, ile *scheme* yake itabadilika. Kwa sababu siamini kwa mtu ambaye ana akili timamu na anaona kuna tatizo la madawa akasema naku-*subject* kwenye hii *competition* wakati sheria imeshakataza kwamba bwana hii ina *short-cut* yake. Tukilipendekeza hilo mnalolipendekeza *loophole* nyingine nayoiona itakuwa ni mwanya pia wa kukwepa *procedure* hizi za manunuzi kwa namna nyingine hata pale ambapo hakuna *emergency* unasema mimi napita *short-cut.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba kushauri mapendekezo haya jinsi ambavyo Serikali imeyaleta yabakie jinsi yalivyo kwa maana moja kwamba utaratibu huu tayari umewekwa kwenye Sheria Mama. Ndiyo maana hata wao wanafanya rejea tena kwenye Ibara ya 65 ya Sheria Mama lakini hicho cha kwao wanachopendekeza ni chembamba sana (*narrow),* ile Ibara ya 65 *all are inclusive,* ina-*take care of all eventualities* lakini pia hiyo *life-saving whatever* si ndiyo hayo unataka ku-*save* yamewekwa hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndiyo ushauri wangu huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Simba.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi napata tabu kidogo, kuna *procurement* ya *emergency* na hapa sisi tunazungumzia *life-saving procurement commodities*. Tunataka utaratibu mzuri wa kuweza kununua haya madawa, madawa yana *priorities* zake, ndiyo tunachotaka kufanya. Ukisema sasa madawa uyatumbukizwe kwenye *emergency* siyo kila siku ni *emergency*, ununuzi wa madawa uwe una utaratibu wake ili kupunguza matatizo haya ambayo yanatukuta kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sielewi kwa nini tunapata shida hapo. Kwa nini tuweke kwenye kanuni wakati tunatunga sheria? Tunataka tuhakikishe hapa haya madawa ambayo siku zote yanatupa tabu leo tunayawekea utaratibu

mzuri. *Emergency* ni kama kumetokea mafuriko, tunataka kununua boti ya haraka haraka kusafirisha watu Dar es Salaam kuna mafuriko, pale mimi nitasema *emergency* lakini madawa yananunuliwa kila siku na yanahitajika yapatikane pasi kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu akubaliane na hoja hii, sioni sababu kwa nini tuifiche kule kwenye kanuni? Mimi nazijua hizo kanuni, kila Waziri atakayekuja ana yake. Waziri mwingine anaweza kuona hii siyo *priority* kutungia kanuni. Kwa hiyo, namsihi sana aone uzito wa haya madawa ambayo manunuzi yake tumekuwa tukipata nayo tabu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu inabidi tuifikishe mwisho hoja hii, nitamsikia Mheshimiwa Kangi Lugola, tutarudi kwa mtoa hoja halafu tutamaliza.

**MHE. KANGI A.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mwanasheria Mkuu wa Serikali anapokuwa anapinga hoja zinazotolewa katika mabadiliko haya na Kamati ndiyo maana sheria hizi zinakuwa mbaya matokeo yake tunalazimika kuzibadili kila wakati kwa sababu mawazo ya Wabunge yanapuuzwa kila wakati. Kila wakati wanachosema Serikali wanakisimamia kiwe hicho hicho ndiyo matokeo yake yanakuwa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema, kuna tofauti kubwa kati ya *emergency procurement* anayozungumzia Mwanasheria Mkuu pamoja na hii *life-saving commodities.* Kwenye masuala ya afya ni masuala ya maisha, maisha siyo dharura, maisha ni kila siku tunataka yawe yameboreshwa. Akina mama wanaenda hospitali kitu kipo muda wote lakini haya mambo ya *emergency* ndiyo hayo shule imeezuliwa hatukutarajia shule iezuliwe lakini inatokea lakini maisha ni kila siku tunayatarajia tuwe nayo. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kubali hili litakapoleta shida tutakuja turekebishe mbona haya mengine yanaleta shida mnaleta hapa turekebishe, kuna tatizo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu ni hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilisema nitarudi kwa mtoa hoja. Mtoa hoja wakati ukikamilisha hoja yako tusaidie, kwenye *definition* ile mliyopendekeza niliyonayo mimi hapa inasema: *Life-saving commodities includes,* ikataja hapa mambo kadhaa. Ukienda kwenye hivi vifungu vinavyopendekezwa kuingizwa kwenye Ibara ya 67 vinaongelea '*life-saving health commodities*'. Sasa utusaidie kama hicho ni kitu kimoja au hii *definition* ni ya kitu kingine kwa sababu yale maneno tunapo-*define* lazima yafanane na yale tuliyoyatolea *definition.* Kwa hiyo, wakati wa kufunga hoja tusaidie hilo ili

Waheshimiwa Wabunge waweze kufanya maamuzi juu ya hili na hilo liko pia kwenye mapendekezo mengine kwa hiyo tusaidie tu hapo.

Mheshimiwa Chenge, kabla hujasimama, kwa sababu ukiliweka kwenye *life-saving commodities* bila kutaja *health* maana yake na yale mengine yanaweza yakaingia hapo kwa mfano, magari ya zima moto ni *life-saving, I suppose* lakini sidhani kama ndiyo ilikuwa *spirit* ya Kamati. Kwa hiyo, tusaidie hii *definition* hapa inasema '*life-saving commodities*' huku kunasema '*life-saving health commodities*'. Mheshimiwa Andrew Chenge kwa niaba ya Kamati.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nafanya kazi hii kwa niaba ya Mwenyekiti. Kwanza, ni kwa sababu ya *pressure* ya muda na ndiyo maana unaona kuna *typo errors* mtaziona siyo kwenye eneo hili tu lakini hata kwenye maeneo mengine ambayo yanakuja. Ndiyo maana jana tulipoiomba Serikali tupate muda wa kutosha naamini lengo lilikuwa ni hilo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo tunachokitafuta ni *life-saving health commodities*. Kwa hiyo, kwenye *definition* kule lile neno '*health*' na nilikuwa nisimame kama tungeendelea, nashukuru busara yako uliyoitumia tuanze na Ibara hii lakini ni *health* ili tujue sasa tunaji-*confine* katika masuala ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoelezewa kuna sura mbili hapa, ya kwanza ni kuharakisha mchakato wa kupata madawa na vifaa tiba kwa mama na mtoto, ndiyo dhana hii unaiona kwenye kipengele cha (1) na (2). Kipengele cha (3), ndiyo sasa inakuja kwenye *emergency*. Ni vyema Serikali wakaliona hilo kwamba kuna *concept* mbili hapo katika Ibara ya 67 inayopendekezwa lakini kwa *clarity* uliyoitaka kwa Kamati yako ni *life-saving health commodities,* ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** La mwisho kabla sijahoji Wabunge, hapa mmetumia neno '*national interest*' mlimaanisha '*public interest*' kwa sababu *Act* inazungumzia *public interest.* Mtusaidie kama tubadilishe hilo neno '*national*' hapa tuweke '*public*' halafu tuhoji Wabunge au ni neno '*national*' kama mlivyoweka ni sahihi tuendelee kuhoji.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sheria unapoitunga lazima iwe na usare wa maneno ambayo yametumika, napenda niwashawishi Wajumbe wa Kamati yako na hapa nachukua tu dhamana kwa niaba ya Mwenyekiti kwamba tutumie lugha ambayo imo kwenye Sheria Mama sasa hivi ile ya '*public interest*' ambayo ndiyo tunaitafuta. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa hapa hii Ibara tuliyonayo ya 24 nadhani nihoji kwa mapendekezo haya halafu tutaenda kwenye mengine

kwa sababu hayafanani. Kwa hiyo, tutaangalia mapendekezo ya hao wengine kama mapendekezo ya Kamati yatakuwa yameyafuta ama vipi, nadhani tumalize hii hoja ya Kamati, kwa hiyo nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawasawa, yale marekebisho yaliyoletwa na Kamati kwa sababu tulianzia Ibara ya 24, maneno yaliyokuwa yanasomeka *national interest*, neno '*national*' unaweka pale '*public*'. Kwa hiyo, tumehoji pakiwa na neno '*public*'.

Waheshimiwa Wabunge, sitawahoji kwenye Ibara nzima kwa sababu tunayo mapendekezo ya Mheshimiwa Tibaijuka na Mheshimiwa Kakunda. Mheshimiwa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, naomba niseme…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka, naomba ukae kidogo. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatujapata fursa ya kuyaona hayo mapendekezo yanayopendekezwa na Mheshimiwa Profesa Tibaijuka labda tupate *copy* yake.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mmegawiwa, hata hivyo twende kwenye hiyo Ibara ya 24, mapendekezo ya Mheshimiwa Tibaijuka anasema yaongezwe maneno '*or contractors*' baada ya neno '*providers*'. Twende hapo kwenye hiyo Ibara ya 24 inayorekebisha Ibara ya 65A, anataka baada ya neno '*provider*' hapa mwisho yaongezwe maneno '*or contractors*'. Sijui kama tupo pamoja Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, umepata nakala? Wengine mnazo nakala za mabadiliko ya Mheshimiwa Tibaijuka? Wengine wanazo. Waheshimiwa Wabunge, mtakuwa mmegawiwa kwa sababu sidhani kama yalienda yakiruka, kwa hiyo, yaangalieni kwenye meza zenu tafadhali. Mheshimiwa Tibaijuka endelea.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, sina budi kuipongeza Serikali, kumpongeza pia na Mheshimiwa Rais kwa kutekeleza ahadi yake ya kutusaidia kurekebisha Sheria hii ya Manunuzi ambayo ilikuwa imeshaleta ukakasi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu kwa mtoa hoja ni boresho tu. Nimeangalia hiki kifungu hapa wanasema, *procurement directly from*

*manufacturer, dealer or service provider* nikaona ili sheria iwe na uhakika kabisa na *contractors* pia wanaweza wakahitajika katika kifungu hiki. Kwa hiyo, napendekeza kwamba, '*or contractor*' aongezwe ili sheria isaidie yule mtekelezaji sheria asibaki ku-*guess* kama *contractor* ni *provider* au ni *supplier* au ni mtu gani. Kwa hiyo, pendekezo langu ndilo hilo la kwanza kwenye *side note* kwamba hiyo *principle* ina-*deal* pia na *contractor*. Kwa wale ambao wamepata sasa hizi *amendments* zangu hiyo ndiyo mantiki yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo katika hiyo Ibara ya 65A napendekeza tuongeze neno '*timely*' kati ya maneno '*and delivery*' kwa sababu tatizo letu ni ucheleweshaji na fedha zinakuwa zimepotea katika ucheleweshaji usio wa lazima. Kwa hiyo, *timely delivery* nayo ni *value for money.* Kwa hiyo, ni ongezeko tu la hayo maneno kusudi sheria ikae vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa MWenyekiti, mwisho chini ya Ibara hiyo ya 65A(1), tunaposema *dealer, wholesaler or service provider,* kwenye *submission* yangu nimeandika '*and*' kuna sahihisho hapo, *or a contractor resident or operational in an area with established capacity for a rapid and cheaper mobilization of works.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kama ifuatavyo. Hapa tunajaribu kuboresha na mantiki nzima ni kutuondoa kwenye sheria iliyokuwa inatuletea hasara badala ya kutusaidia ili tupate faida. Kuna huduma nyingine ni kutoka kwa *contractor* ambaye yupo mahali fulani labda ni *contracto*r mkubwa yuko pale, unataka afanye kitu kwa haraka kwa sababu yupo pale, kwa sheria ya sasa hivi huwezi kumtumia maana watasema hujaenda kwenye *competitive tender* lakini angalia fedha zinavyopotea. Kama *public procurers* maana hii ni *public procurement* hawana uwezo wa kitu kinaitwa *direct shopping* kila wakati tunapoteza muda katika urasimu. Kwa hiyo, pendekezo hili ni kuboresha tu kitu kizuri ambacho tayari kiko mbele yetu tuondokane na urasimu na makandarasi waliopo mahali fulani wanaweza kuombwa kufanya kazi fulani kwa sababu hawana gharama za *mobilization*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba umalize hoja yako.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja yangu mantiki yake ndiyo hiyo, *essence in the same* kwamba na makandarasi wanaweza pia katika mazingira fulani…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele iligonga, sijui kama uliisikia?

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisikia, samahani.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu za msingi zilizofanya Serikali ikaleta mapendekezo haya ya kununua bidhaa hizi kutoka kwa watengenezaji wenyewe moja kwa moja ilikuwa ni kurahisisha upatikanaji wa hizi *goods* kwa urahisi lakini pili ni kuokoa fedha nyingi sana kwenda kwa watu wa kati hapo katikati, ndiyo tukasema tununue moja kwa moja kwa anayetengeneza. Huyu *contractor, a firm, a company whatever,* hapana, hawa wataongeza tu gharama, *we want to save this cost. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Mheshimiwa Profesa Tibaijuka tukiyaweka yatatturudisha kule nyuma na huyu *contractor* mwenyewe amekuwa *defined* kwenye hii sheria yenyewe. Kwa hiyo, ukiisoma ile tafsiri ya *contractor* tutarudi kule nyuma. Kwa hiyo, naomba kushauri Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja ya Serikali kama ilivyo ikubaliwe. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni hili analopendekeza kuongeza maneno '*timely delivery*', sisi tumeweka lile neno '*delivery*' kama *generic* lakini msingi mkubwa unaupata kwenye Ibara ya 3 ya huu Muswada ambayo inaweka kanuni za msingi za manunuzi. Moja ni *economy and efficiency,* wewe utapimwa pale lakini sisi tunazungumzia tu *delivery* tu pale, tutaangalia huyu bwana amefanya *so much timely* au kuna *lagging behind.* Hoja anayoisema Mheshimwa Profesa kuhusu kuongeza neno '*timely delivery*' tayari imeshakuwa *captured* kwenye *principle* ya msingi ya sheria hii tunapozungumza juu ya *efficiency.* Kwa hiyo, hili na lenyewe naomba Waheshimiwa Wabunge wakubali hoja ya Serikali kwamba Ibara hii ibaki jinsi ilivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nakilenga ni tusijibane, *contractor* anatoa *service,* unaweza kuwa na kitu fulani unataka kifanywe na mkandarasi kama *service provider.* Kwa hiyo, nataka kusema kwamba siyo tofauti kubwa lakini katika utekelezaji wa sheria ina maana yake na ndiyo hapo tunapokwama kwa mfano kuweka neno pale '*or contractor*' chini ya ile *side note* inaleta maana kubwa. Labda basi niseme kama Mwanasheria anaifafanua kama alivyofafanua angalau akubali kwamba kuna *value added* kwa kuweka neno '*or contractor*' katika *side note* hata bila kufafanua sana lakini neno '*contractor*' unapoliacha unaacha pia mambo mengi katika utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna Tibaijuka, naomba utoe hoja muda wetu unaenda sana ili niwahoji Wabunge.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja kwamba neno '*contractor*' liwekwe kwenye *side note* ya Ibara ya 24, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji maelezo tu kidogo, maneno unayokuwa umetumia kwenye *side note* kama ndani hayapo inakuwa siyo sahihi kwa sababu *side note* inakupa muhtasari wa yaliyoko ndani. Hoja yako kidogo inanipa taabu Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka kwamba tuiweke huku kwenye *side note* hata kama huku ndani haitakubalika sasa itakuwa inafanya nini humu mwanzoni? Inabidi nikupe nafasi ili Wabunge waelewe ni kitu gani wanapigia kura.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mwanasheria Mkuu anavyofafanua lakini nadhani na yeye amenisikia napotaka kwenda. Kama Sheria ya *Procurement* haijafafanua *contractor* ni mtu gani na anatoa *service* za namna gani, hapo kidogo nashindwa kuelewa. Mimi hoja yangu ni kwamba *contractor* ni mtu ambaye anatoa *special service*. Kwa hiyo, kama inaleta ukakasi badala ya kuipigia kura hoja hii naweza nikaiondoa kwa sababu ilikuwa inalenga kuboresha sheria hii basi angalau nisikie kwenye kanuni za Waziri kwamba hiki kitu kitafafanuliwa kwa sababu sheria nyingi zinakwama kwa sababu zinakuwa hazitekelezeki *operationally*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka nikushukuru kwa kuiondoa hiyo hoja lakini ninayo hapa ile sheria mahsusi na inayo hayo maneno uliyokuwa unasema. Kwa hiyo, ile Sheria Mama yenyewe ambayo tunaibadilisha imefafanua suala hilo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi katika hii Ibara ya 24 mbele ya 65A(1), baada ya neno '*provider',* napendekeza iongezwe *proviso* ya maneno yanayoweka ulinzi ili kusudi kama taifa tunaponunua moja kwa moja kutoka kwa mzalishaji tusipate hasara baadaye. Maneno hayo nayopendekeza kuingia yanasema:-

"*Provided that procuring entity shall make sure that there is early supplier involvement in the required product development in accordance to technical specifications to enhance efficient end results of the procurement process*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaweka ulinzi ili kusudi tusipate hasara na tusipate matatizo ya kuona vitu ambavyo vimetengenezwa siyo ambavyo tulivyoviagiza. Kwa hiyo, inatakiwa yule *manufacturer* awe *involved from the early process* kabla hajatengeneza hivyo vitu tunavyovinunua ili kusudi tununue kitu ambacho kweli tulikitaka. Hii ilileta matatizo mengi katika nchi nyingi na hata hapa Tanzania baadhi ya taasisi zimepata matatizo kama haya. Kwa hiyo, kuweka hii *proviso* inaweka ulinzi ili kusudi tusipate hasara kama taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu pendekezo langu la pili hapo hapo nilikuwa napendekeza iongezwe *para* (c), hiyo nimeifuta kwa sababu nimeona hapo hai-*fit* vizuri. Nilikuwa napendekeza yaongezwe yale maneno yaliyopo pale kwenye *para* (c), hiyo nimeifuta lakini *logic* yake Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Waziri…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda kama umeifuta usiitolee maelezo, malizia tu ile hoja yako ambayo bado ipo mezani.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ya kwanza ndiyo napendekeza iongezwe hiyo *proviso*. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) naongeza nusu saa. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ikiwa ukitaka kununua tu kitu unaanza kumtambua *manufacturer* na *manufacturer* wako wengi sasa unamchukua yupi, si kuna *specifications?* Kwa hiyo, naomba kushauri masuala haya ya kumhusisha huyu *manufacturer from the very beginning* siyo sahihi ni kama *single sourcing* hivi na hii itatuletea shida, hii ndiyo italeta ufisadi namba moja hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kakunda alikuwa na mapendekezo mazuri, nia yake ni nzuri lakini kwa jinsi alivyoyaleta itatupa shida sana. Sisi humu ndani tumeshakubaliana tunataka kununua magari ya aina hii, watengenezaji wa magari wako wa aina fulani, tukishafanya maamuzi tunaenda tu moja kwa moja kule, kama ni *Toyota* au *Nissan Patrol whatever,* tunanunua lakini ukianza kumhusisha moja kwa moja tutapata shida. Naomba kushauri Waheshimiwa Wabunge hii hoja ya Mheshimiwa Kakunda tuiache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo ile Ibara ya 3 kwenye mapendekezo haya imeweka hiyo misingi, kwa hiyo utaua hata hiyo misingi ya *competition* sasa unamchukua nani? Hapa kutakuwa na *a lot of lobbying,* nipe mimi bwana. Waheshimiwa Wabunge, naomba kushauri mapendekezo ya

Mheshimiwa Kakunda hata kama ni mazuri lakini labda asubiri wakati mwingine. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda naona umekubaliana. *(Kicheko)*

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tu kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema haya mapendekezo ni mazuri kwa hiyo ataya-*consider* kwenye maeneo mengine. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo pia kuna marekebisho ya Serikali. Sasa nitawahoji Ibara hii kwa ujumla wake.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunarudi Ibara ya 2.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, marekebisho ya Kamati yalishaletwa pale mwanzo na kwa kuwa muda wetu unakwenda sana na pia kwa sababu Ibara ya 24 marekebisho ya Kamati yamekubalika, naona Mheshimiwa Chenge amesimama, nimalize maelezo kidogo Mheshimiwa Chenge. Kwa kuwa ile Ibara ya 24 ambayo itataka lazima maneno yaliyokuwa yamependekezwa na Kamati yatafsiriwe na Kamati ilileta tafsiri, tukaongeza maneno *health* yaani '*life-saving health commodities* na tulishaisoma hii na Mheshimiwa Hawa Ghasia alikuwa ameshatoa hoja. Kama Mheshimiwa Chenge hakusimama nilitaka tuhojiane baada ya hayo maelezo lakini kama anayo ya ziada basi Mheshimiwa Chenge endelea.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ili Kamati yako na Wajumbe twende pamoja kwenye tafsiri inayopendekezwa, tumeingiza neno '*life-saving health commodities*'.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kutambua kwamba Waziri mwenye dhamana na sheria hii ni Waziri wa Fedha sisi tunapendekeza isomeke hivi, tufanye *modification* ndogo tu ambayo haibadilishi maana, mstari wa nne kutoka juu, isomeke:-

"*… and childhood as the same may be modified from time to time by the Minister in consultation with the Minister responsible for health by order published in the Gazette*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshauri sana kuhusu suala hili, tuwaachie Wabunge wapige kura.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maana ya neno *lifesaving health commodities* Kamati imeleta marekebisho kidogo katika yale mapendekezo yao waliyokuwa wameyatoa mwanzo na wanapendekeza mstari wa pili kutoka mwisho yaongezeke maneno *from time to time by the Minister* yaongezeke maneno *in consultation with the Minister responsible for health,* ili waweze kuwasiliana Waziri wa Fedha na Mipango lakini pia na Waziri wa Afya, ndiyo mapendekezo yaliyoletwa.

Lakini kama nilivyotoa maelezo tangu mwanzo, maana ya haya maneno hatuwezi kuyakataa hapa kwa sababu tumeshakikubali kile kifungu kule ambacho kitatutaka lazima tutoe tafsiri. Kwa sababu hiyo, nitawahoji kwa sababu Katibu ameshakitaja kifungu namba mbili.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 3

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hapa nina pendekezo langu kama nilivyosema na lenyewe linalenga kuboresha mambo ambayo kwa kweli yamekaa vizuri, lakini kuboresha ndiyo mantiki ya kikao hiki. Napendekeza neno *competition* tuweke neno *fair competition*. Nasema hivi kwa sababu hii *procurement* pia ni sehemu ya biashara ya *International trade*. Sasa katika mikataba yetu mingi unakuta kwamba kuna mahali pengine tunalazimika kwa taratibu zilizopo kuingia kwenye *competition,* kwa hiyo, watu wetu wanapo-*compete concept* ya *fair competition* inakubalika Kimataifa kwamba iwepo. Kwa hiyo, nimependekeza kwamba neno *fair competition* liwekwe kwenye clause ya 3(*2)* kwamba neno *fair* liwekwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu la pili, kwa sababu misingi mizuri ya mabadiliko haya ya sharia, tayari sheria kwa kweli inajaribu kuwapa wazawa nafasi katika *procurement*. *Government Procurement* au *Public Procurement* ni kitu kikubwa sana kwa ngazi ya Kimataifa. Kwenye *World Trade Organization* hiki kitu hakuna *agreement,* kila nchi ina haki ya kulinda watu wake, kulinda biashara zake, kulinda *suppliers* wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimeona kwamba naweka maneno ya kuboresha hii sharia ili mtu yeyote anayekuja kwenye nchi yetu ajue kwamba, tunalinda wazawa kwanza. *World Trade Organization* (*WTO*) haina *international agreement on Government procurement.* Kwa hiyo, nimeleta maneno hapo, ambayo yanalenga hilo, yanaboresha sharia, hayapingi kitu chochote ambacho Serikali imeshaweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napendekeza kwamba huo msingi wa kuwalinda wazawa katika kutoa *procurement*, nimeongeza *sub-clause (2)* ilindwe kusudi kwamba watu wetu wasiwe wanabanwa tu na watu wa Kimataifa bila sababu kwa sababu ya *lack of fair competition,* ndiyo mantiki ya mapendekezo yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua umuhimu wa mchango wa Profesa Tibaijuka, lakini wasiwasi wake umezingatiwa sana kwenye sheria hii. Moja, hicho anachokisema, akisoma kifungu kidogo cha (3) cha hiyo Ibara ya 3 ambayo inatengeneza ibara mpya ya 4A inazungumza (1) "*procuring entities shall in the execution of their duties undertake to achieve the highest standards of equity taking into account*:-

*(a) Equality opportunity to all tenderers;*
*(b) Fairness of treatment to all parties; and*
*(c) The need to obtain the best value for money in terms of price, quality and delivery, having regards to prescribed specification and criteria*".

Hiyo ya kwanza, kwa hiyo, hapa kinachozungumzwa kwenye hii ya 3(2) ni msingi tu ile *competition, whether it is fair au not, but* tunaweka tu msingi wa *competition.* Sasa lakini kuna masharti yanasema hii *competition* lazima iwe *fair,* ndiyo msingi wa *sub-section (3)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hayo mengine anayosema, moja la msingi na Mheshimiwa Waziri amesema na kwenye Kamati wametushauri vizuri sana na Serikali ilizingatia. Moja ya malengo makubwa ya Muswada huu ilikuwa ni kuhakikisha kwamba, hawa Watanzania wazawa wanapata na wao fursa ya kushiriki kwenye hivi vitu. Utaona kuna pendekezo lingine la Serikali, *further further schedule of amendment*, ambayo tume-*capture* hata mapendekezo ya Kamati. Kwa mfano, kwenye kifungu cha 55, vifungu vyote vya 55A *up-to D*, tumeongeza *E* ambayo makampuni ambayo yatakuwa *considered* pale ni yale ambayo yanamilikiwa na Watanzania kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hao ndiyo wata-*qualify* ku-*partner* na *foreign company* kwenye *consultant services*. Pia humu ndani unaona kuna *preferential treatment,* kuna *local whatever,* kwa hiyo, hayo yote yamezingatiwa kwenye sheria iliyokuwepo, lakini hata kwenye hii yameboreshwa zaidi. Kwa hiyo, naomba kushauri mapendekezo ya Serikali kama yalivyo yabakie.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**MHE. HAWA A. GHASIA- MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba uniongoze kwa sababu katika ile *clause (2),* Kamati ya Bajeti ilikuwa na *amendment* maeneo mawili, tulileta *further schedule amendment*. Sasa wakati Katibu anatuongoza hapa, anaona tume-*deal* na moja, halafu tumehamia kifungu cha tatu (3), ile *amendment* nyingine tuliyoileta naona imerukwa, sasa naomba maelekezo yako.

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ni mapendekezo gani hayo, yanahusu kitu gani?

**MHE. HAWA A. GHASIA- MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yalikuwa yanahusu *definition* ya *force account* hasa kwenye *Local Government* ambapo wakati mwingine kunakuwa na kazi ambazo ni ndogo sana na ukiangalia mchakato wa zabuni unatumia gharama kubwa sana kuliko ambavyo wangetumia wataalam wao walioko pale pamoja na pesa kidogo. Kwa mfano, unaweza ukakuta labda kuna darasa au palepale ofisini labda choo tu kimevunjika na unahitaji tu kufanya marekebisho ambayo hayazidi wakati mwingine hata milioni au laki tatu hayafiki na kuna *technicians* pale na wenyewe wangeweza kuifanya kwa gharama nafuu, lakini inasubiri mpaka utaratibu wa *tender*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu zamani ulikuwepo, lakini ukaondoshwa. Sasa baada ya kujadiliana na Serikali, tulitaka hiki kipengele cha *force account* kirudi tena kwenye sheria na tulileta *further schedule of amendment*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kanuni tulizonazo mikono yangu imefungwa kwa sababu kifungu cha pili nilishahoji na Bunge limeshaamua. Kwa hiyo, niisihi Kamati pamoja na Serikali kwa umuhimu wa mapendekezo ambayo mlishajadili kwenye Kamati ya Bajeti, wakati ujao mtuletee hayo marekebisho ili tuweze kuyafanya vizuri. Kwa sababu kwa sasa siwezi kukirudia hicho kifungu kwa sababu Bunge limeshatoa uamuzi. Kwa hiyo, Kamati nadhani kidogo pengine na sisi mezani tulipitiwa, lakini pia na Kamati haikusimama kwa wakati, japokuwa wangetarajia kuitwa, lakini kwa sababu tumeshatoa maamuzi, hatuwezi kurudi nyuma tena.

Kwa hiyo tuendelee Waheshimiwa. Mheshimiwa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hapa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye yeye ni mtafsiri wa sharia, maana yake kuna kuandika sheria na kuna kuzitafsiri. Sisi kama *lay people,* mimi kama mtu ambaye nawakilisha wananchi hapa, naona kwamba ingefaa, hivi vifungu vyake vihakikishe kwamba hakuna ukakasi kuhusu *local,* yaani kwamba tunatumia *public procurement* pia kuwasaidia wananchi wetu. Sheria hii huko mbele ana vipengele hivi, lakini naona hapa anapo-*define principles, clarity* isingem-*cost* kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama nilivyosema hapa hakuna badiliko, mimi natafuta *clarity* kusudi *principles* ziwe *clear*. Kwa hiyo, naweza kusema kwamba, kama hilo linaeleweka kwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, katika *interpretation* nitaondoa hoja mezani, lakini *clarity* kwamba watu wetu lazima tutumie sheria hii kuwawezesha vijana kupata ajira, ni muhimu sana. *Public procurement* dunia nzima inatumika kuwawezesha wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha kama imeeleweka naondoa hoja mezani. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka kwa sababu umesema kama imeeleweka, nadhani Wabunge tumeelewa ama hatujaelewa? Nadhani tumeelewa, kwa hiyo, Wabunge wanasema wameelewa kwa hiyo asante. Tunaendelea sasa nawahoji, Katibu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya marekebisho yanahusu Idara ya Sera ya Ununuzi na ufuatiliaji na tathmini ni jukumu la msingi la Idara ya Sera. Idara zote za Sera katika Serikali kwenye kazi zao za msingi ni pamoja na huu ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa sera ili kusudi waweze kushauri watunga sera. Sasa kuondoa hizi kazi za ufuatiliaji na tathmini kwenye vipengele ambavyo vimependekezwa na Serikali ni kuikata miguu hii Idara ya Sera isiweze kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa sera ambao ni jukumu lao la msingi. Kwa hiyo, naomba sana pamoja na kwamba *PPRA* itafanya *procurement audit,* lakini hii Idara ya Sera iendelee kutimiza majukumu yake ya ufuatiliaji na tathmini ili kuwashauri watunga sera. Hayo ndiyo mapendekezo yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba arudie tena kufafanua.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kazi za ufuatiliaji na tathmini ni miongoni mwa majukumu ya msingi ya idara yoyote ya sera, sasa hapa tunazungumzia Idara ya Sera ya Ununuzi. Kwa hiyo, kazi ya kufuatilia na kutathimini utekelezaji pamoja na *systems* za ununuzi ni jukumu la msingi la hii Idara ya Sera ya Ununuzi. Sasa kuiondoa hii kazi kwenye hii idara ni sawasawa na kuikata miguu isiweze kutimiza majukumu yake ya msingi. Kwa hiyo, naomba hii kazi isiondolewe kwenye hii idara, iendelee kuwepo kama ilivyokuwa kwenye sheria ya hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya kuondolewa hapa kwenye *sub-section (2)* yanaondolewa kwa sababu ni *repetition,* yapo kwenye *subsection* (1), ndiyo msingi wa kuondoa hapo hiki kifungu cha sheria yenyewe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sheria mama hiki kifungu kinazungumza hivi, maana lazima turejee kidogo. Kinasema hivi, pale kipengele 6(2)(b*) "monitor, evaluate and review public procurement systems na 6(2)(i) monitor and evaluate performance of public procurement institutions*. Huo ndiyo msingi ambao nasema kwamba, hakuna madhara yoyote haya maneno yakiendelea kuwepo hapo, kwa sababu yanaipa nguvu Idara ya Sera kuhusu kufanya kazi za ufuatiliaji na tathmini za utekelezaji wa sera za ununuzi za nchi. Ndiyo maana nikasema hakuna *harm* yoyote maneno haya yakibakia pale, hivyo yaendelee kuwepo kama yalivyo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Kakunda na kwa kufuatilia kifungu hiki kama Serikali, tunaamini ni sahihi anachokisema, kwa hiyo tuna-*maintain* kama alivyopendekeza. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimeshafanyiwa kazi na Serikali, nashukuru sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**LAWRENCE MAKIGI-KATIBU MEZANI:** Kifungu cha 10 kina marekebisho ya Kamati.

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nisahihishe, tuna marekebisho kifungu cha 20 na siyo cha 10. Kwa hiyo, hapo hatuna marekebisho.

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesha-*take care*. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 12

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya marekebisho ya Serikali yalikuwa yanafuta 35(3), (4) na (5), ambayo inataka *approval* ya bajeti *authority* na wakati mwingine ilikuwa inataka *approval* ya *Paymaster General.* Sasa napendekeza, vipengele vyote vile (3), (4) na (5), vibaki kama vilivyo, isipokuwa tu, maneno *Paymaster General or* hayo ndiyo yafutwe. Kwa sababu *Paymaster General* ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha yuko mbali sana na hizi Taasisi, anaweza asipatikane kwa muda muafaka, lakini *Budget Authority* kwenye Wizara ni *Management* ambayo ipo chini ya Katibu Mkuu, anaweza akaita kama kuna jambo la dharura. Hata sasa hivi anaweza akasema nataka saa nane Menejimenti, anashauriana nao, halafu wana-*prove process* inaendelea.

Kwa hiyo, nafikiri kwamba hivi vipengele 3,4,5 havina madhara isipokuwa madhara yalikuwepo tu pale kwenye *Paymaster General or.* Kwa hiyo, maneno ya *Paymaster General or* yakiondoka inakuwa vipengele vyote vile havina madhara ya kuchelewesha chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili lilitushughulisha sana sisi Serikalini na ndiyo tukaleta mapendekezo haya na kwenye Kamati nako tulizungumza na Kamati tukaelewana nao. Moja walituuliza swali, sasa huyu bajeti *approving authority* mbona hamjamfafanua, yaani hamjampa tafasiri.

Kwa hiyo, matokeo yake ili kuleta *clarity* tulichokifanya, sisi tumefanya mabadiliko, ukiangalia jedwali letu lingine lile la ziada tumeondoa hiyo *budget approving authority* ili kukubaliana na ushauri mzuri wa Kamati. Baada ya hapo tunafikiri kwamba mapendekezo ya Serikali jinsi yalivyo, yabakie tu pale kwamba wapate tu kuendelea na hatua baada ya kuwa wameshauriana na *Paymaster General*, jinsi ambavyo Mheshimiwa anapendekeza na jinsi ambavyo pia kwa sheria ya sasa ilivyo, hiyo inatuletea shida.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ili Wabunge wajue wanachoamua ni kitu gani, mapendekezo ya Mheshimiwa Kakunda yanakubaliwa au yanakataliwa na Serikali? Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kama Serikali imenielewa kuhusu pendekezo langu la kufuta *Paymaster General* or, kwa sababu huyu yuko mbali, lakini *budget authority* kwa Wizara ni menejimenti

timu. Sasa kama Katibu Mkuu anaweza akaitisha, kwa mfano, sasa hivi ni saa saba anaweza akasema saa tisa tukutane. Menejimenti hakuna mtu wa kukataa, watakutana pale, watashauriana na *process* zitaendelea kama kawaida. Kwa hiyo, hakuna *delay* zozote ambazo zinaweza zikasababishwa eti kwa kushauriana na *budget authority*. Kwa hiyo, nashukuru kama imeeleweka hivyo na kama wataviacha hivyo vipengele. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda naomba utoe hoja, Serikali imekataa mapendekezo yako, kwa hiyo, toa hoja Bunge lihojiwe, liamue.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu cha 12, nitawahoji kuhusu mapendekezo ya Mheshimiwa Kakunda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 13

*(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika kifungu hiki, mapendekezo yangu yanalenga kuyaboresha yale ambayo tayari ni ya Serikali, kwa kuzungumza bila kumung'unya maneno kwamba, katika mikataba ya *consultancy assignments*, wazabuni wanaotoka nje ya nchi ni lazima wawe na Watanzania. Miaka 55 baada ya uhuru, hakuna fani ambayo

Watanzania hawana ujuzi nayo. Kwa hiyo, nalenga kabisa hapa na pendekezo la Serikali lipo, lakini wanasheria wanaita *constructive ambiguity*, sasa mimi nimekuja *directly* na kupendekeza kwamba, lugha itamke bayana kwamba watafute wazawa, wataalam wetu waingie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana hawa watu wa nje bila kuwabana na sheria wataendelea kutuchezea, wanaweza hata waka-*collude* wakaitana wao, ukakuta wazawa hawamo. Kwa hiyo, mapendekezo yangu yanalenga tu kuboresha yale mazuri ambayo Serikali imeyaleta na sasa hapo Mwanasheria wa Serikali yeye ndiye anajua *interpretation,* mimi nimeleta lugha ya mtaani, ya kawaida, maana sheria ni za sisi watu wa mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ndilo lengo langu kwamba, wazawa wapewe nafasi, hilo la kwanza. Kwa hiyo, katika sasa kutathimini zile tenda za hao wazabuni, ma-*consultancy,* wale watakaokuwa wameweka wazawa wengi, watapata *point* na hapo sheria imeandikwa vizuri, imejaribu kufafanua katika kipengele cha tatu, kwamba wataweka *relative weight.* Kwa hiyo, mapendekezo yangu yanalenga kuboresha na hao watu wasiendelee kutuchezea watoto wetu wapate maahali pa kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema vijana wajiarijiri, watajiajiri namna gani wakati mwingine sheria zetu haziwawezeshi kuweza kufanya mambo hayo? Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna Tibaijuka, hapo unapopendekeza hayo maneno yaongezwe wakati Serikali inajipanga kuchagua mtu wa kujibu, mimi nayaona maneno yaliyosemwa hapa, *Foreign friends Procuring entity shall ensure that inclusion of local experts and local firms in their assignments is achieved through apportioning proper weight in*, wanaendelea. Maneno haya ndiyo wewe uliyopendekeza hapa, sina uhakika unataka yawe *defined* ama vipi, lakini acha Serikali ijibu yenyewe. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama ambavyo umeshauri, matumizi ya neno lililotumika pale ni *shall* na imeendelea kutoa na Serikali pia baada ya ushauri mzuri wa Kamati ilikubali, ikakifanyia mabadiliko hiki kifungu *at least*. Hata hivyo, tumeenda zaidi, tumefanya mabadiliko zaidi, Waheshimiwa Wabunge mmegawiwa hili jedwali la marekebisho la ziada asubuhi hii, kwamba kwenye kupata zile kazi, acha tu kule kushirikishwa, kwenye *competition* ile ya tenda. Kwenye ile kupata kazi, *partnering* ile iwe ni kati ya huyo *foreign company* halafu na Kampuni ya kizawa ambayo inamilikiwa 100% na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wasiwasi wa Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, unakuwa umeshapewa jibu. Kwa hiyo, naomba kushauri kwamba mapendekezo haya yalivyo ya Serikali kama ilivyofanya marekebisho kwenye majedwali yote mawili ya Serikali yazingatiwe na wasiwasi wa Mheshimiwa Tibaijuka tayari umeshapatiwa jibu kwenye haya marekebisho ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sheria ilivyokaa sasa hivi, hiki kipengele alivyofafanua Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, anasema *where a consultancy assignment are carried out by foreign firms Procuring entities shall ensure that inclusion of local expert and local firms in their assignment is achieved through apportioning proper weight.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napendekeza kwamba, maneno hayo kusudi kuondoa i*nterpretation* za wajanja ambao wanakwepa vijana wetu, wanakosa kufanya kazi ambazo wangeweza kufanya na tayari wameshasoma, tumewasomesha, tumehangaika inasema, *Foreign firms competing to be awarded non-emergency consultancy assignments whether by tender or any other means recognized in this Act shall be required to include local experts and firms in their teams.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi ni *semantics,* mantiki ni hiyo hiyo, lakini naamini kwamba pendekezo langu, ndilo linakwenda sasa kuweka sheria inasema *categorically* kwamba sasa Tanzania vijana wetu wanalindwa, *foreign firms* haziwezi ku-*collude against us*. Hivi vitu navijua, watu hawa kama lugha haiko *clear,* wanaweza bado wakatuzunguka, lakini kama sheria yetu itakuwa hivyo na inasaidia watendaji wa Serikali ambao watakuwa na presha za ku-*deal* na haya mambo *in a day to day basis*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, najua Mwanasheria amepata mapendekezo yangu sasa hivi, ningeyawasilisha tangu jana, kidogo labda angekuwa amepata muda wa kuona kwamba *we are like minded* katika hapa, ila tunavyo-*clarify* mambo. Kwa hiyo, nifikiria kwamba labda upande wa Serikali waangalie pendekezo langu, halipingi wala halitofautiani na la kwao, lakini linakwenda kuondoa *ambiguity, ambiguity* hii ndiyo inafanya watu wanatuchezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko pale, kama Serikali bado hawajanielewa, itanilazimisha kusema natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Naomba utoe hoja kabisa Mheshimiwa tulihoji Bunge.

**MHE. PROF. ANNA TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda wameshanielewa naona kama wanatazamana huko. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wetu siyo rafiki sana, kwa hiyo toa hoja.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, naomba kutoa hoja kwamba sheria iwe *clear* kwamba inalinda wazawa…

**MWENYEKITI:** Toa maelezo Mheshimiwa Tibaijika na wewe unazijua kanuni vizuri, umeshatoa hoja usiendelee na maelezo.

Waheshimiwa sasa nitawahoji kuhusu mapendekezo ya Mheshimiwa Tibaijuka katika kifungu cha 18.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya hoja ya Mheshimiwa Tibaijuka kushinda, lakini tuelewe tu jambo moja kwamba, hiki kifungu itabidi, sijui Serikali mtupe maelezo, sidhani kama kitaweza kufanya kazi kwa sababu kitakuwa na mambo yanajirudia rudia. Mtatupa hayo maelezo baadaye, kwa sababu wao wameshayakubali, ya Mheshimiwa Kakunda tayari hapa au bado?

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Waheshimiwa Wabunge, mnajua msitunge sheria kwa hasira, mtapata hasira, hiki kifungu mlichokitengeneza hivi hakitatekelezeka. Hakiwezi kutekelezeka kwa sababu sisi tumekifafanua sana na Kamati imeshauri na tumefafanua hapa, tumefanya marekebisho katika jedwali lile na tumeleta tena asubuhi.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila utaratibu kuonesha kutokubaliana na Mzungumzaji)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Sisi tunakubali ni Bunge limetunga, lakini utekelezaji wa hii itakuwa shida, kwa sababu ilivyo Mheshimiwa Profesa alikuwa anataka *clarity*. *Clarity* ipo, tungeni hivyo, lakini utekelezaji wake…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Chenge alikuwa amesimama. *(Kicheko)*

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye Kamati, kwenye eneo hili tuliafikiana na Serikali. Hoja ya Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka ni nzuri tu, lakini kwa maelezo ya Serikali, nasema siyo kwamba *AG* amekasirika, hapana, nadhani ndivyo alivyo, maelezo yake, maana ukisoma ibara ya 18(2) unaipata kabisa hiyo ambayo Mheshimiwa Profesa anaitaka, kwa sababu uko katika hatua ya kufanya *evaluation.* Maana lazima wanakwenda kwa tenda, sasa unatakiwa wewe ili upate zile *score* zitakazokuwezesha wewe kwenda mbele, uje na Watanzania hawa upatane nao, upende usipende lazima wawepo. Sasa ukikubali kama Bunge lilivyohojiwa na Kamati ilivyokubaliana kukubali, uandikaji wake hapa utakuwa ni tabu kweli kwa sababu hayo mapendekezo yaliyosemwa na Mheshimiwa yaingie wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nasema, Kamati yako tuone busara kwamba hoja ya Profesa inabaki pale pale, lakini inakuwa *taken care of* kuanzia kwenye kifungu kidogo cha (2) pale, (a) inakueleza vizuri tu na (b). Kwa hiyo, nasema hatupotezi chochote maana tunatunga sheria ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Kamati, pamoja na kwamba umewahoji, tutambue wajibu wetu, taarifa ya Kamati itakapopelekwa Bungeni, lazima ioneshe kwamba tunatunga sheria kwa umakini kwa niaba ya Taifa hili, kwa leo na kesho na keshokutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge tunakushukuru kwa ufafanuzi huo, katika kifungu hiki pia tunayo marekebisho ya Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ambayo napendekeza mimi kwenye *clause* 18 ni…

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Kakunda, naomba ukae kidogo! Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha, hata ule ambao nilikuwa nimeongeza nusa saa, lakini kwa mujibu wa kanuni ya 28(6) sitasitisha hii shughuli mpaka iwe imeakamilika. Kwa hiyo, tunaendelea, Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nilikuwa nataka ku-*define* hii *local participation* kama ambavyo inakuwa *scored* kwenye *evaluation report* ya *Evaluation Committee* kwamba, kumekuwa na udanganyifu mwingi sana, mtu anaweza akaorodhesha *staff* akasema kutakuwa na Profesa Anna Tibaijuka, kutakuwa na Profesa Wangwe kutakuwa na Mheshimiwa Chenge katika *list* ya *staff*. Halafu unapokuja *field* anakwambia, hawa hawakupatikana sasa bwana tutakuwa na Mr. Mjema, Mr. Kakunda *and so and so,* yaani ni kwamba unakuwa ni udanyanyifu. Kwa hiyo, napendekeza

mbele ya 5A(2) kuna (a) (b) pale, iwepo (c) ambayo inasema*, the scored local participation must be visible throughout the project execution period, demonstrated by daily signing on the field attendance book, failure of which may cause termination* ili kuondoa huo uongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebosho mengine madogo ni kuongeza maneno kwenye 55(c) kwa ajili ya ku-*prescribe compliance to agreed standards.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yalikuwa ni hayo tu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Serikali. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sikapunda anavyopendekeza unajua kuna mchanganyiko hapa wa vitu ambavyo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Kakunda, samahani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yenyewe ya kuwataka watu hawa eti *local participation* itatokea kwa sababu mtu atakuwa anasaini *attendance register* kwa kuweka sahihi, *that is not the spirit of the law*. *Spirit* ni *participation*, yaani wao wanayo fursa ya kupewa hizo kazi, washiriki kufanya kazi sio mahudhurio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kushauri kwamba, mapendekezo haya ya Serikali kama yalivyo kwenye majedwali yake yale mawili na kama ambavyo tulishauriwa na Kamati ya Bajeti tukakubali, yanatosha kabisa ku-*guarantee participation* ya Watanzania, ushiriki wa Watanzania humu. Kwa hiyo, naomba kumshauri Mheshimiwa Kakunda, pamoja na nia yake njema ya kutaka kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata ushiriki kwenye kazi hizi, lakini naomba kushauri tu kwamba, Serikali imeridhia mapendekezo ya Wabunge na imerekebisha na marekebisho kwa jinsi yalivyo yanalinda maslahi ya Watanzania kwenye shughuli hizi za tenda kwenye masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kupendekeza kwamba, mapendekezo ya Serikali na marekebisho yake yakubaliwe.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hilo la kwanza naweza nikaelewa msimamo wa Serikali, lakini nina uzoefu kwamba, aliwahi kupewa kazi *local firm* kwenye bonde la Ziwa Rukwa, badala ya kuendelea na wale ambao alikuwa amewaorodhesha kwenye maombi yake ambao walikuwa ni Watanzania, hatimaye kwenye *field* akaajiri Waganda. Kwa hiyo, hiyo ni *experience* tu ambayo naipa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hata kwenye hili la pili 55(c) kuongeza yale maneno *that prescribe compliance to agreed standards* kwa ajili ya kuweka viwango ambavyo vimekubaliwa, nalo Serikali inakataa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshauri hapa kwamba na hata anachokisema kimezingatiwa kwenye yale majedwali. Huku mbele tutakapofika kwenye ile (j) kwenye ile ibara ya 28, tumefanya mabadiliko mapya, baada ya kupata ushauri mzuri kutoka kwenye Kamati na adhabu zipo nyingi sana. Kwa hiyo, naomba kumwondoa wasiwasi tu Mheshimiwa Kakunda kwamba, hoja yake imezingatiwa na haya yako *taken care of* kwenye jedwali la Serikali lile la kwanza la marekebisho, lina haya yote, kwenye ile *item* (j).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda umeelewa ama unataka kutoa hoja yako.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa mazingatio ya Serikali, ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 19

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imezingatia, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwenye clause 20 pale, tu-*delete* ile (b) na tuandike upya (c), (d) na (e) na isomeke kama ni (b), (c) na (d).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nafanya hivyo? Katika sheria ya zamani ilikuwa inasema, kabla ya Halmashauri kwa maana *Accounting Officer* haja-*award* ile tenda kwa mzabuni aliyeshinda ni lazima afikishe katika Baraza la Madiwani au Kamati ya Fedha, lakini sasa hivi Serikali inakusudia kuondoa kipengele hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupeleka kwenye Kamati ya Fedha ya Halmashauri, ilikuwa inasaidia sana kwanza uwazi na uwajibikaji, lakini pia lazima Serikali ifahamu kwamba, uendeshaji wa Serikali za Mitaa, ni uendeshaji ambao unapitia katika vikao ni *Committee Government* na siyo kwamba mtu mmoja anaweza akakaa akafanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimesoma taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2014/2015, katika makosa yaliyoainishwa mle zaidi ya asilimia 99 ni ya watendaji hasa katika upande wa tathimini na pia *Tender Board* zinavyokiuka maagizo ya Serikali na vile vile kuna masuala mazima ya kuwapa *tender* watu ambao hawastahili, hata wale ambao wame-*bid* chini wamekuwa wakifichiwa zile nanihi zao na kumekuwa na udhaifu katika usimamizi wa mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makosa yaliyohusiana na Kamati ya Fedha katika ataarifa ya Mkaguzi na Hesabu za Serikali ya mwaka wa 2014 ni kosa moja tu. Kwa kweli nawashauri na nawahamasisha Wabunge wenzangu na tuiombe Serikali kifungu kilichokuwepo kibaki vile vile; kwa sababu kinasaidia sana katika kuwajibisha watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo sisi wenyewe Wabunge ni Wajumbe katika Baraza lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ndilo pendekezo langu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ngoja niulize kwanza, Wajumbe mnayo hayo mapendekezo ya Kamati? Hapa mezani...

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ile *schedule* yangu *of amendment,* ile ambayo niliiandika *close* 10, ulivyoniita nikasema kwamba nasahihisha, siyo *close* 10, badala yake ni *close* 20, ndiyo hiyo ambayo naizungumzia. Kwa hiyo, unayo ile ile ambayo tumeshughulikia *life saving health commodities,* ile (b) badala ya 10 ni 20, kwa hiyo,unayo.

**MWENYEKITI:** Nimeelewa. Waheshimiwa Wabunge nadhani Mheshimiwa Chenge alitoa maelezo marefu sana tukamwelewa. Nimeuliza kwa sababu hata sisi hapa mezani tulikuwa tunatafuta, lakini kuna Wabunge wawili, watatu wamejibu ndiyo wanayo, yaani kwa maana kwamba hata kama hawana haijalishi. Sidhani kama ni kitu kizuri Waheshimiwa Wabunge, tusifike huko, tufanye kazi yetu kwa namna tunavyofanya siku zote; kwa pamoja tu litakwisha hata hili. Kwa hiyo, tusichukulie hasira kwa kuona kwamba Kamati imesema kwa hivyo hata kama hatuna, sawa, hapana. Kama hatuna ni kwamba hatuna, lazima tutafute, iwepo. Kwa sababu tunafanya kazi hii kama alivyosema Mheshimiwa Chenge, kwa ajili ya Taifa hili, kwa hiyo, hakuna haja ya kuonekana tuna haraka ama tuna hasira, hakuna hiyo sababu.

Kwa hiyo, tunaendelea, katika yale mapendekezo ya Kamati, lile linalosomeka kama B kubwa palipokuwa pameandikwa 10 paandikwe 20, ndiyo mapendekezo ya Kamati. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa Serikali kuleta mapendekezo haya kuondoa hiyo *Subsection* (4) ya *Section* 60, ilikuwa ni kuondoa urasimu, moja ya mapendekezo haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wameshauri ni kwamba, kunakuwa na mlolongo mrefu. Kwa hiyo tukasema kwa sababu yale masharti yao chini ya kifungu cha 31, inabaki; kwenye hili la kitaalam Kamati ile isishiriki, moja ikishiriki itakuwa inaendeleza huo mlolongo mrefu. Cha pili, hata ikishiriki hata haina ule utaalam wa kuweza ku-*scrutiny* yaliyopitishwa na wataalam wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha tatu, ukiwashirikisha wale utaondoa *accountability* kwa watendaji, kwa sababu sasa akifanya hata ufisadi anajitetea kwamba hii ilipitishwa na maamuzi ya Halmashauri. Kwa hiyo, tukadhani kwamba labda Halmashauri zibaki na *role* yake ya *super oversight* kwa maana ya Kanuni zinazotungwa na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya *Local Government Authorities,* lakini kwenye hili tuwaondoe, huo ndiyo ulikuwa msingi wetu, lakini mkisema libaki pale, *well and good,* pigeni kura libaki, *but* utekelezaji wake utawapa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake tutarudi kule ambako tulitaka kutoka, tuwe na *clear line of demarcation*; yaani kila mmoja abaki na jukumu lake. Hawa wanaoandika mikataba mibovu wawajibishwe na sasa hivi tumerekebisha, Mheshimiwa Waziri alirekebisha Kanuni tarehe 22 Aprili, hapa. Anawataka wale wote ambao wanafanya mikataba huko kwenye Halmashauri, wazingatie Sheria zile Sheria yenyewe hii na Sheria nyingine zinazohusika na mikataba ile na maadili yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wetu ni kwamba, mapendekezo yetu yalikuwa yamezingatia kwamba, hii tuiondoe kwa sababu

moja, mamlaka ya Halmashauri yanabaki na ile Kamati ya dhamana ya fedha inabaki chini ya kifungu cha 31 cha ile Sheria ili tutenganishe pia sasa majukumu ya watawala ambao ni watu wa Halmashauri, wale Madiwani na hawa watendaji. Ndiyo ushauri wetu, kwa hiyo, tunaomba kwamba mapendekezo ya Serikali kama yalivyo, Wabunge wayakubali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya kuleta Muswada hapa na kufanya marekebisho ni kuondoa upungufu ambao ulikuwepo huko tulikotoka. Sasa nauliza ni upungufu gani ambao Serikali imeuona, ambao inakusudia kwenda kuuondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuna hoja moja tu; ambayo naweza nikasema, hoja zilizotajwa pale ni nyingi zinazowahusu watendaji. Sasa hicho ambacho anataka kuwaondoa hao Kamati ya Fedha, ni hoja gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama ni suala la muda, Kamati ya Fedha inakaa kila mwezi na hiyo Bodi ya Manunuzi inakaa kila baada ya miezi mitatu. Ina maana hakuna ucheleweshaji utakaotokana kwa sababu hiyo *quarter* wakikaa na Kamati ya Fedha inakaa. Kwa hiyo, narudia tena, Halmashauri zinaendeshwa kwa vikao, asifananishe Halmashauri na Wizara, *Accounting Officer* wa Halmashauri, maamuzi yote hakuna anachoweza kubadilisha bila kikao na kwa kuwepo Sheria hii hakuna tatizo lililoonekana, kupitia kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho anachokitaka sasa hivi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ni kutaka sasa kuleta mapungufu ambayo yaliweza kudhibitiwa kule katika Halmashauri. Natoa hoja kwamba ibaki kama ilivyo sasa hivi kwenye Sheria, ili kuongeza uwajibikaji na uwazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa Waheshimiwa, lakini kwa nafasi hii sasa nawahoji, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima kabisa, nataka kuomba Bunge lako Tukufu; ni muhimu sana kuepuka kuwa *referee* na mchezaji kwa wakati mmoja. Mapendekezo ambayo Serikali imeleta yana nia njema kabisa, haiwezekani Madiwani wale wale wawe *involved* kwenye *process,* lakini wakati huo huo wawe ni sehemu ya shughuli za utendaji. Hata kama huko nyuma haijawahi kutokea kama hizo *report*

anazosema, *standard practice* ulimwenguni hufanyi vyote, naomba mlifikirie tena.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hapa tulipofikia ni sehemu ya kutoa maamuzi, nadhani mmeshasikiliza pande zote mbili; mapendekezo ya Kamati, lakini pia maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Kifungu cha 20 marekebisho imeleta Kamati wanaokubaliana na hoja ya Kamati ya kuacha hii Sheria ambayo inatakiwa kubadilishwa kama ilivyo waseme ndiyo, wasiyo kubaliana na hoja hiyo waseme siyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kakunda ulitangulia kwenye kutoa hili jambo, kwa hiyo tulishalimaliza jambo hili. Kifungu cha 20 kina marekebisho ya Serikali pamoja na ya Kamati, kifungu kinaafikiwa, Waheshimiwa Wabunge naomba mkihojiwa mjibu, kifungu namba 20 kina marekebisho ya Serikali pamoja na marekebisho ya Kamati kinaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 21

*(Ibara iliyotajwa hao juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 22

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii ya 22 kulikuwa na marekebisho ya Kamati, ambayo tulileta ile *additional amendment*.

**MWENYEKITI:** Kwenye *definition* hiyo *amendment* tulipaswa kuiangalia wakati huo, nadhani ni hiyo ambayo tumesema itakuja baadaye, ama ni kitu kingine tofauti, Mheshimiwa Jitu.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hiyo hiyo moja ilikuwa ni ya *definition,* lakini ya pili ilikuwa iingie kama kifungu.

**MWENYEKITI:** Basi Mheshimiwa Mwenyekiti alishakitolea maelezo na nikasema kitawekwa baadaye. Tunaendelea Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**MHE. HAWA A. GHASIA-MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ilikuwa ni kwenye *definition* lakini kifungu chenyewe hapa ndipo ambapo ilitakiwa kingie, cha *force account*; naomba Mwanasheria wangu anisaidie. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Inavyoonekana Kamati ya Bajeti imeajiri Mwanasheria wa Kamati.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nimshukuru pia Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa kunipatia nafasi hii. Hapa ndiyo tulikuwa tumependekeza ili kupata ile dhana ya *force account* ifafanuliwe sasa kwa kuweka kifungu kidogo cha tano, ambacho kinasema:

"*The use of force account may be justified where:-*

*(a) The works are small, scattered and in remote location for which qualified construction firms are unlikely to tender at reasonable prices;*
(b) *Work is required to be carried out without disrupting on going operations; and*
*(c) There is an emergence needing immediate attention*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tulitaka tuanze na ile dhana ya tafsiri ili sasa ku-*capture* kwenye Sheria yenyewe, ni nini hasa tunachotaka kifanyike, lakini matukio ndio hayo. Kama alivyoeleza mapema Mwenyekiti, huko nyuma utaratibu huu ulikuwepo na ulifanya kazi vizuri tu na badala ya kugharamika na kuwafuta wazabuni, kwenda kwa utaratibu wa zabuni, utaratibu huu ulikuwa na manufaa sana kwa Halmashauri zetu nyingi na unatumika tu pale ambapo wao wanaona kwamba unaenda kwa hii na wala hau-*set aside* au kuweka pembeni taratibu za ununuzi kwa njia ya *tender*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hatutaweza kupata fursa ya kurudi tena kwenye kifungu cha pili ili tuwe na maana ya hili neno *force account,* lakini ukichukua hiki kifungu cha 64, ambacho kinapendekezwa kwamba iongezewe hii sehemu ya nne, hayo maneno ambayo maana yake lazima iwepo kwenye hii sheria, labda kama yatahamishiwa hapo kwenye hicho kifungu; kwa sababu kuna namna mbili tu ya kushughulika na hili. Namna moja ni ya hiki kifungu cha 64 kukifanya kisubiri mpaka tutakapoweka tafsiri ya hayo maneno, au yote haya yaingie kwa pamoja. Sasa kwa sababu ndiyo tunapitisha Sheria hapa maana yake sasa tuseme hii maana itakaa wapi, ili tujue ni kitu gani tunachokipitisha. Sasa Mwanasheria wa Kamati ya Bajeti, pendekeza ili Serikali iweze kutoa maelezo.

**MHE. ANDREW J. CHENGE :** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa vile eneo ambalo tunadhani linafaa kuipata tafsiri ya *force account* ni hapa, tuseme maneno yafuatayo; kwa kuwa na kwa kiuandishi tutasema:

*"For the purposes of this Subsection (5), force account means a process of where works are carried out by a public, semi public department or agency by using its personal and equipment; or in collaboration with any other public or private entity.* Hiyo ndiyo itakuwa tafsiri ya *force account.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge tusaidie, hii inakuwa ni (d) ama;

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa vile tuko kwenye *Section* hiyo hiyo ya 64 na 64(1),(2),(3), zinalenga masuala haya tumeanza nayo, nilikuwa nachukua ile *schedule* kwa *amendment* ile kubwa, kwenye kifungu hiki tulikuwa tunataka kisimame peke yake; lakini kilenge tu katika (5). *For the purposes of the word force account* ni s*ubsection (5),* maana maneno haya, hutayakuta mahali pengine;

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya shida tunayoipata kuhusiana na mapendekezo ya Kamati, ni kwamba hayajawahi kutumika kwenye Sheria yenyewe Sheria mama; kwa hiyo ni kitu tunakianza upya na tunakiwekea sasa tafasiri. Hata hivyo, Kanuni ya 167 ya Kanuni hizi za manunuzi inazungumza hayo mambo ya *force account.* Sasa kwa sababu tu hili suala Mheshimiwa unaliona limeanza hapa, tunashauri kwamba, haya mapendekezo wanayoyapendekeza Waheshimiwa Wabunge kwenye Kamati, sisi tuyapokee, lakini tuyafikirie kuyaweka na kuboresha kwenye ile Kanuni ili tuwe na *scheme* ambayo ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tuki-*adopt* hiyo *force account definition* hapa, kuna uwezekano hii ikawa na *impact* pia kwenye vifungu na ikaathiri na vifungu vingine. Kwa hiyo, sisi tunaomba kuwashauri Waheshimiwa Wabunge kwamba, hoja hii tunaiona lakini iko tayari kwenye Kanuni ya 167 ya Kanuni za manunuzi ya Umma, basi mtupe fursa hii tukaiboreshe zaidi kule kama ni lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuki-*adopt* hapa jinsi ilivyo, moja iliyoletwa mara ya kwanza siyo yenyewe ambayo sasa Mheshimiwa Chenge anaisoma; kwa hiyo, tugehitaji na sisi tupate fursa twende tu-*reconcile* na vifungu vingine vya Sheria. Je, tukiisema jinsi ambavyo Waheshimiwa wanaisema, inakuwa na *impact* gani kwenye vifungu vile vingine, haitaharibu *scheme* nzima ya Sheria ile. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge sisi tunashauri kwamba, labda tulichukue sisi Serikali, halafu tulifikirie kwenye Kanuni, kwa sababu Kanuni ya 167 ya Kanuni

za Manunuzi ya Umma hii *Government Notice number* 446 mwaka 2013 inazungumzia hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndio ushauri wetu.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nieleweshwe na Serikali, hivi unaweza ukaenda kukiweka kitu kwenye kanuni ambacho kwenye sheria hakijazungumzwa kabisa. Nataja tu anisaidie Mwanasheria unaweza ukakiweka kitu kwenye kanuni ambapo kwenye sheria hakuna mahali kinazungumzwa hata kidogo, akinipa hiyo halafu baadaye ndiyo nadhani nitakuwa na maswali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti hutapewa hiyo fursa, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua hizi sheria zina maneno mengi sana. Kama kila kitu utakiandika humu ndani hutakaa utunge sheria na ndiyo maana mengine ameachiwa Waziri kwenye kanuni. Hiki kifungu cha 105 ndiyo alikopewa mamlaka *and any other thing* ambayo ataona itasababisha utekelezaji mzuri wa sheria hii na ndiyo maana tayari ameshatunga kanuni ya 167, lakini kama kwa kuboresha tu matumizi ya sheria hii hata hii anaweza kuweka *provided* kwamba *doesn't divert from the scheme* ya msingi kwenye masuala ya msingi ya ile sheria kwa sababu vinginevyo watasema hii ni *ultra vires,* lakini kama wanaleta kwa kuboresha kitu, sawa. Kwa hiyo, huo ndiyo ushauri wangu sasa, kama mnapiga kura, pigeni.

**MWENYEKITI:** Kabla Mwanasheria wa Kamati ya Bajeti hujasimama, ninazo hapa zile kanuni, zenyewe zinazungumzia *Force Account,* mapendekezo ya Kamati yanazungumzia *False Account,* sasa sijajua kama ni kitu kimoja au ni vitu viwili tofauti, Serikali itusaidie turudi kwa Kamati ya Bajeti. Maana hii nyingine ni akaunti ya nguvu ama kama mimi sijaelewa vizuri, nguvu ya akaunti au kitu kama hicho, lakini hii nyingine *false* ina maana kama ile akaunti kama uwongo, tusaidie tafadhali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni *force account* ni mojawapo ya njia za manunuzi *is the one of methods of procurement,* sio matumizi ya nguvu, kwa hiyo, hii ndiyo maana yake.

**MWENYEKITI:** Samahani nisaidie ni neno lipi ndiyo liko sawasawa, *false* au *force?*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ni *force, force* hii ya kijeshi *force.*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Kamati ilipaswa kutumia *force* siyo *false*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Siyo *False*.

**MWENYEKITI:** Sawa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na nimshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kusahihisha hiyo *typo* na yako mengi tu kama nilivyosema mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya *AG*, kifungu cha 105 cha sheria hii, kifungu kidogo cha (2) ambacho ndiyo kinampatia Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na sheria hii kutengeneza kanuni. Sasa suala hili hata ukienda sasa hivi Serikali ina mapendekezo ya kuongeza vifungu viwili kwa maana fulani. *Force Account* ambayo sisi tunataka ionekane kwenye *main body* ya sheria, haipo na ndiyo maana tulikuwa tunapendekeza tu ili tuendane vizuri na *force account* iliyomo kwenye kanuni, uhalali wake tuionyeshe huku na Waziri akipenda sasa kwenda kuiboresha hiyo kanuni, atakuwa amepata uhalali wake vizuri zaidi kupitia sheria mama. Nawaombeni sana Waheshimiwa tuielewe hii, kwani ni kwa faida ya halmashauri zetu na ni kwa faida ya nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi tulionao ni kwamba, ukiweka hii jinsi inavyopendekezwa na Kamati, itafungua mlango mwingine wa ufisadi humu ndani, ndiyo tunaloogopa na ndiyo maana tuliweka kwenye kanuni kule, kwa sababu taratibu zote hizi ziko *regulated*. Serikali haiwezi kuleta hapa Muswada kwa nia mbaya, ninyi Waheshimiwa Wabunge mmesema tulikuwa na ufisadi mkubwa sana kwenye manunuzi, kulikuwa na urasimu mkubwa sana kwenye ununuzi, kulikuwa hakuna *value for money*, Serikali inaleta mapendekezo haya. Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge, wazo lenu kwenye Kamati ya Bajeti ni nzuri kabisa, lakini mtuachie hili libaki kwenye kanuni, mkileta kwa jinsi linavyopendekezwa hili litatuletea shida sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kamati imetoa mapendekezo na Serikali imetoa maelezo. Sasa nitawahoji kuhusiana na hoja ya Kamati ya kuongeza kifungu hicho kidogo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 23

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 26
Ibara ya 27

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naondoa mapendekezo yangu kwenye (a) na (c) nabakiza kwenye (b)(2) yaani badala ya neno *or* kati ya *funds and cancel* iwe *and* yaani iwe *funds and cancel* ni hayo tu.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali nadhani umeyasikia mapendekezo ya Mheshimiwa Kakunda. Mheshimiwa Kakunda wanaomba urudie.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Katika *section* 83(2)(c) kuna maneno *funds or council,* ukurasa wa 28, kifungu cha 83(2)(b)(4) *upon receipt of the notification under subsection (3), the authority shall make further declaration of the period of the debarment…*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda ngoja nikusaidie, mimi nimeiona, iko kwenye 28(2)(c) inasema: "*Require such person or tenderer to reimburse the portion of disbursed funds or cancel the portion,* sasa Mheshimiwa Kakunda anapendekeza neno *or* liwe *and*, Serikali!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumemsikiliza Mheshimiwa Kakunda nadhani tunakubali *or* iondoke, iingie *and*.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 32

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, madogo tu, hapo inahamishwa mamlaka ya Bodi kutoka Bodi kwenda kwa Katibu Mkuu. Napendekeza kwamba mamlaka hayo ya Bodi yaendelee kuwepo kama kifungu kilivyokuwa zamani, inawezekana hapo pengine huyu Mtendaji Mkuu huyu *Executive Secretary* inawezekana labda yeye ndiyo mzembe, sasa kama yeye ni mzembe isichukuliwe kwamba hilo ni tatizo la utaratibu mzima. Kwa hiyo, nafikiri kwamba. kama Katibu Mtendaji ni mzembe. basi aondolewe awe replaced lakini Mamlaka ya Bodi kufanya maamuzi yabaki pale pale, wafanye maamuzi kabla hayajakwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Kakunda, ana hoja, lakini naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba, moja ya sababu ambayo wote tulikuwa tukipiga kelele sana humu ndani ni mlolongo mrefu wa maamuzi. Kwa hiyo, hii kuipunguza kumrejeshea Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, naamini Serikali ina nia njema kabisa kwamba, sasa tumwamini na aweze kufanya kazi, anaweza anaaminiwa na Serikali kwa mambo mengi sana. Kwa hiyo, niombe tu Bunge lako tukubaliane na hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 38

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 38 cha Muswada cha marekebisho, *section* 105 inampa mamlaka Mheshimiwa Waziri ya kutengeneza kanuni, kwa hiyo, tunaomba ikimpendeza wakati anatengeneza hizo kanuni, pia aongeze na maneno *aircrafts* na lifesaving *health commodity* na naomba isomeke kama *ifuatavyo; clause 38 of the Bill is amended in section 105 subsection 2 by adding immediately after the word aircrafts appearing in paragraph (d) the following; lifesaving health commodities and equipment.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kwa sababu haya yanayopendekezwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti yalisharidhiwa na Bunge lako Tukufu, kwa hiyo na sisi tunakubali haya yaingizwe.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 39

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeelewa *concern* ya Serikali, nimeondoa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 40

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hapo tulipofika, tunaomba Kamati ya Bajeti itusaidie kwenye kile kifungu cha *force account,* ikiweke vizuri yale maneno namna ambavyo tumekubaliana hapa ndani na kikabidhi kwa Serikali.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKINGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae, mtoa hoja taarifa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma *(The Public Procurement (Amendment) Act,* 2016) kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imepita, walioafikiwa wameshinda. Katibu.

**NDG. ZAINABU A. ISSA – KATIBU MEZANI:**

(Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 Kupitia Muundo na Majukumu ya Vyombo Vinavyohusika na Michakato ya Ununuzi Ndani ya Taasisi ili Kupunguza Gharama na Kuongeza Ufanisi, Kuweka Sharti la Kisheria la Kuzingatia Viwango Vilivyoidhinishwa na Serikali katika Ununuzi wa Mahitaji ya Taasisi ili Kunufaika na Matumizi ya Viwango na Kuweka Sharti la Kisheria la Kutumia Mifumo ya Kuongeza Uwazi katika Ununuzi kwa Lengo la Kuongeza Uadilifu na Uwajibikaji).

*(A Bill for an Act to Review Institution Arrangement and Responsibilities Within Procuring Entities in Order to Reduce Cost and Increase Efficiency Set Legal Requirement on the Use of Government Approved Standard and to Set Legal Requirement Enhancing Transparency and Accountability and Procurement System and to Provide for other Related Matters).*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria wa Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri ambayo ilileta, lakini pia nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati ya Bajeti kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuboresha, lakini na Wabunge mbalimbali ambao walileta mapendekezo yao, yale yaliyopita na ambayo hayakupita, lakini yameboresha yote kwa mawazo mazuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Muswada huu sasa umeshapitishwa na Bunge na utapelekwa kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kusainiwa kama Katiba yetu inavyotaka na niwatakie kila la heri Serikali katika utekelezaji wa sheria hii, maana ililalamikiwa sana na Wabunge katika mjadala wa Bajeti tangu Bunge hili lianze. Naamini sasa fedha zile Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambazo pia Bunge hili limepitisha, bajeti ya Serikali, zitapata matumizi mazuri kwa kutumia mabadiliko haya ambayo yameletwa na ofisi yako kwa kadri Wabunge walivyoshauri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninalo tangazo moja hapa, Mheshimiwa Katibu wa Wabunge wa CCM, anawatangazia kwamba leo saa kumi jioni ukumbi wa Msekwa kutakuwa na kikao kwa maana ya *Party Caucus* ya Wabunge wa CCM, saa kumi kamili, ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, niliombwa Mwongozo leo hapa na Mheshimiwa Kangi Lugola kuhusu Serikali kutokujibu kwa kikamilifu swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, kwa Waziri wa Mambo ya Nje. Hili swali halikuwa leo, ilikuwa ni jana, lakini naona ki-*note* kinasema leo haya mambo yalitokea jana.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Jumanne, tarehe 28 Juni, katika kikao cha 52 cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola alisimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu Wabunge kutopata majibu yanayoridhisha kutoka kwa Serikali wakati Mawaziri ambao ndiyo wawakilishi wa Serikali wapo ndani ya Bunge. Mwongozo wa Mheshimiwa Kangi Lugola ulitokana na swali la nyongeza

lililoulizwa na Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib ambaye aliuliza kama ifuatavyo:-

"Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wanaoathirika zaidi ni wanachama wa CCM kwa kule Pemba, je, Serikali haioni umuhimu wa Chama hiki cha *CUF* kukifutia usajili na kuweza kupata amani ndani ya Tanzania yetu?

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alijibu swali hilo pamoja na mambo mengine kama ifuatavyo; na ndiyo maana nikasisitiza kwa Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba wanachukua sheria kali kwa kiongozi yoyote wa chama chochote kiwe cha *CUF* au chama kingine ambacho kinahatarisha ama kinachochea amani ya nchi yetu. Kuhusiana na suala la kukifutia usajili chama hiki, nadhani hayo ni mamlaka ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuona kama kuna haja hiyo kulingana na taratibu na sheria za nchi yetu zilivyo." Mwisho wa kunukuu.

Kutokana na majibu hayo ya Mheshimiwa Waziri wa mambo ya Ndani ya Nchi, ndipo Mheshimiwa Kangi Lugola aliomba Mwongozo wa Spika kwamba swali kuhusu kufutwa kwa usajili kwa chama cha *CUF* halikupata majibu sahihi kutoka kwa Serikali, alitaka kujua kama jambo hilo ni sahihi?

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 46(1) inamtaka Waziri aliyeulizwa swali, kujibu swali hilo kwa ukamilifu. Pia fasili ya (3) ya kanuni hiyo inafafanua kuwa Waziri Mkuu au Waziri mwingine yeyote au Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kutoa majibu ya nyongeza kwa majibu yaliyotolewa na Waziri. Kama nilivyonukuu hapo juu, swali la nyongeza la Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib lililohusu kukifutia usajili Chama cha *CUF,* lilijibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambaye alieleza kwamba suala hilo liko chini ya Mamlaka ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Aidha, mchakato wa kufuta usajili wa Vyama vya Siasa huzingatia taratibu na sheria za nchi. Hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 45(3) naridhika kuwa jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, lilikuwa sahihi. *(Makofi)*

Huo ndiyo Mwongozo wa Spika kuhusu jambo hilo. Baada ya kuyasema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho siku ya Alhamisi, tarehe 30, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 8.25 Mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 30 Juni, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*